## SURA YA 2

# KATIBA YA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA YA MWAKA 1977

## YALIYOMO

*Kifungu* *Jina*

## UTANGULIZI


SURA YA KWANZA
JAMHURI YA MUUNGANO, VYAMA VYA SIASA, WATU NA SIASA YA UJAMAA NA KUJITEGEMEA

SEHEMU YA KWANZA
JAMHURI YA MUUNGANO NA WATU

1. Kutangaza Jamhuri ya Muungano.
2. Eneo la Jamhuri ya Muungano.
3. Tangazo la Nchi yenye Mfumo wa vyama vingi.
4. Utekelezaji wa shughuli za Mamlaka ya Nchi.
5. Haki ya kupiga kura.

SEHEMU YA PILI
MALENGO MUHIMU NA MISINGI YA MWELEKEO WA SHUGHULI ZA SERIKALI

6. Ufafanuzi.
7. Matumizi ya masharti ya Sehemu ya Pili.
8. Serikali na watu.
9. Ujenzi wa Ujamaa na Kujitegemea.
10. Nafasi na mamlaka ya Chama.
11. Haki ya kufanya kazi, kupata elimu na nyinginezo.

SEHEMU YA TATU
HAKI NA WAJIBU MUHIMU

*Haki ya Usawa*

12. Usawa wa binadamu.
13. Usawa mbele ya Sheria.


©2025 Government of Tanzania. All rights reserved. No part of this book may be reproduced or distributed without permission of OAG.

*Haki ya Kuishi*

**14.** Haki ya kuwa hai.
**15.** Haki ya uhuru wa mtu binafsi.
**16.** Haki ya faragha na usalama wa mtu.
**17.** Uhuru wa mtu kwenda atakako.

*Haki ya Uhuru wa Mawazo*

**18.** Uhuru wa maoni.
**19.** Uhuru wa mtu kuamini dini atakayo.
**20.** Uhuru wa mtu kushirikiana na wengine.
**21.** Uhuru wa kushiriki shughuli za umma.

*Haki ya Kufanya Kazi*

**22.** Haki ya kufanya kazi.
**23.** Haki ya kupata ujira wa haki.
**24.** Haki ya kumiliki mali.

*Wajibu kwa Jamii*

**25.** Wajibu wa kushiriki kazini.
**26.** Wajibu wa kutii sheria za nchi.
**27.** Kulinda mali ya umma.
**28.** Ulinzi wa taifa.

*Masharti ya Jumla*

**29.** Haki na wajibu muhimu.
**30.** Mipaka kwa haki na uhuru na hifadhi kwa haki na wajibu.

*Madaraka ya Pekee ya Mamlaka ya Nchi*

**31.** Ukiukaji wa haki na uhuru.
**32.** Madaraka ya kutangaza hali ya hatari.

**SURA YA PILI**
**SERIKALI YA JAMHURI YA MUUNGANO**

**SEHEMU YA KWANZA**
**RAIS**

**33.** Rais wa Jamhuri ya Muungano.
**34.** Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Mamlaka yake.
**35.** Utekelezaji wa shughuli za Serikali.
**36.** Mamlaka ya kuanzisha na kuwateua watu wa kushika nafasi za madaraka.
**37.** Utekelezaji wa kazi na shughuli za Rais.

©2025 Government of Tanzania. All rights reserved. No part of this book may be reproduced or distributed without permission of OAG.

**38.** Uchaguzi wa Rais.
**39.** Sifa za mtu kuchaguliwa kuwa Rais.
**40.** Haki ya kuchaguliwa tena.
**41.** Utaratibu wa uchaguzi wa Rais.
**42.** Wakati na muda wa kushika madaraka ya Rais.
**43.** Masharti ya kazi ya Rais.
**44.** Madaraka ya kutangaza vita.
**45.** Uwezo wa kutoa msamaha.
**46.** Kinga dhidi ya mashtaka na madai.
**46A.** Bunge laweza kumshtaki Rais.
**46B.** Wajibu wa Viongozi Wakuu wa vyombo vya mamlaka ya utendaji kudumisha Muungano.

SEHEMU YA PILI
**MAKAMU WA RAIS**

**47.** Makamu mmoja wa Rais kazi na mamlaka yake.
**48.** Wakati wa Makamu wa Rais kushika madaraka.
**49.** Kiapo cha Makamu wa Rais kushika madaraka.
**50.** Muda wa Makamu wa Rais kushika madaraka.

SEHEMU YA TATU
**WAZIRI MKUU, BARAZA LA MAWAZIRI NA SERIKALI**

*Waziri Mkuu*

**51.** Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano.
**52.** Kazi na mamlaka ya Waziri Mkuu.
**53.** Uwajibikaji wa Serikali.
**53A.** Kura ya kutokuwa na imani.

*Baraza la Mawaziri na Serikali*

**54.** Baraza la Mawaziri.
**55.** Uteuzi wa Mawaziri.
**56.** Kiapo cha Mawaziri na Naibu Mawaziri.
**57.** Wakati na muda wa Mawaziri kushika Madaraka.
**58.** Masharti ya kazi ya Mawaziri.
**59.** Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano.
**59A.** Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali.
**59B.** Mkurugenzi wa Mashtaka.
**60.** Katibu wa Baraza la Mawaziri.
**61.** Wakuu wa Mikoa.

©2025 Government of Tanzania. All rights reserved. No part of this book may be reproduced or distributed without permission of OAG.

## SURA YA TATU
## BUNGE LA JAMHURI YA MUUNGANO

### SEHEMU YA KWANZA
### BUNGE

**62.** Bunge.
**63.** Madaraka ya Bunge.
**64.** Madaraka ya kutunga Sheria.
**65.** Muda wa Bunge.

### SEHEMU YA PILI
### WABUNGE, WILAYA ZA UCHAGUZI NA UCHAGUZI WA WABUNGE

*Wajumbe wa Bunge*

**66.** Wabunge.
**67.** Sifa za mtu kuwa Mbunge.
**68.** Kiapo cha Wabunge.
**69.** Tamko rasmi la Wabunge kuhusu maadili ya viongozi.
**70.** Wabunge kutoa taarifa ya mali.
**71.** Muda wa Wabunge kushika madaraka.
**72.** Watu wenye madaraka Serikalini kukoma utumishi wanapochaguliwa.
**73.** Masharti ya kazi ya Wabunge.

*Tume ya Uchaguzi*

**74.** Tume ya uchaguzi.

*Majimbo ya Uchaguzi*

**75.** Majimbo ya uchaguzi.

*Uchaguzi na Uteuzi wa Wabunge*

**76.** Uchaguzi katika majimbo ya uchaguzi.
**77.** Utaratibu wa uchaguzi wa Wabunge wa Majimbo ya uchaguzi.
**78.** Utaratibu wa uchaguzi wa Wabunge wanawake.
**79.** Utaratibu wa uchaguzi wa Wabunge wa kuchaguliwa na Baraza la Wawakilishi.
**80.** Utaratibu wa uchaguzi wa Wabunge wa Taifa waliopendekezwa na Jumuiya za Wananchi.
**81.** Utaratibu wa Kupendekeza majina ya wagombea Uchaguzi wa Wabunge wanawake.
**82.** Wabunge wa kuteuliwa na Rais.
**83.** Uamuzi wa suala kama mtu ni Mbunge.

©2025 Government of Tanzania. All rights reserved. No part of this book may be reproduced or distributed without permission of OAG.

SEHEMU YA TATU
UTARATIBU, MADARAKA NA HAKI ZA BUNGE

*Spika na Naibu wa Spika*

**84.** Spika na Mamlaka yake.
**85.** Naibu wa Spika.
**86.** Utaratibu wa kumchagua Spika na Naibu Spika.

*Ofisi ya Bunge*

**87.** Katibu wa Bunge.
**88.** Sekretarieti ya Bunge.

*Utaratibu wa shughuli Bungeni*

**89.** Kanuni za Kudumu za Bunge.
**90.** Kuitishwa kwa mikutano ya Bunge na kuvunjwa kwa Bunge.
**91.** Rais aweza kulihutubia Bunge.
**92.** Mikutano ya Bunge.
**93.** Uongozi wa Vikao vya Bunge.
**94.** Akidi ya Vikao vya Bunge.
**95.** Viti vilivyo wazi katika Bunge.
**96.** Kamati za Bunge.

*Utaratibu wa Kutunga Sheria*

**97.** Namna ya kutumia madaraka ya kutunga Sheria.
**98.** Utaratibu wa kubadilisha Katiba hii na baadhi ya Sheria.
**99.** Utaratibu wa kutunga sheria kuhusu mambo ya fedha.

*Madaraka na Haki za Bunge*

**100.** Uhuru wa majadiliano na utaratibu wa shughuli.
**101.** Kuhifadhi na kutilia nguvu uhuru wa majadiliano na wa shughuli.

SURA YA NNE
SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR, BARAZA LA MAPINDUZI LA ZANZIBAR NA BARAZA LA WAWAKILISHI LA ZANZIBAR

SEHEMU YA KWANZA
SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR NA RAIS WA ZANZIBAR

**102.** Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Mamlaka yake.
**103.** Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Mamlaka yake.
**104.** Uchaguzi wa Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.


©2025 Government of Tanzania. All rights reserved. No part of this book may be reproduced or distributed without permission of OAG.

SEHEMU YA PILI
BARAZA LA MAPINDUZI LA ZANZIBAR

**105.** Baraza la Mapinduzi la Zanzibar na Kazi zake.

SEHEMU YA TATU
BARAZA LA WAWAKILISHI LA ZANZIBAR

**106.** Baraza la Wawakilishi Zanzibar na madaraka ya kutunga sheria za Zanzibar.
**107.** Madaraka ya Baraza la Wawakilishi.

SURA YA TANO
UTOAJI HAKI KATIKA JAMHURI YA MUUNGANO, MAHAKAMA KUU YA JAMHURI YA MUUNGANO, TUME YA KUAJIRI YA MAHAKAMA YA TANZANIA BARA, MAHAKAMA KUU YA ZANZIBAR, MAHAKAMA YA RUFANI YA JAMHURI YA MUUNGANO NA MAHAKAMA MAALUM YA KATIBA YA JAMHURI YA MUUNGANO

SEHEMU YA KWANZA
UTOAJI HAKI KATIKA JAMHURI YA MUUNGANO

**107**A. Mamlaka ya utoaji haki.
**107**B. Uhuru wa Mahakama.

SEHEMU YA TATU
MAHAKAMA KUU YA JAMHURI YA MUUNGANO

**108.** Mahakama Kuu ya Jamhuri ya Muungano na Mamlaka yake.
**109.** Majaji wa Mahakama Kuu na uteuzi wao.
**110.** Muda wa Majaji wa Mahakama Kuu kushika madaraka.
**110**A. Utaratibu wa kushughulikia nidhamu ya Majaji wa Mahakama Kuu.
**111.** Kiapo cha Majaji.

SEHEMU YA TATU
TUME YA UTUMISHI WA MAHAKAMA

**112.** Tume ya Utumishi wa Mahakama.
**113.** Majukumu na Madaraka ya Tume.
**113**A. Uanachama katika Vyama vya Siasa.

SEHEMU YA NNE
MAHAKAMA KUU YA ZANZIBAR

**114.** Mahakama Kuu ya Zanzibar.
**115.** Mamlaka ya Mahakama Kuu ya Zanzibar.

©2025 Government of Tanzania. All rights reserved. No part of this book may be reproduced or distributed without permission of OAG.

SEHEMU YA TANO
MAHAKAMA YA RUFANI YA JAMHURI YA MUUNGANO

**116.** Tafsiri.
**117.** Mahakama ya Rufani ya Jamhuri ya Muungano na Mamlaka yake.
**118.** Jaji Mkuu na Majaji wa Mahakama ya Rufani na uteuzi wao.
**119.** Mamlaka ya Majaji wa Mahakama ya Rufani.
**120.** Muda wa utumishi wa Majaji wa Rufani.
**120A.** Utaratibu wa kushughulikia nidhamu ya Majaji wa Rufani.
**121.** Kiapo cha Majaji wa Mahakama ya Rufani.
**122.** Akidi ya vikao vya Mahakama ya Rufani.
**123.** Mashauri yanayoweza kuamuliwa na Jaji mmoja wa Mahakama ya Rufani.

SEHEMU YA SITA
UTARATIBU WA KUPELEKA HATI NA KUTEKELEZA MAAGIZO YALIYOMO KATIKA HATI ZILIZOTOLEWA NA MAHAKAMA

**124.** Utekelezaji wa maagizo ya Mahakama utafanywa nchini Tanzania kote.

SEHEMU YA SABA
MAHAKAMA MAALUM YA KATIBA YA JAMHURI YA MUUNGANO

**125.** Mahakama Maalum ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano.
**126.** Mamlaka ya Mahakama Maalum ya Katiba.
**127.** Muundo wa Mahakama Maalum ya Katiba.
**128.** Utaratibu katika vikao vya Mahakama Maalum ya Katiba.

SURA YA SITA
TUME YA HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA BORA NA SEKRETARIETI YA MAADILI YA VIONGOZI WA UMMA

SEHEMU YA KWANZA
TUME YA HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA BORA

**129.** Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora.
**130.** Majukumu ya Tume na taratibu za utekelezaji.
**131.** Mamlaka ya Tume na Utaratibu wa shughuli zake.

SEHEMU YA PILI
SEKRETARIETI YA MAADILI YA VIONGOZI WA UMMA

**132.** Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma.


©2025 Government of Tanzania. All rights reserved. No part of this book may be reproduced or distributed without permission of OAG.

SURA YA SABA
MASHARTI KUHUSU FEDHA ZA JAMHURI YA MUUNGANO

SEHEMU YA KWANZA
MCHANGO NA MGAWANYO WA MAPATO YA JAMHURI YA MUUNGANO

**133.** Akaunti ya Fedha ya pamoja.

**134.** Tume ya Pamoja ya Fedha.

SEHEMU YA PILI
MFUKO MKUU WA HAZINA NA FEDHA ZA JAMHURI YA MUUNGANO

**135.** Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano.

**136.** Masharti ya kutoa fedha za matumizi kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali.

**137.** Utaratibu wa kuidhinisha matumizi ya fedha zilizomo katika Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali.

**138.** Masharti ya kutoza kodi.

**139.** Utaratibu wa kuidhinisha matumizi ya fedha kabla ya Sheria za Matumizi kuanza kutumika.

**140.** Mfuko wa Matumizi ya Dharura.

**141.** Deni la Taifa.

**142.** Mishahara ya watumishi fulani wa Serikali kudhaminiwa na Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali.

**143.** Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali wa Jamhuri ya Muungano.

**144.** Kumwondoa kazini Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu.

SURA YA NANE
MADARAKA YA UMMA

**145.** Serikali za Mitaa.

**146.** Kazi za Serikali za Mitaa.

SURA YA TISA
MAJESHI YA ULINZI

**147.** Marufuku kuunda majeshi ya ulinzi yasiyo majeshi ya ulinzi ya Umma.

**148.** Madaraka ya Amiri Jeshi Mkuu.

SURA YA KUMI
MENGINEYO

**149.** Maelezo ya mambo yanayohusika na madaraka ya kazi mbalimbali zilizoanzishwa na Katiba hii.

**150.** Maelezo kuhusu utaratibu wa kukabidhi madaraka ya kazi katika utumishi wa Serikali.

©2025 Government of Tanzania. All rights reserved. No part of this book may be reproduced or distributed without permission of OAG.

**151.** Ufafanuzi.

**152.** Jina kamili la Katiba, tarehe za kuanza kutumika na matumizi ya Katiba hii.

*NYONGEZA YA KWANZA*

[Mambo ya Muungano]

***NYONGEZA YA PILI***

ORODHA YA KWANZA

*(Sheria ambazo mabadiliko yake yahitaji kuungwa mkono na theluthi mbili ya Wabunge wote)*

ORODHAYA PILI

*(Mambo ambayo mabadiliko yake yahitaji kuungwa mkono na theluthi mbili ya Wabunge wote kutoka Tanzania Bara na theluthi mbili ya Wabunge kutoka Tanzania Zanzibar)*

©2025 Government of Tanzania. All rights reserved. No part of this book may be reproduced or distributed without permission of OAG.

## SURA YA 2

# KATIBA YA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA YA MWAKA 1977

[26 Aprili, 1977]

*Sura ya 500; [Toleo la 1965.]
*Sura ya 598; [Toleo la 1965.]
Sheria Na.
14 ya 1979;
1 na 28 za 1980;
21 ya 1982;
15 ya 1984;
14 na 16 za 1990;
4 na 20 za 1992;
7 ya 1993;
7 na 34 za 1994;
12 ya 1995;
3 ya 2000;
1 ya 2005;
*TS. Na.133 ya 2001
TS. Na.150 ya 2005

## UTANGULIZI
## MISINGI YA KATIBA

Sheria Na. 15 ya1984 ib. 3

KWA KUWA SISI Wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tumeamua rasmi na kwa dhati kujenga katika nchi yetu jamii inayozingatia misingi ya uhuru, haki, udugu na amani:

Sheria Na. 1 ya 2005 ib. 3

NA KWA KUWA misingi hiyo yaweza tu kutekelezwa katika jamii yenye demokrasia, ambayo Serikali yake husimamiwa na Bunge lenye wajumbe waliochaguliwa na linalowawakilisha wananchi, na pia yenye Mahakama huru zinazotekeleza wajibu wa kutoa haki bila woga wala upendeleo wowote, na hivyo kuhakikisha kwamba haki zote za binadamu zinadumishwa na kulindwa, na wajibu wa kila mtu unatekelezwa kwa uaminifu:

KWA HIYO, BASI, KATIBA HII IMETUNGWA NA BUNGE MAALUM LA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA, kwa niaba ya Wananchi, kwa madhumuni ya kujenga jamii kama hiyo, na pia kwa ajili ya kuhakikisha

---

* Sura zilizofanyiwa urekebu mwaka, 1965.
* TS. Na. ina maana ya Tangazo la Serikali Namba.

©2025 Government of Tanzania. All rights reserved. No part of this book may be reproduced or distributed without permission of OAG.

kwamba Tanzania inaongozwa na Serikali yenye kufuata misingi ya demokrasia, ujamaa na isiyokuwa na dini.

## SURA YA KWANZA

Sheria Na
15 ya 1984 ib. 5

## JAMHURI YA MUUNGANO, VYAMA VYA SIASA, WATU NA SIASA YA UJAMAA NA KUJITEGEMEA

### SEHEMU YA KWANZA

### JAMHURI YA MUUNGANO NA WATU

Kutangaza Jamhuri ya Muungano
Sheria Na.
15 ya 1984 ib. 6

**1.** Tanzania ni nchi moja na ni Jamhuri ya Muungano.

Eneo la Jamhuri ya Muungano
Sheria Na.
15 ya 1984 ib. 6
4 ya 1992 ib. 4

**2.**–(1) Eneo la Jamhuri ya Muungano ni eneo lote la Tanzania Bara na eneo lote la Tanzania Zanzibar, na ni pamoja na sehemu yake ya bahari ambayo Tanzania inapakana nayo.

(2) Kwa ajili ya utekelezaji bora wa shughuli za Serikali ya Jamhuri ya Muungano au Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Rais aweza kuigawa Jamhuri ya Muungano katika mikoa, wilaya na maeneo mengineyo, kwa kufuata utaratibu uliowekwa na sheria au kwa mujibu wa sheria iliyotungwa na Bunge.

Isipokuwa kwamba Rais atashauriana kwanza na Rais wa Zanzibar kabla ya kuigawa Tanzania Zanzibar katika mikoa, wilaya au maeneo mengineyo.

Tangazo la Nchi yenye Mfumo wa vyama vingi
Sheria Na.
4 ya 1992 ib. 5
1 ya 2005 ib. 4

**3.**–(1) Jamhuri ya Muungano ni nchi ya kidemokrasia na ya kijamaa, isiyokuwa na dini, yenye kufuata mfumo wa vyama vingi vya siasa.

(2) Mambo yote yahusuyo uandikishaji na uendeshaji wa vyama vya siasa nchini yatasimamiwa kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii na ya sheria iliyotungwa na Bunge kwa ajili hiyo.

©2025 Government of Tanzania. All rights reserved. No part of this book may be reproduced or distributed without permission of OAG.

Utekelezaji wa shughuli za Mamlaka ya Nchi
Sheria Na. 15 ya 1984 ib. 6

**4.**–(1) Shughuli zote za Mamlaka ya Nchi katika Jamhuri ya Muungano zitatekelezwa na kudhibitiwa na vyombo viwili vyenye mamlaka ya utendaji, vyombo viwili vyenye mamlaka ya kutekeleza utoaji haki, na pia vyombo viwili vyenye mamlaka ya kutunga sheria na kusimamia utekelezaji wa shughuli za umma.

(2) Vyombo vyenye mamlaka ya utendaji vitakuwa ni Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar; vyombo vyenye mamlaka ya kutekeleza utoaji haki vitakuwa ni Mahakama ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Mahakama ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, na vyombo vyenye mamlaka ya kutunga sheria na kusimamia utekelezaji wa shughuli za umma vitakuwa ni Bunge na Baraza la Wawakilishi.

(3) Kwa ajili ya utekelezaji bora wa shughuli za umma katika Jamhuri ya Muungano, na kwa ajili ya mgawanyo wa madaraka juu ya shughuli hizo baina ya vyombo vilivyotajwa katika ibara hii, kutakuwa na Mambo ya Muungano kama yalivyoorodheshwa katika Nyongeza ya Kwanza iliyoko mwishoni mwa Katiba hii, na pia kutakuwa na mambo yasiyo ya Muungano, ambayo ni mambo mengine yote yasiyo Mambo ya Muungano.

(4) Kila chombo kilichotajwa katika ibara hii kitaundwa na kutekeleza majukumu yake kwa kufuata masharti mengine yaliyomo katika Katiba hii.

Haki ya kupiga kura
Sheria Na 15 ya 1984 ib. 6
3 ya 2000 ib. 4

**5.**–(1) Kila raia wa Tanzania aliyetimiza umri wa miaka kumi na minane anayo haki ya kupiga kura katika uchaguzi unaofanywa Tanzania na wananchi. Na haki hii itatumiwa kwa kufuata masharti ya ibara ndogo ya (2) pamoja na masharti mengineyo ya Katiba hii na ya sheria inayotumika nchini Tanzania kuhusu mambo ya uchaguzi.

(2) Bunge laweza kutunga sheria na kuweka masharti yanayoweza kuzuia raia asitumie haki ya kupiga kura kutokana na yoyote kati ya sababu zifuatazo, yaani raia huyo-

(a) kuwa na uraia wa nchi nyingine;
(b) kuwa na ugonjwa wa akili;
(c) kutiwa hatiani kwa makosa fulani ya jinai; au

©2025 Government of Tanzania. All rights reserved. No part of this book may be reproduced or distributed without permission of OAG.

(d) kukosa au kushindwa kuthibitisha au kutoa kitambulisho cha umri, uraia au uandikishwaji kama mpiga kura,

mbali na sababu hizo hakuna sababu nyingine yoyote inayoweza kumzuia raia asitumie haki ya kupiga kura.

(3) Bunge litatunga Sheria ya Uchaguzi na kuweka masharti kuhusu mambo yafuatayo-

(a) kuanzisha Daftari la Kudumu la Wapiga Kura, na kuweka utaratibu wa kurekebisha yaliyomo katika Daftari hilo;

(b) kutaja sehemu na nyakati za kuandikisha wapiga kura na kupiga kura;

(c) utaratibu wa kumwezesha mpiga kura aliyejiandikisha sehemu moja kupiga kura sehemu nyingine na kutaja masharti ya utekelezaji wa utaratibu huo; na

(d) kutaja kazi na shughuli za Tume ya Uchaguzi na utaratibu wa kila uchaguzi ambao utaendeshwa chini ya uongozi na usimamizi wa Tume ya Uchaguzi.

## SEHEMU YA PILI
## MALENGO MUHIMU NA MISINGI YA MWELEKEO WA SHUGHULI ZA SERIKALI

Ufafanuzi
Sheria Na. 15 ya 1984 ib. 6

**6.** Katika Sehemu hii ya Sura hii, isipokuwa kama maelezo yahitaji vinginevyo, neno "Serikali" maana yake ni pamoja na Serikali ya Jamhuri ya Muungano, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, serikali za mitaa na pia mtu anayetekeleza madaraka au mamlaka yoyote kwa niaba ya Serikali yoyote.

Matumizi ya masharti ya Sehemu ya Pili
Sheria Na. 15 ya 1984 ib. 6

**7.**–(1) Bila ya kujali masharti ya ibara ndogo ya (2), Serikali, vyombo vyake vyote na watu wote au mamlaka yoyote yenye kutekeleza madaraka ya utawala, madaraka ya kutunga sheria au madaraka ya utoaji haki, watakuwa na jukumu na wajibu wa kuzingatia, kutia maanani na kutekeleza masharti yote ya Sehemu hii ya Sura hii.

©2025 Government of Tanzania. All rights reserved. No part of this book may be reproduced or distributed without permission of OAG.

(2) Masharti ya Sehemu hii ya Sura hii hayatatiliwa nguvu ya kisheria na mahakama yoyote. Mahakama yoyote nchini haitakuwa na uwezo wa kuamua juu ya suala kama kutenda au kukosa kutenda jambo kwa mtu au mahakama yoyote, au kama sheria, au hukumu yoyote, inaambatana na masharti ya Sehemu hii ya Sura hii.

Serikali na watu
Sheria Na.
15 ya 1984 ib. 6

**8.**–(1) Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni Nchi inayofuata misingi ya demokrasia na haki ya kijamii, na kwa hiyo-

(a) wananchi ndio msingi wa mamlaka yote, na Serikali itapata madaraka na mamlaka yake yote kutoka kwa wananchi kwa mujibu wa Katiba hii;
(b) lengo kuu la Serikali litakuwa ni ustawi wa wananchi;
(c) Serikali itawajibika kwa wananchi;
(d) wananchi watashiriki katika shughuli za Serikali yao kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii.

(2) Muundo wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, au wa chochote kati ya vyombo vyake na uendeshaji wa shughuli zake utatekelezwa kwa kuzingatia umoja wa Jamhuri ya Muungano na haja ya kukuza umoja wa kitaifa na kudumisha heshima ya Taifa.

Ujenzi wa
Ujamaa na
Kujitegemea
Sheria Na.
15 ya 1984 ib. 6
4 ya 1992 ib. 6

**9.** Lengo la Katiba hii ni kuwezesha ujenzi wa Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar au wa chochote kati ya vyombo vyake na udugu na amani kutokana na kufuata siasa ya Ujamaa na Kujitegemea, ambayo inasisitiza utekelezaji wa misingi ya kijamaa kwa kuzingatia mazingira yaliyomo katika Jamhuri ya Muungano. Kwa hiyo, Mamlaka ya Nchi na vyombo vyake vyote vinawajibika kuelekeza sera na shughuli zake zote katika lengo la kuhakikisha-

(a) kwamba utu na haki nyinginezo zote za binadamu zinaheshimiwa na kuthaminiwa;
(b) kwamba sheria za nchi zinalindwa na kutekelezwa;
(c) kwamba shughuli za Serikali zinatekelezwa kwa njia ambazo zitahakikisha kwamba utajiri wa Taifa unaendelezwa, unahifadhiwa na unatumiwa kwa

©2025 Government of Tanzania. All rights reserved. No part of this book may be reproduced or distributed without permission of OAG.

manufaa ya wananchi wote kwa jumla na pia kuzuia mtu kumnyonya mtu mwingine;

(d) kwamba maendeleo ya uchumi wa Taifa yanakuzwa na kupangwa kwa ulinganifu na kwa pamoja;

(e) kwamba kila mtu mwenye uwezo wa kufanya kazi anafanya kazi, na kazi maana yake ni shughuli yoyote ya halali inayompatia mtu riziki yake;

(f) kwamba heshima ya binadamu inahifadhiwa na kudumishwa kwa kufuata Kanuni za Tangazo la Dunia kuhusu Haki za Binadamu;

(g) kwamba Serikali na vyombo vyake vyote vya umma vinatoa nafasi zilizo sawa kwa raia wote, wake kwa waume, bila ya kujali rangi, kabila, dini au hali ya mtu;

(h) kwamba aina zote za dhuluma, vitisho, ubaguzi, rushwa, uonevu au upendeleo zinaondolewa nchini;

(i) kwamba matumizi ya utajiri wa Taifa yanatilia mkazo maendeleo ya wananchi na hasa zaidi yanaelekezwa kwenye jitihada ya kuondosha umaskini, ujinga na maradhi;

(j) kwamba shughuli za uchumi haziendeshwi kwa njia zinazoweza kusababisha ulimbikizaji wa mali au njia kuu za uchumi katika mamlaka ya watu wachache binafsi; na

(k) kwamba nchi inatawaliwa kwa kufuata misingi ya demokrasia na Ujamaa.

Nafasi na mamlaka ya Chama
Sheria Na. 15 ya 1984 ib. 6

**10.** [Ibara ya 10 ya Katiba imefutwa na Sheria Na. 4 ya 1992].

Haki ya kufanya kazi, kupata elimu na nyinginezo
Sheria Na. 15 ya 1984 ib. 6

**11.**–(1) Mamlaka ya Nchi itaweka utaratibu unaofaa kwa ajili ya kufanikisha utekelezaji wa haki ya mtu kufanya kazi, haki ya kujipatia elimu na haki ya kupata msaada kutoka kwa jamii wakati wa uzee, maradhi au hali ya ulemavu, na katika hali nyinginezo za mtu kuwa hajiwezi. Na bila kuathiri haki hizo, Mamlaka ya Nchi itaweka utaratibu wa kuhakikisha kwamba kila mtu anaishi kwa jasho lake.

©2025 Government of Tanzania. All rights reserved. No part of this book may be reproduced or distributed without permission of OAG.

(2) Kila mtu anayo haki ya kujielimisha, na kila raia atakuwa huru kutafuta elimu katika fani anayopenda hadi kufikia upeo wowote kulingana na stahili na uwezo wake.

(3) Serikali itafanya jitihada kuhakikisha kwamba watu wote wanapata fursa sawa na za kutosha kuwawezesha kupata elimu na mafunzo ya ufundi katika ngazi zote za shule na vyuo vinginevyo vya mafunzo.

## SEHEMU YA TATU
## HAKI NA WAJIBU MUHIMU

*Haki ya Usawa*

Usawa wa binadamu Sheria Na. 15 ya 1984 ib. 6

**12.**–(1) Binadamu wote huzaliwa huru, na wote ni sawa.

(2) Kila mtu anastahili heshima ya kutambuliwa na kuthaminiwa utu wake.

Usawa mbele ya Sheria Sheria Na. 15 ya 1984 ib. 6; 4 ya 1992 ib. 6; 7 ya 1994 Fungu la 8[1][k] 3 ya 2000 ib. 5

**13.**–(1) Watu wote ni sawa mbele ya sheria, na wanayo haki, bila ya ubaguzi wowote, kulindwa na kupata haki sawa mbele ya sheria.

(2) Ni marufuku kwa sheria yoyote iliyotungwa na mamlaka yoyote katika Jamhuri ya Muungano kuweka sharti lolote ambalo ni la ubaguzi ama wa dhahiri au kwa taathira yake.

(3) Haki za raia, wajibu na maslahi ya kila mtu na jumuiya ya watu yatalindwa na kuamuliwa na mahakama na vyombo vinginevyo vya Mamlaka ya Nchi vilivyowekwa na sheria au kwa mujibu wa sheria.

(4) Ni marufuku kwa mtu yeyote kubaguliwa na mtu au mamlaka yoyote inayotekeleza madaraka yake chini ya sheria yoyote au katika utekelezaji wa kazi au shughuli yoyote ya Mamlaka ya Nchi.

(5) Kwa madhumuni ya ufafanuzi wa masharti ya ibara hii neno "kubagua" maana yake ni kutimiza haja, haki au mahitaji mengineyo kwa watu mbalimbali kwa kuzingatia utaifa wao, kabila, pahala walipotokea, maoni yao ya kisiasa, rangi, dini,

©2025 Government of Tanzania. All rights reserved. No part of this book may be reproduced or distributed without permission of OAG.

jinsia au hali yao ya maisha kwa namna ambayo watu wa aina fulani wanafanywa au kuhesabiwa kuwa dhaifu au duni na kuwekewa vikwazo au masharti ya vipingamizi ambapo watu wa aina nyingine wanatendewa tofauti au wanapewa fursa au faida iliyoko nje ya masharti au sifa za lazima, isipokuwa kwamba neno "kubagua" halitafafanuliwa kwa namna ambayo itaizuia Serikali kuchukua hatua za makusudi zenye lengo la kurekebisha matatizo mahususi katika jamii.

(6) Kwa madhumuni ya kuhakikisha usawa mbele ya sheria, Mamlaka ya Nchi itaweka taratibu zinazofaa au zinazozingatia misingi kwamba -

(a) wakati haki na wajibu kwa mtu yeyote inapohitajika kufanyiwa maamuzi na mahakama au chombo kingine chochote kinachohusika, basi mtu huyo atakuwa na haki ya kupewa fursa ya kusikilizwa kwa ukamilifu, na pia haki ya kukata rufaa au kupata nafuu nyingine ya kisheria kutokana na maamuzi ya mahakama au chombo hicho kinginecho kinachohusika;

(b) ni marufuku kwa mtu aliyeshtakiwa kwa kosa la jinai kutendewa kama mtu mwenye kosa hilo mpaka itakapothibitika kuwa anayo hatia ya kutenda kosa hilo;

(c) ni marufuku kwa mtu kuadhibiwa kwa sababu ya kitendo chochote ambacho alipokitenda hakikuwa ni kosa chini ya sheria, na pia kwamba ni marufuku kwa adhabu kutolewa ambayo ni kubwa kuliko adhabu iliyokuwapo wakati kosa linalohusika lilipotendwa;

(d) kwa ajili ya kuhifadhi haki ya usawa wa binadamu, heshima ya mtu itatunzwa katika shughuli zote zinazohusu upelelezi na uendeshaji wa mambo ya jinai na katika shughuli nyinginezo ambazo mtu anakuwa chini ya ulinzi bila uhuru, au katika kuhakikisha utekelezaji wa adhabu; na

(e) ni marufuku kwa mtu kuteswa, kuadhibiwa kinyama au kupewa adhabu zinazomtweza au kumdhalilisha.

©2025 Government of Tanzania. All rights reserved. No part of this book may be reproduced or distributed without permission of OAG.

*Haki ya Kuishi*

Haki ya kuwa hai
Sheria Na. 15 ya 1984 ib. 6

**14.** Kila mtu anayo Haki ya Kuishi na kupata kutoka katika jamii, hifadhi ya maisha yake, kwa mujibu wa sheria.

Haki ya uhuru wa mtu binafsi
Sheria Na. 15 ya 1984 ib. 6

**15.**–(1) Kila mtu anayo haki ya kuwa huru na kuishi kama mtu huru.

(2) Kwa madhumuni ya kuhifadhi haki ya mtu kuwa huru na kuishi kwa uhuru, itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote kukamatwa, kufungwa, kufungiwa, kuwekwa kizuizini, kuhamishwa kwa nguvu au kunyang'anywa uhuru wake vinginevyo, isipokuwa tu-

(a) katika hali na kwa kufuata utaratibu uliowekwa na sheria; au

(b) katika kutekeleza hukumu, amri au adhabu iliyotolewa na mahakama kutokana na shauri au na mtu kutiwa hatiani kwa kosa la jinai.

Haki ya faragha na usalama wa mtu
Sheria Na. 15 ya 1984 ib. 6

**16.**–(1) Kila mtu anastahili kuheshimiwa na kupata hifadhi kwa nafsi yake, maisha yake binafsi na familia yake na unyumba wake, na pia heshima na hifadhi ya maskani yake na mawasiliano yake ya binafsi.

(2) Kwa madhumuni ya kuhifadhi haki ya mtu kwa mujibu wa ibara hii, Mamlaka ya Nchi itaweka utaratibu wa sheria kuhusu hali, namna na kiasi ambacho haki ya mtu ya faragha na ya usalama wa nafsi yake, mali yake na maskani yake, yaweza kuingiliwa bila ya kuathiri ibara hii.

Uhuru wa mtu kwenda atakako
Sheria Na. 15 ya 1984 ib. 6

**17.**–(1) Kila raia wa Jamhuri ya Muungano anayo haki ya kwenda kokote katika Jamhuri ya Muungano na kuishi katika sehemu yoyote, kutoka nje ya nchi na kuingia, na pia haki ya kutoshurutishwa kuhama au kufukuzwa kutoka katika Jamhuri ya Muungano.

(2) Kitendo chochote cha halali au sheria yoyote yenye madhumuni ya-

(a) kupunguza uhuru wa mtu kwenda atakako na kumweka chini ya ulinzi au kifungoni; au

©2025 Government of Tanzania. All rights reserved. No part of this book may be reproduced or distributed without permission of OAG.

(b) kuweka mipaka kwa matumizi ya uhuru wa mtu kwenda anakotaka ili-
   (i) kutekeleza hukumu au amri ya mahakama;
   (ii) kumlazimisha mtu kutimiza kwanza wajibu wowote anaotakiwa na sheria nyingine kuutimiza; au
   (iii) kulinda manufaa ya umma kwa jumla au kuhifadhi maslahi fulani mahususi au maslahi ya sehemu fulani ya umma,

kitendo hicho hakitahesabiwa au sheria hiyo haitahesabiwa kuwa ni haramu au ni kinyume cha ibara hii.

*Haki ya Uhuru wa Mawazo*

Uhuru wa maoni
Sheria Na.
1 ya 2005 ib. 5

**18.** Kila mtu-
(a) anayo haki ya kupewa taarifa wakati wote kuhusu matukio mbalimbali muhimu kwa maisha na shughuli za wananchi na pia kuhusu masuala muhimu kwa jamii.
(b) anayo haki ya kutafuta, kupokea na kutoa habari bila ya kujali mipaka ya nchi;
(c) anao uhuru wa kufanya mawasiliano na haki ya kutoingiliwa katika mawasiliano yake; na
(d) anao uhuru wa kuwa na maoni na kueleza fikra zake;

Uhuru wa mtu kuamini dini atakayo
Sheria Na.
15 ya 1984 ib. 6;
4 ya 1992 ib. 9;
1 ya 2005 ib. 6

**19.**–(1) Kila mtu anastahili kuwa na uhuru wa mawazo, imani na uchaguzi katika mambo ya dini, pamoja na uhuru wa mtu kubadilisha dini au imani yake.

(2) Kazi ya kutangaza dini, kufanya ibada na kueneza dini itakuwa ni huru na jambo la hiari la mtu binafsi, na shughuli na uendeshaji wa jumuiya za dini zitakuwa nje ya shughuli za mamlaka ya nchi.

(3) Hifadhi ya haki zilizotajwa katika ibara hii itakuwa chini ya taratibu zilizowekwa na sheria ambazo ni muhimu katika jamii ya kidemokrasia kwa ajili ya usalama wa jamii, amani katika jamii, maadili ya jamii na umoja wa kitaifa.

©2025 Government of Tanzania. All rights reserved. No part of this book may be reproduced or distributed without permission of OAG.

(4) Kila palipotajwa neno "dini" katika ibara hii ifahamike kwamba maana yake ni pamoja na madhehebu ya dini, na maneno mengineyo yanayofanana au kuambatana na neno hilo nayo yatatafsiriwa kwa maana hiyo.

Uhuru wa mtu kushirikiana na wengine
Sheria Na. 15 ya 1984 ib. 6; 1 ya 2005 ib. 7

**20.**–(1) Kila mtu anao uhuru wa kukutana na watu wengine kwa hiari yake na kwa amani, kuchanganyika, kushirikiana na watu wengine, na kwa ajili hiyo kutoa mawazo yake hadharani na kuanzisha na kujiunga na vyama au mashirika yaliyoanzishwa kwa madhumuni ya kuhifadhi au kuendeleza imani au maslahi yake au maslahi mengineyo.

(2) Bila ya kujali masharti ya ibara ndogo ya (1) na ya (4), haitakuwa halali kwa chama chochote cha siasa kuandikishwa ambacho kutokana na katiba au sera yake-

(a) kinakusudia kukuza au kupigania maslahi ya-
  (i) imani au kundi lolote la dini;
  (ii) kundi lolote la kikabila, mahali watu watokeapo, rangi au jinsia; au
  (iii) eneo fulani tu katika sehemu yoyote ya Jamhuri ya Muungano;
(b) kinapigania kuvunjwa kwa Jamhuri ya Muungano;
(c) kinakubali au kupigania matumizi ya nguvu au mapambano kama njia za kufikia malengo yake ya kisiasa;
(d) kinapigania au kinakusudia kuendesha shughuli zake za kisiasa katika sehemu moja tu ya Jamhuri ya Muungano; au
(e) hakiruhusu uongozi wake kuchaguliwa kwa vipindi na kwa njia za kidemokrasia.

(3) Bunge laweza kutunga sheria inayoweka masharti yatakayohakikisha kuwa vyama vya siasa vinazingatia mipaka na vigezo vilivyowekwa na masharti ya ibara ndogo ya (2) kuhusu uhuru na haki ya watu kushirikiana na kujumuika.

(4) Itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote kulazimishwa kujiunga na chama chochote au shirika lolote au kwa chama

©2025 Government of Tanzania. All rights reserved. No part of this book may be reproduced or distributed without permission of OAG.

chochote cha siasa kukataliwa kusajiliwa kwa sababu tu ya itikadi au falsafa ya chama hicho.

Uhuru wa kushiriki shughuli za umma
Sheria Na. 15 ya 1984 ib. 6; 34 ya 1994 ib. 4

**21.**–(1) Bila ya kuathiri masharti ya ibara ya 39, ya 47 na ya 67 ya Katiba hii na ya sheria za nchi kuhusiana na masharti ya kuchagua na kuchaguliwa, au kuteua na kuteuliwa kushiriki katika shughuli za utawala wa nchi, kila raia wa Jamhuri ya Muungano anayo haki ya kushiriki katika shughuli za utawala wa nchi, ama moja kwa moja au kwa kupitia wawakilishi waliochaguliwa na wananchi kwa hiari yao, kwa kuzingatia utaratibu uliowekwa na sheria au kwa mujibu wa sheria.

(2) Kila raia anayo haki na uhuru wa kushiriki kwa ukamilifu katika kufikia uamuzi juu ya mambo yanayomhusu yeye, maisha yake au yanayolihusu Taifa.

*Haki ya Kufanya Kazi*

Haki ya kufanya kazi
Sheria Na. 15 ya 1984 ib. 6

**22.**–(1) Kila mtu anayo haki ya kufanya kazi.

(2) Kila raia anastahili fursa na haki sawa, kwa masharti ya usawa, ya kushika nafasi yoyote ya kazi na shughuli yoyote iliyo chini ya mamlaka ya nchi.

Haki ya kupata ujira wa haki
Sheria Na. 15 ya 1984 ib. 6

**23.**–(1) Kila mtu, bila ya kuwapo ubaguzi wa aina yoyote, anayo haki ya kupata ujira unaolingana na kazi yake, na watu wote wanaofanya kazi kulingana na uwezo wao watapata malipo kulingana na kiasi na sifa za kazi wanazozifanya.

(2) Kila mtu anayefanya kazi anastahili kupata malipo ya haki.

Haki ya kumiliki mali
Sheria Na. 15 ya 1984 ib. 6 1 ya 2005 ib. 9

**24.**–(1) Kila mtu anayo haki ya kumiliki mali, na haki ya hifadhi ya mali yake aliyonayo kwa mujibu wa sheria.

(2) Bila ya kuathiri masharti ya ibara ndogo ya (1), ni marufuku kwa mtu yeyote kunyang'anywa mali yake kwa madhumuni ya kuitaifisha au madhumuni mengineyo bila ya idhini ya sheria ambayo inaweka masharti ya kutoa fidia inayostahili.

©2025 Government of Tanzania. All rights reserved. No part of this book may be reproduced or distributed without permission of OAG.

*Wajibu wa Jamii*

Wajibu wa kushiriki kazini
Sheria Na. 15 ya 1984 ib. 6
7 ya 1994 Fungu la 8(1)(k)

**25.**–(1) Kazi pekee ndiyo huzaa utajiri wa mali katika jamii, ndilo chimbuko la ustawi wa wananchi na kipimo cha utu. Na kila mtu anao wajibu wa -

(a) kushiriki kwa kujituma na kwa uaminifu katika kazi halali na ya uzalishaji mali; na

(b) kutimiza nidhamu ya kazi na kujitahidi kufikia malengo ya uzalishaji mali ya binafsi na yale malengo ya pamoja yanayotakiwa au yaliyowekwa na sheria.

(2) Bila ya kujali masharti ya ibara ndogo ya (1), hakutakuwapo na kazi ya shuruti katika Jamhuri ya Muungano.

(3) Kwa madhumuni ya ibara hii, na katika Katiba hii kwa jumla, ifahamike kwamba kazi yoyote haitahesabiwa kuwa ni kazi ya shuruti au kazi ya kikatili au ya kutweza endapo kazi hiyo, kwa mujibu wa sheria ni-

(a) kazi inayobidi ifanywe kutokana na hukumu au amri ya mahakama;

(b) kazi inayobidi ifanywe na askari wa jeshi lolote katika kutekeleza majukumu yao;

(c) kazi ambayo mtu yeyote inabidi aifanye kutokana na kuwapo hali ya hatari au baa lolote linalotishia uhai wa ustawi wa jamii;

(d) kazi au huduma yoyote ambayo ni sehemu ya-

(i) majukumu ya kawaida ya kuhakikisha ustawi wa jamii;

(ii) ujenzi wa taifa wa lazima kwa mujibu wa sheria; na

(iii) jitihada za taifa za kutumia uwezo wa kila mtu kufanya kazi kwa ajili ya kuimarisha jamii na uchumi wa taifa na kuhakikisha maendeleo na tija ya kitaifa.

Wajibu wa kutii sheria za nchi
Sheria Na. 15 ya 1984 ib. 6

**26.**–(1) Kila mtu ana wajibu wa kufuata na kuitii Katiba hii na sheria za Jamhuri ya Muungano.

(2) Kila mtu ana haki, kwa kufuata utaratibu uliowekwa na sheria, kuchukua hatua za kisheria kuhakikisha hifadhi ya Katiba na sheria za nchi.

©2025 Government of Tanzania. All rights reserved. No part of this book may be reproduced or distributed without permission of OAG.

Kulinda mali ya umma
Sheria Na. 15 ya 1984 ib. 6

**27.**–(1) Kila mtu ana wajibu wa kulinda mali asilia ya Jamhuri ya Muungano, mali ya mamlaka ya nchi na mali yote inayomilikiwa kwa pamoja na wananchi, na pia kuiheshimu mali ya mtu mwingine.

(2) Watu wote watatakiwa na sheria kutunza vizuri mali ya mamlaka ya nchi na ya pamoja, kupiga vita aina zote za uharibifu na ubadhilifu, na kuendesha uchumi wa taifa kwa makini kama watu ambao ndio waamuzi wa hali ya baadaye ya taifa lao.

Ulinzi wa taifa
Sheria Na. 15 ya 1984 ib. 6

**28.**–(1) Kila raia ana wajibu wa kulinda, kuhifadhi na kudumisha uhuru, mamlaka, ardhi na umoja wa taifa.

(2) Bunge laweza kutunga sheria zinazofaa kwa ajili ya kuwawezesha wananchi kutumikia katika majeshi na katika ulinzi wa taifa.

(3) Mtu yeyote hatakuwa na haki ya kutia sahihi kwenye mkataba wa kukubali kushindwa vita na kulitoa taifa kwa mshindi, wala kuridhia au kutambua kitendo cha uvamizi au mgawanyiko wa Jamhuri ya Muungano au wa sehemu yoyote ya ardhi ya eneo la taifa na bila ya kuathiri Katiba hii na sheria zilizowekwa, hakuna mtu atakayekuwa na haki ya kuwazuia raia wa Jamhuri ya Muungano kupigana vita dhidi ya adui yeyote anayeshambulia nchi.

(4) Uhaini kama unavyofafanuliwa na sheria utakuwa ni kosa la juu kabisa dhidi ya Jamhuri ya Muungano.

*Masharti ya Jumla*

Haki na wajibu muhimu
Sheria Na. 15 ya 1984 ib. 6

**29.**–(1) Kila mtu katika Jamhuri ya Muungano anayo haki ya kufaidi haki za msingi za binadamu, na matokeo ya kila mtu kutekeleza wajibu wake kwa jamii, kama zilivyofafanuliwa katika ibara ya 12 hadi ya 28 za sehemu hii ya Sura hii ya Katiba.

(2) Kila mtu katika Jamhuri ya Muungano anayo haki ya kupata hifadhi sawa chini ya sheria za Jamhuri ya Muungano.

(3) Raia yeyote wa Jamhuri ya Muungano hatakuwa na haki, hadhi au cheo maalum kwa misingi ya nasaba, jadi au urithi wake.

©2025 Government of Tanzania. All rights reserved. No part of this book may be reproduced or distributed without permission of OAG.

(4) Ni marufuku kwa sheria yoyote kutoa haki, hadhi au cheo maalum kwa raia yeyote wa Jamhuri ya Muungano kwa msingi ya nasaba, jadi au urithi.

(5) Ili watu wote waweze kufaidi haki na uhuru vilivyotajwa na Katiba hii kila mtu ana wajibu wa kutenda na kuendesha shughuli zake kwa namna ambayo haitaingilia haki na uhuru wa watu wengine au maslahi ya umma.

Mipaka kwa haki na uhuru na hifadhi kwa haki na wajibu
Sheria Na. 15 ya 1984 ib. 6; 34 ya 1994 ib. 6

**30.**–(1) Haki na uhuru wa binadamu ambavyo misingi yake imeorodheshwa katika Katiba hii havitatumiwa na mtu mmoja kwa maana ambayo itasababisha kuingiliwa kati au kukatizwa kwa haki na uhuru wa watu wengine au maslahi ya umma.

(2) Ifahamike kwamba masharti yaliyomo katika Sehemu hii ya Katiba hii, yanayofafanua misingi ya haki, uhuru na wajibu wa binadamu, hayaharamishi sheria yoyote iliyotungwa wala kuzuia sheria yoyote kutungwa au jambo lolote halali kufanywa kwa mujibu wa sheria hiyo, kwa ajili ya-

(a) kuhakikisha kwamba haki na uhuru wa watu wengine au maslahi ya umma haviathiriwi na matumizi mabaya ya uhuru na haki za watu binafsi;

(b) kuhakikisha ulinzi, usalama wa jamii, amani katika jamii, maadili ya jamii, afya ya jamii, mipango ya maendeleo ya miji na vijiji, ukuzaji na matumizi ya madini au ukuzaji na uendelezaji wa mali au maslahi mengineyo yoyote kwa nia ya kukuza manufaa ya umma;

(c) kuhakikisha utekelezaji wa hukumu au amri ya mahakama iliyotolewa katika shauri lolote la madai au la jinai;

(d) kulinda sifa, haki na uhuru wa watu wengine au maisha binafsi ya watu wanohusika katika mashauri mahakamani; kuzuia kutoa habari za siri; kutunza heshima, mamlaka na uhuru wa mahakama;

(e) kuweka vizuizi, kusimamia na kudhibiti uanzishaji, uendeshaji na shughuli za vyama na mashirika ya watu binafsi nchini; au

©2025 Government of Tanzania. All rights reserved. No part of this book may be reproduced or distributed without permission of OAG.

(f) kuwezesha jambo jingine lolote kufanyika ambalo linastawisha au kuhifadhi maslahi ya taifa kwa jumla.

(3) Mtu yeyote anayedai kuwa sharti lolote katika Sehemu hii ya Sura hii au katika sheria yoyote inayohusu haki yake au wajibu kwake, limevunjwa, linavunjwa au inaelekea litavunjwa na mtu yeyote popote katika Jamhuri ya Muungano, anaweza kufungua shauri katika Mahakama Kuu.

(4) Bila ya kuathiri masharti mengineyo yaliyomo katika Katiba hii, Mahakama Kuu itakuwa na mamlaka ya kusikiliza kwa mara ya kwanza na kuamua shauri lolote lililoletwa mbele yake kwa kufuata ibara hii; na mamlaka ya nchi yaweza kuweka sheria kwa ajili ya-

(a) kusimamia utaratibu wa kufungua mashauri kwa mujibu wa ibara hii;

(b) kufafanua uwezo wa Mahakama Kuu katika kusikiliza mashauri yaliyofunguliwa chini ya ibara hii; na

(c) kuhakikisha utekelezaji bora wa madaraka ya Mahakama Kuu, hifadhi na kutilia nguvu haki, uhuru na wajibu kwa mujibu wa Katiba hii.

(5) Endapo katika shauri lolote inadaiwa kwamba sheria yoyote iliyotungwa au hatua yoyote iliyochukuliwa na Serikali au mamlaka nyingine inafuta au inakatiza haki, uhuru na wajibu muhimu zitokanazo na ibara ya 12 hadi ya 29 za Katiba hii, na Mahakama Kuu inaridhika kwamba sheria au hatua inayohusika, kwa kiwango inachopingana na Katiba ni batili au kinyume cha Katiba basi Mahakama Kuu ikiona kuwa yafaa au hali au masilahi ya jamii yahitaji hivyo, badala ya kutamka kuwa sheria au hatua hiyo ni batili, itakuwa na uwezo wa kuamua kutoa fursa kwa ajili ya Serikali au mamlaka nyingine yoyote inayohusika kurekebisha hitilafu iliyopo katika sheria inayotuhumiwa au hatua inayohusika katika muda na kwa jinsi itakavyotajwa na Mahakama Kuu, na sheria hiyo au hatua inayohusika itaendelea kuhesabiwa kuwa ni halali hadi ama marekebisho yatakapofanywa au muda uliowekwa na Mahakama Kuu utakapokwisha, mradi muda mfupi zaidi ndio uzingatiwe.

©2025 Government of Tanzania. All rights reserved. No part of this book may be reproduced or distributed without permission of OAG.

*Madaraka ya Pekee ya Mamlaka ya Nchi*

Ukiukaji wa haki na uhuru
Sheria Na. 15 ya 1984 ib. 6

**31.**–(1) Mbali na masharti ya ibara ya 30(2), sheria yoyote iliyotungwa na Bunge haitakuwa haramu kwa sababu tu kwamba inawezesha hatua kuchukuliwa wakati wa hali ya hatari, au wakati wa hali ya kawaida kwa watu wanaoaminika kuwa wanafanya vitendo vinavyohatarisha au kudhuru usalama wa taifa, ambazo zinakiuka masharti ya ibara ya 14 na ya 15 za Katiba hii.

(2) Ni marufuku kwa hatua zilizotajwa katika ibara ndogo ya (1) ya ibara hii kuchukuliwa kwa mujibu wa sheria yoyote wakati wa hali ya hatari, au wakati wa hali ya kawaida kwa mtu yeyote isipokuwa tu kwa kiasi ambacho ni lazima na halali kwa ajili ya kushughulikia hali iliyopo wakati wa hali ya hatari au wakati wa hali ya kawaida kushughulikia hali iliyosababishwa na mwenendo wa mtu anayehusika.

(3) Ifahamike kwamba masharti yaliyomo katika ibara hii hayataidhinisha mtu kunyang'anywa haki yake ya kuwa hai isipokuwa tu kwa kifo kama matokeo ya vitendo vya kivita.

(4) Kwa madhumuni ya ibara hii na ibara zifuatazo za Sehemu hii "wakati wa hali ya hatari" maana yake ni kipindi chochote ambapo Tangazo la Hali ya Hatari, lililotolewa na Rais kwa kutumia uwezo aliopewa katika ibara ya 32, linatumika.

Madaraka ya kutangaza hali ya hatari
Sheria Na. 15 ya 1984 ib. 6; 4 ya 1992 ib. 11

**32.**–(1) Bila ya kuathiri Katiba hii, au sheria iliyotungwa na Bunge kwa ajili hiyo, Rais aweza kutangaza hali ya hatari katika Jamhuri ya Muungano au katika sehemu yake yoyote.

(2) Rais aweza tu kutangaza kuwa kuna hali ya hatari iwapo-

(a) Jamhuri ya Muungano iko katika vita;

(b) kuna hatari hasa kwamba Jamhuri ya Muungano inakaribia kuvamiwa au kuingia katika hali ya vita;

(c) kuna hali halisi ya kuvurugika kwa amani ya jamii au kutoweka kwa usalama wa jamii katika Jamhuri ya Muungano au sehemu yake yoyote kiasi kwamba ni lazima kuchukua hatua za pekee ili kurejesha amani na usalama;

©2025 Government of Tanzania. All rights reserved. No part of this book may be reproduced or distributed without permission of OAG.

(d) kuna hatari dhahiri na kubwa, kiasi kwamba amani ya jamii itavurugika na usalama wa raia kutoweka katika Jamhuri ya Muungano au sehemu yake yoyote ambayo haiwezi kuepukika isipokuwa kwa kutumia mamlaka ya pekee;

(e) karibu kutatokea tukio la hatari au tukio la balaa au la baa la kimazingira ambalo linatishia jamii au sehemu ya jamii katika Jamhuri ya Muungano; au

(f) kuna aina nyingineyo ya hatari ambayo kwa dhahiri ni tishio kwa nchi.

(3) Endapo inatangazwa kwamba kuna hali ya hatari katika Jamhuri ya Muungano nzima au katika Tanzania Bara nzima au katika Tanzania Zanzibar nzima, Rais atatuma mara nakala ya tangazo hilo kwa Spika wa Bunge, ambaye baada ya kushauriana na Kiongozi wa shughuli za Serikali Bungeni, ataitisha mkutano wa Bunge ndani ya siku zisizozidi kumi na nne, ili kuitafakari hali ya mambo na kuamua kupitisha au kutopitisha azimio, litakaloungwa mkono na kura za wajumbe wasiopungua theluthi mbili ya wajumbe wote, la kuunga mkono tangazo la hali ya hatari lililotolewa na Rais.

(4) Bunge laweza kutunga sheria inayoweka masharti kuhusu nyakati na utaratibu ambao utawawezesha watu fulani wenye kusimamia utekelezaji wa mamlaka ya Serikali katika sehemu mahususi za Jamhuri ya Muungano kumuomba Rais kutumia madaraka aliyopewa na ibara hii kuhusiana na yoyote kati ya sehemu hizo endapo katika sehemu hizo kunatokea yoyote kati ya hali zilizotajwa katika aya ya (c), (d) na (e) za ibara ndogo ya (2) na hali hiyo haivuki mipaka ya sehemu hizo; na pia kwa ajili ya kufafanua utekelezaji wa mamlaka ya Serikali wakati wa hali ya hatari.

(5) Tangazo la hali ya hatari lililotolewa na Rais kwa mujibu wa ibara hii litakoma kutumika-

(a) endapo zitapita siku kumi na nne tangu tangazo lilipotolewa kabla ya kupitishwa azimio lililotajwa katika ibara ndogo ya (3);

©2025 Government of Tanzania. All rights reserved. No part of this book may be reproduced or distributed without permission of OAG.

(b) baada ya kupita muda wa miezi sita tangu tangazo hilo lilipotolewa; isipokuwa kwamba kikao cha Bunge chaweza, kabla ya muda wa miezi sita kupita, kuongeza mara kwa mara muda wa tangazo hilo kutumika kwa vipindi vya miezi mingine sita kwa azimio litakaloungwa mkono na kura za wajumbe wa kikao hicho wasiopungua theluthi mbili ya wajumbe wote; na

(c) wakati wowote ambapo mkutano wa Bunge utalitangua tangazo hilo kwa azimio litakaloungwa mkono na kura za wajumbe wasiopungua theluthi mbili ya wajumbe wote.

(6) Kwa madhumuni ya kuondoa mashaka juu ya ufafanuzi au utekelezaji wa masharti ya ibara hii, masharti ya sheria iliyotungwa na Bunge na ya sheria nyingine yoyote, inayohusu utangazaji wa hali ya hatari kama ilivyotajwa katika ibara hii, yatatumika tu katika sehemu ya Jamhuri ya Muungano ambapo hali hiyo ya hatari imetangazwa.

## SURA YA PILI
## SERIKALI YA JAMHURI YA MUUNGANO

### SEHEMU YA KWANZA
### RAIS

Rais wa Jamhuri ya Muungano
Sheria Na. 15 ya 1984 ib. 9

**33.**–(1) Kutakuwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano.

(2) Rais atakuwa Mkuu wa Nchi, Kiongozi wa Serikali na Amiri Jeshi Mkuu.

Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Mamlaka yake
Sheria Na. 15 ya 1984 ib. 9

**34.**–(1) Kutakuwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano ambayo itakuwa na mamlaka juu ya mambo yote ya Muungano katika Jamhuri ya Muungano, na pia juu ya mambo mengine yote yahusuyo Tanzania Bara.

(2) Mamlaka ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano yatahusu utekelezaji na hifadhi ya Katiba hii na pia mambo mengineyo yote ambayo Bunge lina mamlaka ya kuyatungia sheria.

(3) Mamlaka yote ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano juu ya mambo yote ya Muungano katika Jamhuri ya Muungano,

©2025 Government of Tanzania. All rights reserved. No part of this book may be reproduced or distributed without permission of OAG.

na pia juu ya mambo mengineyo yote yahusuyo Tanzania Bara, yatakuwa mikononi mwa Rais wa Jamhuri ya Muungano.

(4) Bila ya kuathiri masharti mengineyo ya Katiba hii, madaraka ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano yatatekelezwa ama na Rais mwenyewe moja kwa moja au kwa kukasimu madaraka hayo kwa watu wengine wenye madaraka katika utumishi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano.

(5) Ifahamike kwamba masharti yaliyomo katika ibara hii hayatahesabiwa kwamba -

(a) yanahamishia kwa Rais madaraka yoyote ya kisheria yaliyowekwa na sheria mikononi mwa mtu au mamlaka yoyote ambayo si Rais; au

(b) yanalizuia Bunge kukabidhi madaraka yoyote ya kisheria mikononi mwa mtu au watu au mamlaka yoyote ambayo si Rais.

Utekelezaji wa shughuli za Serikali
Sheria Na. 15 ya 1984 ib. 9

**35.**–(1) Shughuli zote za utendaji za Serikali ya Jamhuri ya Muungano zitatekelezwa na watumishi wa Serikali kwa niaba ya Rais.

(2) Amri na maagizo mengine yanayotolewa kwa madhumuni ya ibara hii yatathibitishwa kwa namna itakavyoelezwa katika kanuni zilizowekwa na Rais, kwa kuzingatia masharti ya Katiba hii.

Mamlaka ya kuanzisha na kuwateua watu wa kushika nafasi za madaraka
Sheria Na. 15 ya 1984 ib. 9; 3 ya 2000 ib. 6

**36.**–(1) Bila ya kuathiri masharti mengineyo yaliyomo katika Katiba hii na ya sheria nyingine yoyote, Rais atakuwa na mamlaka ya kuanzisha na kufuta nafasi za madaraka ya namna mbalimbali katika utumishi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano.

(2) Rais atakuwa na madaraka ya kuteua watu wa kushika nafasi za madaraka ya viongozi wanaowajibika kuweka sera za idara na taasisi za Serikali, na watendaji wakuu wanaowajibika kusimamia utekelezaji wa sera za idara na taasisi hizo katika utumishi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano, nafasi ambazo zimetajwa katika Katiba hii au katika sheria mbalimbali zilizotungwa na Bunge kwamba zitajazwa kwa uteuzi unaofanywa na Rais.

©2025 Government of Tanzania. All rights reserved. No part of this book may be reproduced or distributed without permission of OAG.

(3) Bila ya kuathiri masharti ya ibara ndogo ya (2), masharti mengineyo yaliyomo katika Katiba hii na ya sheria yoyote inayohusika, mamlaka ya kuwateua watu wengine wote wasiokuwa viongozi wala watendaji wakuu, kushika nafasi za madaraka katika utumishi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano, na pia mamlaka ya kuwapandisha vyeo watu hao, kuwaondoa katika madaraka, kuwafukuza kazi na mamlaka ya kudhibiti nidhamu ya watu waliokabidhiwa madaraka, yatakuwa mikononi mwa Tume za Utumishi na mamlaka mengineyo yaliyotajwa na kupewa madaraka kuhusu nafasi za madaraka kwa mujibu wa Katiba hii au kwa mujibu wa sheria yoyote inayohusika.

(4) Masharti ya ibara ndogo ya (2) na ya (3) hayatahesabiwa kuwa yanamzuia Rais kuchukua hatua za kudhibiti nidhamu ya watumishi na utumishi katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano.

Utekelezaji wa kazi na shughuli za Rais
Sheria Na. 15 ya 1984 ib. 9; 4 ya 1992 ib. 12; 20 ya 1992 ib. 4; 34 ya 1994 ib. 6; 1 ya 2005 ib. 9 TS. Na. 150 la 2005

**37.**–(1) Mbali na kuzingatia masharti yaliyomo katika Katiba hii, na sheria za Jamhuri ya Muungano katika utendaji wa kazi na shughuli zake, Rais atakuwa huru na hatalazimika kufuata ushauri atakaopewa na mtu yeyote, isipokuwa tu pale anapotakiwa na Katiba hii au na sheria nyingine yoyote kufanya jambo lolote kulingana na ushauri anaopewa na mtu au mamlaka yoyote.

(2) Endapo Baraza la Mawaziri litaona kuwa Rais hawezi kumudu kazi zake kwa sababu ya maradhi ya mwili au ya akili, laweza kuwasilisha kwa Jaji Mkuu azimio la kumwomba Jaji Mkuu athibitishe kwamba Rais, kwa sababu ya maradhi ya mwili au akili, hawezi kumudu kazi zake. Baada ya kupokea azimio kama hilo, Jaji Mkuu atateua Bodi ya utabibu ya watu wasiopungua watatu atakaowateua kutoka miongoni mwa mabingwa wanaotambuliwa na sheria ya matabibu ya Tanzania, na Bodi hiyo itachunguza suala hilo na kumshauri Jaji Mkuu ipasavyo, naye aweza, baada ya kutafakari ushahidi wa kitabibu kuwasilisha kwa Spika hati ya kuthibitisha kwamba Rais, kutokana na maradhi ya mwili au ya akili, hamudu kazi

©2025 Government of Tanzania. All rights reserved. No part of this book may be reproduced or distributed without permission of OAG.

zake; na iwapo Jaji Mkuu hatabatilisha tamko hilo ndani ya siku saba kutokana na Rais kupata nafuu na kurejea kazini, basi itahesabiwa kwamba kiti cha Rais ki-wazi, na yaliyomo katika ibara ndogo ya (5) yatatumika.

(3) Endapo Rais atakuwa hayupo katika Jamhuri ya Muungano au atashindwa kutekeleza majukumu yake kwa sababu nyingine yoyote, kazi na shughuli za Rais zitatekelezwa na mmojawapo wa wafuatao kwa kufuata mpangilio ufuatao, yaani -

(a) Makamu wa Rais au kama nafasi yake iwazi au kama naye hayupo au ni mgonjwa; basi;

(b) Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano.

(4) Endapo Waziri Mkuu ndiye atatekeleza kazi na shughuli za Rais kutokana na sababu kwamba Makamu wa Rais hayupo basi Waziri Mkuu ataacha kutekeleza kazi na shughuli hizo endapo lolote kati ya mambo yafuatayo litatokea mwanzo-

(a) Rais atakaporejea katika Jamhuri ya Muungano au atakapopata nafuu kutokana na maradhi na kuanza kutekeleza kazi za Rais; au

(b) Makamu wa Rais atakaporejea katika Jamhuri ya Muungano.

(5) Endapo kiti cha Rais kitakuwa wazi kutokana na Rais kufariki dunia, kujiuzulu, kupoteza sifa za uchaguzi au kutomudu kazi zake kutokana na maradhi ya mwili au kushindwa kutekeleza kazi na shughuli za Rais, basi Makamu wa Rais ataapishwa na atakuwa Rais kwa muda uliobaki katika kipindi cha miaka mitano na kwa masharti yaliyoelezwa katika ibara ya 40, kisha baada ya kushauriana na chama cha siasa anachotoka Rais atapendekeza jina la mtu atakayekuwa Makamu wa Rais na uteuzi huo utathibitishwa na Bunge kwa kura zisizopungua asilimia hamsini ya Wabunge wote.

(6) Ifahamike kwamba kiti cha Rais hakitakuwa ki-wazi na Rais hatahesabiwa kwamba hayuko katika Jamhuri ya Muungano au hawezi kumudu kazi zake endapo-

(a) atakuwa hayupo katika mji ambao ndio makao makuu ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano;

©2025 Government of Tanzania. All rights reserved. No part of this book may be reproduced or distributed without permission of OAG.

(b) atakuwa hayupo katika Jamhuri ya Muungano kwa kipindi cha muda wa saa ishirini na nne; au
(c) atakuwa ni mgonjwa lakini anatumaini kuwa atapata nafuu baada ya muda si mrefu.

(7) Iwapo kutatokea lolote kati ya mambo yaliyotajwa katika ibara ndogo ya (6) na Rais akiona kuwa inafaa kukasimu kutoa maagizo kwa maandishi ya kumteua yeyote kati ya watu waliotajwa katika aya ya (a) au ya (b) za ibara ndogo ya (3) ya ibara hii kwa ajili ya kutekeleza madaraka ya Rais wakati yeye hayupo au ni mgonjwa, na mtu huyo atakayeteuliwa atatekeleza madaraka hayo ya Rais kwa kufuata masharti yoyote yatakayowekwa na Rais; isipokuwa kwamba masharti yaliyomo katika ibara hii ndogo yafahamike kuwa hayapunguzi wala kuathiri uwezo wa Rais alionao kwa mujibu wa sheria nyingine yoyote wa kukasimu madaraka yake kwa mtu mwingine yeyote.

(8) Rais aweza, akiona inafaa kufanya hivyo, kumwagiza kwa maandishi Waziri yeyote kutekeleza kazi na shughuli zozote za Rais ambazo Rais atazitaja katika maagizo yake na Waziri aliyeagizwa hivyo kwa mujibu wa masharti ya ibara hii ndogo, atakuwa na mamlaka ya kutekeleza kazi na shughuli hizo kwa kufuata masharti yoyote yaliyowekwa na Rais, lakini bila ya kujali masharti ya sheria nyingine yoyote; isipokuwa kwamba-

(a) Rais hatakuwa na mamlaka ya kukasimu kwa Waziri kwa mujibu wa masharti ya ibara hii ndogo kazi yoyote ya Rais aliyokabidhiwa na sheria yoyote inayotokana na masharti ya mkataba wowote uliotiwa sahihi na Jamhuri ya Muungano iwapo kisheria Rais haruhusiwi kukasimu kazi hiyo kwa mtu mwingine yeyote;
(b) ifahamike kwamba maagizo yanayotolewa na Rais kwa mujibu wa masharti ya ibara hii ndogo, ya kumwagiza Waziri yeyote kutekeleza kazi yoyote ya Rais, hayatahesabiwa kwamba yanamzuia Rais kutekeleza kazi hiyo yeye mwenyewe.

©2025 Government of Tanzania. All rights reserved. No part of this book may be reproduced or distributed without permission of OAG.

(9) Kwa madhumuni ya ufafanuzi wa masharti ya ibara hii-

(a) mkutano wa Baraza la Mawaziri uliofanywa kwa ajili ya kuwasilisha kwa Jaji Mkuu azimio kuhusu hali ya afya ya Rais utahesabiwa kuwa ni mkutano halali hata kama mjumbe yeyote wa Baraza hilo hayupo au kiti chake ki-wazi, na itahesabiwa kuwa Baraza limepitisha azimio hilo ikiwa litaungwa mkono kwa kauli ya wajumbe walio wengi waliohudhuria mkutano na kupiga kura; na

(b) Rais hatahesabiwa kuwa hayupo katika Jamhuri ya Muungano kwa sababu tu ya kupitia nje ya Tanzania wakati yuko safarini kutoka sehemu moja ya Tanzania kwenda sehemu nyingine, au kwa sababu kwamba ametoa maagizo kwa mujibu wa masharti ya ibara ndogo ya (7) na maagizo hayo bado hayajabatilishwa.

(10) Bila ya kujali masharti yaliyoelezwa hapo awali katika ibara hii mtu atakayetekeleza kazi na shughuli za Rais kwa mujibu wa ibara hii hatakuwa na mamlaka ya kulivunja Bunge, kumwondoa yeyote kati ya Mawaziri katika madaraka yake, au kufuta uteuzi wowote uliofanywa na Rais.

(11) Mtu yeyote atakayetekeleza kazi na shughuli za Rais kwa mujibu wa masharti ya ibara hii kama ni Mbunge hatapoteza kiti chake katika Bunge wala hatapoteza sifa zake za kuchaguliwa kuwa Mbunge kwa sababu tu ya kutekeleza kazi na shughuli za Rais kwa mujibu wa masharti ya ibara hii.

Uchaguzi wa Rais
Sheria Na. 14 ya 1979 ib. 3; 15 ya 1984 ib. 9; 20 ya 1992 ib. 5; 34 ya 1994 ib. 7; TS. Na. 133 la 2001

**38.**–(1) Rais atachaguliwa na wananchi kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii na kwa mujibu wa sheria itakayoweka masharti kuhusu uchaguzi wa Rais ambayo itatungwa na Bunge kwa kufuata masharti ya Katiba hii.

(2) Bila ya kuathiri masharti mengineyo ya Katiba hii, kiti cha Rais kitakuwa ki-wazi, na uchaguzi wa Rais utafanyika au nafasi hiyo itajazwa vinginevyo kwa mujibu wa Katiba hii, kadri itakavyokuwa, kila mara litokeapo lolote kati ya mambo yafuatayo:

(a) baada ya Bunge kuvunjwa;

©2025 Government of Tanzania. All rights reserved. No part of this book may be reproduced or distributed without permission of OAG.

(b) baada ya Rais kujiuzulu bila ya kuvunja Bunge kwanza;
(c) baada ya Rais kupoteza sifa za kushika nafasi ya madaraka ya kuchaguliwa;
(d) baada ya Rais kushtakiwa Bungeni kwa mujibu wa Katiba hii na kuondolewa katika madaraka;
(e) baada ya kuthibitishwa kwa mujibu wa masharti ya ibara ya 37 ya Katiba hii kwamba Rais hawezi kumudu kazi na shughuli zake; au
(f) baada ya Rais kufariki.

(3) Kiti cha Rais hakitahesabiwa kuwa ki-wazi kwa sababu tu ya Bunge kupitisha hoja ya kutokuwa na imani kwa Waziri Mkuu.

Sifa za mtu kuchaguliwa kuwa Rais
Sheria Na. 15 ya 1984 ib. 9; 4 ya 1992 ib. 13; 34 ya 1994 ib. 8; 3 ya 2000 ib. 7

**39.**–(1) Mtu hatastahili kuchaguliwa kushika kiti cha Rais wa Jamhuri ya Muungano isipokuwa tu kama -
(a) ni raia wa kuzaliwa wa Jamhuri ya Muungano kwa mujibu wa Sheria ya Uraia;
(b) ametimiza umri wa miaka arobaini;
(c) ni mwanachama, na mgombea aliyependekezwa na chama cha siasa;
(d) anazo sifa za kumwezesha kuwa Mbunge au Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi; na
(e) katika kipindi cha miaka mitano kabla ya Uchaguzi Mkuu hajawahi kutiwa hatiani katika Mahakama yoyote kwa kosa lolote la kukwepa kulipa kodi yoyote ya Serikali.

(2) Bila ya kuingilia haki na uhuru wa mtu kuwa na maoni yake, kuamini dini atakayo, kushirikiana na wengine na kushiriki shughuli za umma kwa mujibu wa sheria za nchi, mtu yeyote hatakuwa na sifa za kuchaguliwa kushika kiti cha Rais wa Jamhuri ya Muungano kama si mwanachama na mgombea aliyependekezwa na chama cha siasa.

Haki ya kuchaguliwa tena
Sheria Na. 15 ya 1984 ib. 9; 34 ya 1994 ib. 9

**40.**–(1) Bila ya kuathiri masharti mengineyo yaliyomo katika ibara hii, mtu yeyote ambaye ni Rais anaweza kuchaguliwa tena kushika kiti hicho.

(2) Hakuna mtu atakayechaguliwa zaidi ya mara mbili kushika kiti cha Rais.

©2025 Government of Tanzania. All rights reserved. No part of this book may be reproduced or distributed without permission of OAG.

(3) Mtu aliyewahi kuwa Rais wa Zanzibar hatapoteza sifa za kuweza kuchaguliwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano kwa sababu tu kwamba aliwahi kushika madaraka ya Rais wa Zanzibar.

(4) Endapo Makamu wa Rais anashika kiti cha Rais kwa mujibu wa masharti ya ibara ya 37(5) kwa kipindi kinachopungua miaka mitatu ataruhusiwa kugombea nafasi ya Rais mara mbili, lakini kama akishika kiti cha Rais kwa muda wa miaka mitatu au zaidi ataruhusiwa kugombea nafasi ya Rais mara moja tu.

Utaratibu wa uchaguzi wa Rais
Sheria Na. 20 ya 1992 ib. 5; 34 ya 1994 ib. 10

**41.**–(1) Baada ya Bunge kuvunjwa au kukitokea jambo jingine lolote lililotajwa katika ibara ndogo ya (2) ya ibara ya 38 na inalazimu uchaguzi wa Rais kufanyika, kila chama cha siasa kinachopenda kushiriki katika uchaguzi wa Rais kitawasilisha kwa Tume ya Uchaguzi, kwa mujibu wa sheria, jina la mwanachama wake mmoja kinayetaka asimame kama mgombea katika uchaguzi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano na jina la mwanachama wake mwingine kinayempendekeza kwa nafasi ya Makamu wa Rais.

(2) Mapendekezo ya majina ya wagombea katika uchaguzi wa Rais yatawasilishwa kwa Tume ya Uchaguzi katika siku na saa itakayotajwa kwa mujibu wa sheria iliyotungwa na Bunge, na mtu hatakuwa amependekezwa kwa halali isipokuwa tu kama kupendekezwa kwake kunaungwa mkono na wananchi wapiga kura kwa idadi na kwa namna itakayotajwa na sheria iliyotungwa na Bunge.

(3) Endapo inapofika saa na siku iliyotajwa kwa ajili ya kuwasilisha mapendekezo ya majina ya wagombea, ni mgombea mmoja tu ambaye anapendekezwa kwa halali, Tume itawasilisha jina lake kwa wananchi, nao watapiga kura ya kumkubali au kumkataa kwa mujibu wa masharti ya ibara hii na ya sheria iliyotungwa na Bunge.

(4) Uchaguzi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano utafanywa siku itakayoteuliwa na Tume ya Uchaguzi kwa mujibu wa sheria iliyotungwa na Bunge.

©2025 Government of Tanzania. All rights reserved. No part of this book may be reproduced or distributed without permission of OAG.

(5) Mambo mengine yote yahusuyo utaratibu wa uchaguzi wa Rais yatakuwa kama itakavyofafanuliwa katika sheria iliyotungwa na Bunge kwa ajili hiyo.

(6) Mgombea yeyote wa kiti cha Rais atatangazwa kuwa amechaguliwa kuwa Rais iwapo tu amepata kura nyingi zaidi kuliko mgombea mwingine yeyote.

(7) Iwapo mgombea ametangazwa na Tume ya Uchaguzi kwamba amechaguliwa kuwa Rais kwa mujibu wa ibara hii, basi hakuna mahakama yoyote itakayokuwa na mamlaka ya kuchunguza kuchaguliwa kwake.

Wakati na muda wa kushika madaraka ya Rais
Sheria Na. 15 ya 1984 ib. 9

**42.**–(1) Rais mteule atashika madaraka ya Rais mapema iwezekanavyo baada ya kutangazwa kwamba amechaguliwa kuwa Rais, lakini kwa hali yoyote itabidi ashike madaraka kabla ya kupita siku saba.

(2) Isipokuwa kama atajiuzulu au atafariki mapema zaidi, mtu aliyechaguliwa kuwa Rais, bila ya kuathiri masharti yaliyo katika ibara ndogo ya (3), atashika kiti cha Rais kwa muda wa miaka mitano tangu siku alipochaguliwa kuwa Rais.

(3) Mtu aliyechaguliwa kuwa Rais atashika kiti cha Rais hadi-

(a) siku ambapo mtu atakayemfuatia katika kushika kiti hicho atakula kiapo cha Rais;
(b) siku ambapo atafariki dunia akiwa katika madaraka;
(c) siku atakapojiuzulu; au
(d) atakapoacha kushika kiti cha Rais kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii.

(4) Iwapo Jamhuri ya Muungano inapigana vita dhidi ya adui na Rais anaona kuwa haiwezekani kufanya uchaguzi, Bunge laweza mara kwa mara kupitisha azimio la kuongeza muda wa miaka mitano uliotajwa katika ibara ndogo ya (2) ya ibara hii isipokuwa kwamba muda wowote utakaoongezwa kila mara hautazidi miezi sita.

(5) Kila Rais mteule na kila mtu atakayeshikilia kiti cha Rais, kabla ya kushika madaraka ya Rais, ataapa mbele ya Jaji Mkuu wa Jamhuri ya Muungano kiapo cha uaminifu na kiapo

©2025 Government of Tanzania. All rights reserved. No part of this book may be reproduced or distributed without permission of OAG.

kingine chochote kinachohusika na utendaji wa kazi yake kitakachowekwa kwa mujibu wa sheria iliyotungwa na Bunge.

Masharti ya kazi ya Rais
Sheria Na. 15 ya 1984 ib. 9

**43.**–(1) Rais atalipwa mshahara na malipo mengineyo, na atakapostaafu atapokea malipo ya uzeeni, kiinua mgongo au posho, kadri itakavyoamuliwa na Bunge, na mshahara, malipo hayo mengineyo, malipo ya uzeeni na kiinua mgongo hicho, vyote vitatokana na Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano na vitatolewa kwa mujibu wa masharti ya ibara hii.

(2) Mshahara na malipo mengineyo yote ya Rais havitapunguzwa wakati Rais atakapokuwa bado ameshika madaraka yake kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii.

Madaraka ya kutangaza vita
Sheria Na. 15 ya 1984 ib. 9; 4 ya 1992 ib. 14

**44.**–(1) Bila ya kuathiri Katiba hii, au sheria yoyote iliyotungwa na Bunge kwa ajili hiyo, Rais aweza kutangaza kuwapo kwa hali ya vita kati ya Jamhuri ya Muungano na nchi yoyote.

(2) Baada ya kutoa tangazo, Rais atapeleka nakala ya tangazo hilo kwa Spika wa Bunge ambaye, baada ya kushauriana na Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni, ndani ya siku kumi na nne kuanzia tarehe ya tangazo, ataitisha mkutano wa Bunge ili kutafakari hali ya mambo na kufikiria kupitisha au kutopitisha azimio la kuunga mkono tangazo la vita lililotolewa na Rais.

Uwezo wa kutoa msamaha
Sheria Na. 15 ya 1984 ib. 9

**45.**–(1) Bila ya kuathiri masharti mengineyo yaliyomo katika ibara hii, Rais anaweza kutenda lolote kati ya mambo yafuatayo:

(a) kutoa msamaha kwa mtu yeyote aliyepatikana na hatia mbele ya mahakama kwa kosa lolote, na aweza kutoa msamaha huo ama bila ya masharti au kwa masharti, kwa mujibu wa sheria;

(b) kumwachilia kabisa au kwa muda maalum mtu yeyote aliyehukumiwa kuadhibiwa kwa ajili ya kosa lolote ili mtu huyo asitimize kabisa adhabu hiyo au asitimize adhabu hiyo wakati wa muda huo maalum;

(c) kuibadilisha adhabu yoyote aliyopewa mtu yeyote kwa kosa lolote iwe adhabu tahafifu;

©2025 Government of Tanzania. All rights reserved. No part of this book may be reproduced or distributed without permission of OAG.

(d) kufuta adhabu yote au sehemu ya adhabu yoyote aliyopewa mtu yeyote kwa ajili ya kosa lolote au kufuta adhabu yote au sehemu ya adhabu ya kutoza, au kuhozi (au kuchukua) kitu cha mtu mwenye hatia ambacho vinginevyo kingechukuliwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano.

(2) Bunge laweza kutunga sheria kwa ajili ya kuweka utaratibu utakaofuatwa na Rais katika utekelezaji wa madaraka yake kwa mujibu wa ibara hii.

(3) Masharti ya ibara hii yatatumika kwa watu waliohukumiwa na kuadhibiwa Tanzania Zanzibar na kwa adhabu zilizotolewa Tanzania Zanzibar kwa mujibu wa sheria iliyotungwa na Bunge inayotumika Tanzania Zanzibar, hali kadhalika, masharti hayo yatatumika kwa watu waliohukumiwa na kuadhibiwa Tanzania Bara kwa mujibu wa sheria.

Kinga dhidi ya mashtaka na madai
Sheria Na. 15 ya 1984 ib. 9; 20 ya 1992 ib. 7

**46.**–(1) Wakati wote Rais atakapokuwa bado ameshika madaraka yake kwa mujibu wa Katiba hii, itakuwa ni marufuku kumshitaki au kuendesha mashataka ya aina yoyote juu yake mahakamani kwa ajili ya kosa lolote la jinai.

(2) Wakati wote Rais atakapokuwa bado ameshika madaraka yake kwa mujibu wa Katiba hii, haitaruhusiwa kufungua mahakamani shauri kuhusu jambo lolote alilolitenda au alilokosa kulitenda yeye binafsi kama raia wa kawaida ama kabla au baada ya kushika madaraka ya Rais, ila tu kama angalau siku thelathini kabla ya shauri kufunguliwa mahakamani, Rais atapewa au atakuwa ametumiwa kwanza taarifa ya madai kwa maandishi kwa kufuata utaratibu uliowekwa kwa mujibu wa sheria iliyotungwa na Bunge, na taarifa hiyo ikiwa inatoa maelezo kuhusu chanzo cha shauri hilo, kiini cha madai yenyewe, jina lake na anwani ya mahali anapoishi huyo mdai na jambo hasa analodai.

(3) Isipokuwa kama ataacha kushika madaraka ya Rais kutokana na masharti ya ibara ya 46A (10), itakuwa ni marufuku kumshtaki au kufungua mahakamani shauri lolote la jinai au la kumdai mtu aliyekuwa anashika madaraka ya Rais

©2025 Government of Tanzania. All rights reserved. No part of this book may be reproduced or distributed without permission of OAG.

baada ya kuacha madaraka hayo kutokana na jambo lolote alilofanya yeye kama Rais wakati alipokuwa bado anashika madaraka ya Rais kwa mujibu wa Katiba hii.

Bunge laweza kumshtaki Rais
Sheria Na. 20 ya 1992 ib. 8; 12 ya 1995 ib. 4

**46A.**–(1) Bila ya kujali masharti ya ibara ya 46 ya Katiba hii, Bunge linaweza kupitisha azimio la kumuondoa Rais madarakani endapo itatolewa hoja ya kumshtaki Rais na ikapitishwa kwa mujibu wa masharti ya ibara hii.

(2) Bila ya kuathiri masharti mengineyo ya ibara hii, hoja yoyote ya kumshtaki Rais haitatolewa isipokuwa tu kama inadaiwa kwamba Rais -

(a) ametenda vitendo ambavyo kwa jumla vinaivunja Katiba au Sheria ya Maadili ya Viongozi wa umma;

(b) ametenda vitendo ambavyo vinakiuka maadili yanayohusu uandikishwaji wa vyama vya siasa yaliyotajwa katika ibara ya 20(2) ya Katiba, au

(c) amekuwa na mwenendo unaodhalilisha kiti cha Rais wa Jamhuri ya Muungano, na haitatolewa hoja ya namna hiyo ndani ya miezi kumi na miwili tangu hoja kama hiyo ilipotolewa na ikakataliwa na Bunge;

(3) Bunge halitapitisha hoja ya kumshtaki Rais isipokuwa tu kama-

(a) taarifa ya maandishi, iliyotiwa sahihi na kuungwa mkono na Wabunge wasiopungua asilimia ishirini ya Wabunge wote itawasilishwa kwa Spika siku thelathini kabla ya kikao ambapo hoja hiyo inakusudiwa kutolewa Bungeni, ikifafanua makosa aliyoyatenda Rais, na ikipendekeza kuwa Kamati Maalum ya Uchunguzi iundwe ili ichunguze mashtaka yaliyowasilishwa dhidi ya Rais; na

(b) wakati wowote baada ya Spika kupokea taarifa iliyotiwa sahihi na Wabunge na kujiridhisha kuwa masharti ya Katiba kwa ajili ya kuleta hoja yametimizwa, Spika atamruhusu mtoa hoja kuiwasilisha hoja hiyo, na kisha Spika atalitaka Bunge, bila ya kufanya majadiliano, lipige kura juu ya hoja ya kuunda Kamati Maalum ya

©2025 Government of Tanzania. All rights reserved. No part of this book may be reproduced or distributed without permission of OAG.

Uchunguzi na kama ikiungwa mkono na Wabunge wasiopungua theluthi mbili ya Wabunge wote, atatangaza majina ya wajumbe wa Kamati Maalum ya Uchunguzi.

(4) Kamati Maalum ya Uchunguzi, kwa madhumuni ya ibara hii, itakuwa na wajumbe wafuatao, yaani-

(a) Jaji Mkuu wa Jamhuri ya Muungano, ambaye atakuwa ndiye Mwenyekiti wa Kamati;

(b) Jaji Mkuu wa Tanzania Zanzibar; na

(c) Wajumbe saba walioteuliwa na Spika kwa mujibu wa Kanuni za Bunge na kwa kuzingatia uwiano wa uwakilishi baina ya vyama vya siasa vinavyowakilishwa Bungeni.

(5) Endapo Bunge litapitisha hoja ya kuunda Kamati Maalum ya Uchunguzi, Rais atahesabiwa kuwa hayupo kazini, kisha kazi na madaraka ya Rais yatatekelezwa kwa mujibu wa masharti ya ibara 37(3) ya Katiba hii hadi Spika atakapomfahamisha Rais juu ya azimio la Bunge kuhusiana na mashtaka yaliyotolewa dhidi yake.

(6) Ndani ya siku saba baada ya Kamati Maalum ya Uchunguzi kuundwa, itakaa, ichunguze na kuchambua mashtaka dhidi ya Rais, pamoja na kumpatia Rais fursa ya kujieleza, kwa kufuata utaratibu uliowekwa na Kanuni za Bunge.

(7) Mapema iwezekanavyo, na kwa vyovyote vile katika muda usiozidi siku tisini, Kamati Maalum ya Uchunguzi itatoa taarifa yake kwa Spika.

(8) Baada ya Spika kupokea taarifa ya Kamati Maalum ya Uchunguzi, taarifa hiyo itawasilishwa Bungeni kwa kufuata utaratibu uliowekwa na Kanuni za Bunge.

(9) Baada ya taarifa ya Kamati Maalum ya Uchunguzi kuwasilishwa kwa mujibu wa ibara ndogo ya (8), Bunge litaijadili taarifa hiyo na litampa Rais fursa ya kujieleza, na kisha, kwa kura za Wabunge wasiopungua theluthi mbili ya Wabunge wote, Bunge litapitisha azimio ama kuwa mashtaka

©2025 Government of Tanzania. All rights reserved. No part of this book may be reproduced or distributed without permission of OAG.

dhidi ya Rais yamethibitika, na kwamba hastahili kuendelea kushika kiti cha Rais, au kuwa mashtaka hayo hayakuthibitika.

(10) Endapo Bunge litapitisha azimio kuwa mashtaka dhidi ya Rais yamethibitika na kwamba hastahili kuendelea kushika kiti cha Rais, Spika atawafahamisha Rais na Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi juu ya azimio la Bunge, na hapo Rais atawajibika kujiuzulu kabla ya kuisha kwa siku ya tatu tangu Bunge lilipopitisha azimio hilo.

(11) Endapo Rais ataacha kushika kiti cha Rais kutokana na mashtaka dhidi yake kuthibitika, hatakuwa na haki ya kupata malipo yoyote ya pensheni wala kupata haki.

Wajibu wa Viongozi Wakuu wa vyombo vya mamlaka ya utendaji kudumisha Muungano Sheria Na. 12 ya 1995 ib. 5

**46B**.–(1) Bila ya kuathiri wajibu wa kila raia uliotajwa katika ibara ya 28 ya Katiba hii, viongozi wakuu wa vyombo vyenye mamlaka ya utendaji katika Jamhuri ya Muungano vilivyotajwa katika, ibara ya 4 ya Katiba hii, watawajibika, kila mmoja wao katika kutekeleza madaraka aliyopewa kwa mujibu wa Katiba hii au Katiba ya Zanzibar, 1984, kuhakikisha kuwa analinda, kuimarisha na kudumisha umoja wa Jamhuri ya Muungano.

(2) Kwa madhumuni ya masharti ya ibara ndogo ya (1), kila mmojawapo wa viongozi wakuu wa vyombo vyenye mamlaka ya utendaji katika Jamhuri ya Muungano kabla ya kushika madaraka yake kwa mujibu wa Katiba hii ataapa kuitetea na kudumisha umoja wa Jamhuri ya Muungano kwa mujibu wa Katiba hii.

(3) Viongozi wakuu wanaohusika na masharti ya ibara hii ni -

(a) Rais wa Jamhuri ya Muungano;

(b) Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano;

(c) Rais wa Zanzibar, na

(d) Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano.

©2025 Government of Tanzania. All rights reserved. No part of this book may be reproduced or distributed without permission of OAG.

## SEHEMU YA PILI
## MAKAMU WA RAIS

Makamu mmoja wa Rais kazi na mamlaka yake
Sheria Na. 34 ya 1994 ib. 11; 3 ya 2000 ib. 9

**47.**–(1) Kutakuwa na Makamu wa Rais ambaye atakuwa ndiye Msaidizi Mkuu wa Rais kuhusu mambo yote ya Jamhuri ya Muungano kwa jumla, na hususan-

(a) atamsaidia Rais katika kufuatilia utekelezaji wa siku hata siku wa Mambo ya Muungano;

(b) atafanya kazi zote atakazoagizwa na Rais; na

(c) atafanya kazi zote za Rais kama Rais hayuko kazini au yuko nje ya nchi.

(2) Bila ya kuathiri masharti ya ibara ya 37(5), Makamu wa Rais atapatikana kwa kuchaguliwa katika uchaguzi ule ule kwa pamoja na Rais, baada ya kupendekezwa na chama chake wakati ule ule anapopendekezwa mgombea kiti cha Rais na watapigiwa kura kwa pamoja. Mgombea kiti cha Rais akichaguliwa basi na Makamu wa Rais atakuwa amechaguliwa.

(3) Mtu atateuliwa kugombea kiti cha Makamu wa Rais kwa kufuata kanuni kwamba endapo Rais wa Jamhuri ya Muungano atatoka sehemu moja ya Muungano, basi Makamu wa Rais atakuwa ni mtu anayetoka sehemu ya pili ya Muungano.

(4) Mtu hatateuliwa kugombea au kushika kiti cha Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano isipokuwa tu kama-

(a) ni raia wa kuzaliwa wa Jamhuri ya Muungano kwa mujibu wa sheria ya Uraia;

(b) ametimiza umri wa miaka arobaini;

(c) ni mwanachama na mgombea aliyependekezwa na Chama cha Siasa;

(d) anazo sifa za kumwezesha kuwa Mbunge au Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi; na

(e) katika kipindi cha miaka mitano kabla ya tarehe ya uchaguzi hajawahi kutiwa hatiani katika Mahakama yoyote kwa kosa lolote la kukwepa kulipa kodi yoyote ya Serikali.

(5) Chama chochote hakitazuiwa kumpendekeza mtu yeyote kuwa mgombea kiti cha Makamu wa Rais kwa sababu tu

©2025 Government of Tanzania. All rights reserved. No part of this book may be reproduced or distributed without permission of OAG.

kwamba mtu huyo kwa wakati huo ameshika kiti cha Rais wa Zanzibar au kiti cha Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano.

(6) Makamu wa Rais hatakuwa kwa wakati huo huo Mbunge, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wala Rais wa Zanzibar.

(7) Endapo mtu ambaye ni Waziri Mkuu, au Rais wa Zanzibar atateuliwa au kuchaguliwa kuwa Makamu wa Rais ataacha kiti cha Waziri Mkuu, au cha Rais wa Zanzibar, kadri itakavyokuwa.

(8) Makamu wa Rais atatekeleza madaraka yake chini ya uongozi na usimamizi wa Rais, na ataongoza na kuwajibika kwa Rais kuhusu mambo au shughuli zozote atakazokabidhiwa na Rais.

Wakati wa Makamu wa Rais kushika madaraka Sheria Na. 34 ya 1994 ib. 11

**48.**–(1) Makamu wa Rais atashika madaraka ya Makamu wa Rais siku hiyo hiyo Rais anaposhika madaraka.

(2) Makamu wa Rais aliyeteuliwa kwa mujibu wa ibara ya 50(4) ataapa na kushika madaraka yake baada ya uteuzi wake kuthibitishwa na Bunge.

Kiapo cha Makamu wa Rais kushika madaraka Sheria Na. 34 ya 1994 ib. 11

**49.** Makamu wa Rais, kabla ya kushika madaraka yake ataapishwa mbele ya Jaji Mkuu wa Jamhuri ya Muungano, kiapo cha uaminifu na pia kiapo kingine chochote kinachohusika na utendaji wa kazi yake kitakachowekwa kwa mujibu wa sheria iliyotungwa na Bunge.

Muda wa Makamu wa Rais kushika madaraka Sheria Na. 15 ya 1984 ib. 9; 34 ya 1994 ib. 11; 12 ya 1995 ib. 6; 3 ya 2000 ib 10; TS. Na. 133 la 2001

**50.**–(1) Isipokuwa kama atajiuzulu au atafariki mapema zaidi, mtu aliyechaguliwa, au kuteuliwa kwa mujibu wa ibara ya 37(5), kuwa Makamu wa Rais, bila ya kuathiri masharti mengine ya ibara hii, atashika kiti cha Makamu wa Rais kwa muda wa miaka mitano tangu alipochaguliwa kuwa Makamu wa Rais.

(2) Makamu wa Rais atashika kiti hicho hadi-

(a) muda wake utakapokwisha;

(b) akifariki dunia akiwa katika madaraka;

(c) atakapojiuzulu;

©2025 Government of Tanzania. All rights reserved. No part of this book may be reproduced or distributed without permission of OAG.

(d) atakapoapishwa kuwa Rais baada ya kiti cha Rais kuwa wazi;
(e) atakapotiwa hatiani kwa kosa la jinai linaloonyesha utovu wake wa uaminifu;
(f) atakapoapishwa Rais mwingine kushika nafasi ya Rais pamoja na Makamu wake;
(g) atakapoondolewa madarakani baada ya kushtakiwa Bungeni kwa mujibu wa masharti ya ibara ndogo ya (3) ya ibara hii; au
(h) atakapoacha kushika kiti cha Makamu wa Rais vinginevyo kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii.

(3) Bunge litakuwa na madaraka ya kumuondoa Makamu wa Rais madarakani kama yale liliyonayo kuhusiana na Rais, isipokuwa kwamba hoja yoyote ya kumshtaki Makamu wa Rais itatolewa tu kama inadaiwa kwamba-
(a) Rais amewasilisha hati kwa Spika inayoeleza kwamba Makamu wa Rais ameacha au ameshindwa kutekeleza kazi za Makamu wa Rais;
(b) ametenda vitendo ambavyo kwa jumla vinaivunja Katiba au Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma;
(c) ametenda vitendo ambavyo vinakiuka maadili yanayohusu uandikishwaji wa vyama vya siasa yaliyotajwa katika ibara ya 20(2) ya Katiba; au
(d) amekuwa na mwenendo unaodhalilisha kiti cha Rais wa Jamhuri ya Muungano au kiti cha Makamu wa Rais, na haitatolewa hoja ya namna hiyo ndani ya miezi kumi na miwili tangu hoja ilipotolewa na ikakataliwa na Bunge.

(4) Ikitokea kwamba kiti cha Makamu wa Rais ki-wazi kutokana na masharti yaliyomo katika ibara ndogo ya (3), kifo au kujiuzulu, basi mapema iwezekanavyo na kwa vyovyote ndani ya siku zisizozidi kumi na nne baada ya kushika madaraka yake, Rais atamteua mtu atakayekuwa Makamu wa Rais na uteuzi huo utathibitishwa na Bunge kwa kura za Wabunge walio wengi.

©2025 Government of Tanzania. All rights reserved. No part of this book may be reproduced or distributed without permission of OAG.

(5) Masharti mengine yote ya ibara ya 46A ya Katiba yatatumika pia kuhusiana na Makamu wa Rais isipokuwa tu kwamba Makamu wa Rais aliyeondolewa tena madarakani chini ya ibara ndogo ya (3) hatakuwa na sifa za kushika nafasi ya Rais, Makamu wa Rais, Waziri Mkuu wala Rais wa Zanzibar.

## SEHEMU YA TATU
## WAZIRI MKUU, BARAZA LA MAWAZIRI NA SERIKALI

*Waziri Mkuu*

Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano Sheria Na. 20 ya 1992 ib. 9

**51.**–(1) Kutakuwa na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano atakayeteuliwa na Rais kwa kufuata masharti ya ibara hii na ambaye kabla ya kushika madaraka yake ataapa mbele ya Rais kwa kiapo kinachohusika na kiti cha Waziri Mkuu kitakachowekwa na Bunge.

(2) Mapema iwezekanavyo, na kwa vyovyote vile ndani ya siku kumi na nne, baada ya kushika madaraka yake, Rais atamteua Mbunge wa kuchaguliwa kutoka katika jimbo la uchaguzi anayetokana na chama cha siasa chenye Wabunge wengi zaidi Bungeni au, kama hakuna chama cha siasa chenye Wabunge wengi zaidi, anayeelekea kuungwa mkono na Wabunge walio wengi kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano, naye hatashika madaraka hayo mpaka kwanza uteuzi wake uwe umethibitishwa na Bunge kwa azimio litakaloungwa mkono na kura za Wabunge walio wengi.

(3) Bila ya kuathiri masharti mengineyo ya Katiba hii, Waziri Mkuu atashika kiti cha Waziri Mkuu hadi-

(a) siku ambapo Rais mteule ataapa kushika kiti chake;

(b) siku ambapo atafariki dunia akiwa katika madaraka;

(c) siku atakapojiuzulu;

(d) siku Rais atakapomteua Mbunge mwingine kuwa Waziri Mkuu; au

(e) atakapoacha kushika kiti cha Waziri Mkuu kwa mujibu wa masharti mengineyo ya Katiba hii.

©2025 Government of Tanzania. All rights reserved. No part of the book may be reproduced or distributed without permission of OAG.

Kazi na mamlaka ya Waziri Mkuu Sheria Na. 15 ya 1984 ib. 9

**52.**–(1) Waziri Mkuu atakuwa na madaraka juu ya udhibiti, usimamiaji, utekelezaji wa siku hata siku wa kazi na shughuli za Serikali ya Jamhuri ya Muungano.

(2) Waziri Mkuu atakuwa Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni.

(3) Katika utekelezaji wa madaraka yake, Waziri Mkuu atatekeleza au kusababisha utekelezaji wa jambo lolote au mambo yoyote ambayo Rais ataagiza kwamba yatekelezwe.

Uwajibikaji wa Serikali Sheria Na. 15 ya 1984 ib. 9

**53.**–(1) Bila ya kuathiri masharti ya Katiba hii, Waziri Mkuu atawajibika kwa Rais kuhusu utekelezaji wa madaraka yake.

(2) Serikali ya Jamhuri ya Muungano, chini ya mamlaka ya Rais, ndiyo itakuwa na uwezo wa kufanya maamuzi juu ya sera ya Serikali kwa jumla, na Mawaziri, chini ya uongozi wa Waziri Mkuu, watawajibika kwa pamoja Bungeni kuhusu utekelezaji wa shughuli za Serikali ya Jamhuri ya Muungano.

Kura ya kutokuwa na imani Sheria Na. 20 ya 1992 ib.10; 12 ya 1995 ib. 7

**53A.**–(1) Bila ya kujali masharti ya ibara ya 51 ya Katiba hii, Bunge linaweza kupitisha azimio la kura ya kutokuwa na imani na Waziri Mkuu endapo itatolewa hoja kupendekeza hivyo na ikapitishwa kwa mujibu wa masharti ya ibara hii.

(2) Bila ya kuathiri masharti mengineyo ya ibara hii, hoja yoyote ya kutaka kupitisha kura ya kutokuwa na imani na Waziri Mkuu haitatolewa Bungeni endapo-

(a) haina uhusiano na utekelezaji wa majukumu ya Waziri Mkuu kwa mujibu wa ibara ya 52 ya Katiba, wala hakuna madai kwamba Waziri Mkuu amevunja sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma;

(b) haijapita miezi sita tangu alipoteuliwa; au

(c) haijapita miezi tisa tangu hoja ya namna hiyo ilipotolewa Bungeni na Bunge likakataa kuipitisha.

(3) Hoja ya kura ya kutokuwa na imani na Waziri Mkuu haitapitishwa na Bunge isipokuwa tu kama-

(a) taarifa ya maandishi, iliyotiwa sahihi na kuungwa mkono na Wabunge wasiopungua asilimia ishirini ya Wabunge wote itatolewa kwa Spika, siku angalau kumi

©2025 Government of Tanzania. All rights reserved. No part of this book may be reproduced or distributed without permission of OAG.

na nne kabla ya siku inapokusudiwa kuwasilishwa Bungeni; na

(b) Spika atajiridhisha kuwa masharti ya Katiba kwa ajili ya kuleta hoja yametimizwa.

(4) Hoja iliyotimiza masharti ya ibara hii itawasilishwa Bungeni mapema iwezekanavyo kwa mujibu wa Kanuni za Bunge.

(5) Hoja ya kutokuwa na imani na Waziri Mkuu itapitishwa tu iwapo inaungwa mkono na Wabunge walio wengi.

(6) Endapo hoja ya kura ya kutokuwa na imani kwa Waziri Mkuu itaungwa mkono na Wabunge wengi, Spika atawasilisha azimio hilo kwa Rais, na mapema iwezekanavyo, na kwa vyovyote vile ndani ya siku mbili tangu Bunge lilipopitisha azimio la hoja ya kura ya kutokuwa na imani kwa Waziri Mkuu, Waziri Mkuu atatakiwa ajiuzulu, na Rais atamteua Mbunge mwingine kuwa Waziri Mkuu.

*Baraza la Mawaziri na Serikali*

Baraza la Mawaziri
Sheria Na. 15 ya 1984 ib. 9; 4 ya 1992 ib. 15; 34 ya 1994 ib. 12

**54.**–(1) Kutakuwa na Baraza la Mawaziri ambalo wajumbe wake watakuwa ni Makamu wa Rais, Waziri Mkuu, Rais wa Zanzibar na Mawaziri wote.

(2) Rais atahudhuria mikutano ya Baraza la Mawaziri na ndiye atakayeongoza mikutano hiyo. Na endapo Rais hayupo basi mikutano itaongozwa na Makamu wa Rais na kama wote wawili Rais na Makamu wa Rais hawapo Waziri Mkuu ndiye ataongoza Mikutano hiyo.

(3) Bila ya kuathiri masharti yaliyomo katika ibara ya 37(1) ya Katiba hii, Baraza la Mawaziri litakuwa ndicho chombo kikuu cha kumshauri Rais juu ya mambo yote yanayohusika na utekelezaji wa madaraka yake kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii, na litamsaidia na kumshauri Rais juu ya jambo lolote litakalowasilishwa kwenye Baraza hilo kwa mujibu wa maagizo maalum au maagizo ya jumla yatakayotolewa na Rais.

(4) Mwanasheria Mkuu wa Serikali atahudhuria mikutano yote ya Baraza la Mawaziri na atakuwa na haki zote za mjumbe

©2025 Government of Tanzania. All rights reserved. No part of this book may be reproduced or distributed without permission of OAG.

wa mikutano hiyo isipokuwa hatakuwa na haki ya kupiga kura katika mikutano hiyo.

(5) Suala kama ushauri wowote, na ni ushauri gani uliotolewa na Baraza la Mawaziri kwa Rais, halitachunguzwa katika mahakama yoyote.

Uteuzi wa Mawaziri

**55.**–(1) Mawaziri wote ambao ni wajumbe wa Baraza la Mawaziri kwa mujibu wa ibara ya 54 watateuliwa na Rais baada ya kushauriana na Waziri Mkuu.

(2) Pamoja na Mawaziri waliotajwa katika ibara ndogo ya (1), Rais aweza, baada ya kushauriana na Waziri Mkuu, kuwateua Naibu Mawaziri. Naibu Mawaziri wote hawatakuwa wajumbe wa Baraza la Mawaziri.

(3) Rais aweza kuteua idadi yoyote ya Naibu Mawaziri ambao watawasaidia Mawaziri katika utekelezaji wa kazi na shughuli zao.

(4) Mawaziri na Naibu Mawaziri wote watateuliwa kutoka miongoni mwa Wabunge.

(5) Bila ya kujali masharti ya ibara ndogo ya (1), ikitokea kwamba Rais anahitajika kumteua Waziri au Naibu Waziri baada ya Bunge kuvunjwa, basi aweza kumteua mtu yeyote ambaye alikuwa Mbunge kabla ya Bunge kuvunjwa.

Kiapo cha Mawaziri na Naibu Mawaziri
Sheria Na. 15 ya 1984 ib. 9

**56.** Waziri au Naibu Waziri hatashika madaraka yake ila mpaka awe ameapa kwanza mbele ya Rais kiapo cha uaminifu na pia kiapo kingine chochote kinachohusika na utendaji wa kazi yake kitakachowekwa kwa mujibu wa sheria iliyotungwa na Bunge.

Wakati na muda wa Mawaziri kushika Madaraka
Sheria Na. 15 ya 1984; ib. 9; 20 ya 1992; ib. 9; 20 ya 1992 ib. 11; 12 ya 1995 ib. 8

**57.**–(1) Muda wa kushika madaraka ya Waziri na Naibu Waziri utaanza tarehe atakapoteuliwa kushika madaraka hayo.

(2) Kiti cha Waziri au Naibu Waziri kitakuwa wazi litokeapo lolote kati ya mambo yafuatayo:

(a) endapo mwenye madaraka atajiuzulu au kufariki dunia;

(b) ikiwa mwenye madaraka hayo atakoma kuwa Mbunge kwa sababu yoyote isiyohusika na kuvunjwa kwa Bunge;



©2025 Government of Tanzania. All rights reserved. No part of this book may be reproduced or distributed without permission of OAG.

(c) ikiwa Rais atafuta uteuzi na kumuondoa kazini mwenye madaraka hayo;
(d) iwapo atachaguliwa kuwa Spika;
(e) iwapo Waziri Mkuu atajiuzulu au kiti chake kikiwa wazi kwa sababu nyingine yoyote;
(f) ukiwadia wakati wa Rais mteule kushika madaraka ya Rais basi mara tu kabla Rais mteule hajashika madaraka hayo; au
(g) iwapo Baraza la Maadili linatoa uamuzi unaothibitisha kwamba amevunja sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma.

Masharti ya kazi ya Mawaziri
Sheria Na. 15 ya 1984 ib. 9

**58.** Mawaziri na Naibu Mawaziri watashika madaraka yao kwa ridhaa ya Rais, na watalipwa mshahara, posho na malipo mengineyo kwa mujibu wa sheria iliyotungwa na Bunge.

Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano
Sheria Na. 15 ya 1984 ib. 9; 1 ya 2005 ib. 11

**59.**–(1) Kutakuwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano ambaye katika ibara zifuatazo za Katiba hii atatajwa tu kwa kifupi kama "Mwanasheria Mkuu" ambaye atateuliwa na Rais.

(2) Mwanasheria Mkuu atateuliwa kutoka miongoni mwa watumishi wa umma wenye sifa ya kufanya kazi za wakili au watu wenye sifa ya kusajiliwa kuwa wakili na amekuwa na sifa hizo mfululizo kwa muda usiopungua miaka kumi na tano.

(3) Mwanasheria Mkuu atakuwa ndiye mshauri wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano juu ya mambo ya sheria na, kwa ajili hiyo, atawajibika kutoa ushauri kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano kuhusu mambo yote ya kisheria, na kutekeleza shughuli nyinginezo zozote zenye asili ya au kuhusiana na sheria zitakazopelekwa kwake au atakazoagizwa na Rais kuzitekeleza, na pia kutekeleza kazi au shughuli nyinginezo zilizokabidhiwa kwake na Katiba hii au na Sheria yoyote.

(4) Katika kutekeleza kazi na shughuli zake kwa mujibu wa ibara hii, Mwanasheria Mkuu atakuwa na haki ya kuhudhuria na kusikilizwa katika mahakama zote katika Jamhuri ya Muungano.

©2025 Government of Tanzania. All rights reserved. No part of this book may be reproduced or distributed without permission of OAG.

(5) Mwanasheria Mkuu atakuwa Mbunge kutokana na wadhifa wake, na atashika madaraka yake mpaka-

(a) uteuzi wake utakapofutwa na Rais; au

(b) mara tu kabla ya Rais mteule kushika madaraka ya Rais, na atalipwa mshahara, posho na malipo mengine kwa mujibu wa sheria iliyotungwa na Bunge.

Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali
Sheria Na. 1 ya 2005 ib. 12

**59A.**–(1) Kutakuwa na Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali atakayeteuliwa na Rais kutoka miongoni mwa watu wenye sifa zilizoainishwa katika ibara ndogo ya (2) ya ibara ya 59 na amekuwa na sifa hizo mfululizo kwa muda usiopungua miaka kumi.

(2) Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali atakuwa msaidizi mkuu katika kutekeleza kazi za Mwanasheria Mkuu wa Serikali na atafanya kazi nyingine kama atakavyoelekezwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mkurugenzi wa Mashtaka
Sheria Na. 1 ya 2005 ib. 12

**59B.**–(1) Kutakuwa na Mkurugenzi wa Mashtaka ambaye atateuliwa na Rais, kutoka miongoni mwa watu wenye sifa zilizoainishwa katika ibara ndogo ya (2) ya ibara ya 59 na amekuwa na sifa hizo mfululizo kwa muda usiopungua miaka kumi.

(2) Mkurugenzi wa Mashtaka atakuwa na uwezo wa kufungua, kuendesha na kusimamia mashtaka yote nchini.

(3) Mamlaka ya Mkurugenzi wa Mashtaka kwa mujibu wa ibara ndogo ya (2) yaweza kutekelezwa na yeye mwenyewe au kwa maelekezo yake na maofisa waliopo chini yake, au wengineo wanaotekeleza kazi hizo kwa maelekezo yake.

(4) Katika kutekeleza mamlaka yake, Mkurugenzi wa Mashtaka atakuwa huru, hataingiliwa na mtu yeyote au na mamlaka yoyote na atazingatia mambo yafuatayo:

(a) nia ya kutenda haki;

(b) kuzuia matumizi mabaya ya taratibu za utoaji haki; na

(c) maslahi ya umma.

(5) Mkurugenzi wa Mashtaka atatekeleza mamlaka yake kama ilivyoelekezwa katika sheria yoyote iliyotungwa au itakayotungwa na Bunge.

©2025 Government of Tanzania. All rights reserved. No part of this book may be reproduced or distributed without permission of OAG.

Katibu wa Baraza la Mawaziri Sheria Na. 15 ya 1984 ib. 9

**60.** Kutakuwa na Katibu wa Baraza la Mawaziri ambaye atakuwa ndiye mtendaji mkuu katika Ofisi ya Baraza la Mawaziri, na atatekeleza shughuli zifuatazo kwa kufuata maagizo ya jumla au malumu atakayopewa na Rais, yaani-

(a) kuandaa ratiba ya mikutano ya Baraza na kutayarisha orodha ya shughuli za kila mkutano;

(b) kuandika na kuweka kumbukumbu za mikutano ya Baraza;

(c) kutoa taarifa na maelezo ya maamuzi ya Baraza kwa kila mtu au chombo cha umma kinachohusika na uamuzi wowote; na

(d) kutekeleza kazi na shughuli nyingine zozote atakazoagizwa mara kwa mara na Rais.

Wakuu wa Mikoa Sheria Na. 15 ya 1984 ib. 9

**61.**–(1) Kutakuwa na Mkuu wa Mkoa kwa kila mkoa katika Jamhuri ya Muungano ambaye, bila ya kuathiri ibara ndogo ya (3), atakuwa ni kiongozi katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano.

(2) Wakuu wa Mikoa katika Tanzania Bara watateuliwa na Rais baada ya kushauriana na Waziri Mkuu.

(3) Wakuu wa Mikoa katika Tanzania Zanzibar watateuliwa na Rais wa Zanzibar baada ya kushauriana na Rais.

(4) Bila ya kuathiri masharti ya ibara ndogo ya (5), kila Mkuu wa Mkoa, atakuwa na wajibu wa kusimamia utekelezaji wa kazi na shughuli zote za Serikali ya Jamhuri ya Muungano katika mkoa aliokabidhiwa; na kwa ajili hiyo, atatekeleza kazi na shughuli zote zilizotajwa na sheria, au kwa mujibu wa sheria kama ni kazi au shughuli za Mkuu wa Mkoa na atakuwa na madaraka yote yatakayotajwa na sheria yoyote iliyotungwa na Bunge.

(5) Pamoja na wajibu na madaraka yake yaliyotajwa kwenye masharti yaliyotangulia ya ibara hii, Mkuu wa Mkoa kwa mkoa wowote katika Tanzania Zanzibar atatekeleza kazi na shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar atakazokabidhiwa na Rais wa Zanzibar, na kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar, 1984, au sheria yoyote iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi.

©2025 Government of Tanzania. All rights reserved. No part of this book may be reproduced or distributed without permission of OAG.

# SURA YA TATU
# BUNGE LA JAMHURI YA MUUNGANO

## SEHEMU YA KWANZA
## BUNGE

Bunge
Sheria Na. 15 ya 1984 ib. 12

**62.**–(1) Kutakuwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano ambalo litakuwa na sehemu mbili, yaani Rais na Wabunge.

(2) Bunge litakuwa na Wajumbe wa aina zote zilizotajwa katika ibara ya 66 ya Katiba hii ambao wote wataitwa Wabunge.

(3) Iwapo jambo lolote lahitaji kuamuliwa au kutekelezwa na sehemu zote mbili za Bunge kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii au masharti ya sheria nyingine yoyote, basi jambo hilo halitahesabiwa kuwa limeamuliwa au limetekelezwa ipasavyo ila mpaka liwe limeamuliwa au limetekelezwa na Wabunge na vilevile na Rais, kwa mujibu wa madaraka yao kuhusu jambo hilo.

Madaraka ya Bunge
Sheria Na. 15 ya 1984 ib. 12; 4 ya 1992 ib. 17; 20 ya 1992 ib. 11

**63.**–(1) Rais kama sehemu moja ya Bunge atatekeleza madaraka yote aliyokabidhiwa na Katiba hii kwa ajili hiyo.

(2) Sehemu ya pili ya Bunge itakuwa ndicho chombo kikuu cha Jamhuri ya Muungano ambacho kitakuwa na madaraka, kwa niaba ya wananchi, kuisimamia na kuishauri Serikali ya Jamhuri ya Muungano na vyombo vyake vyote katika utekelezaji wa majukumu yake kwa mujibu wa Katiba hii.

(3) Kwa madhumuni ya utekelezaji wa madaraka yake Bunge laweza-

(a) kumuuliza Waziri yeyote swali lolote kuhusu mambo ya umma katika Jamhuri ya Muungano ambayo yako katika wajibu wake;

(b) kujadili utekelezaji wa kila Wizara wakati wa Mkutano wa Bunge wa kila mwaka wa bajeti;

(c) kujadili na kuidhinisha mpango wowote wa muda mrefu au wa muda mfupi unaokusudiwa kutekelezwa katika Jamhuri ya Muungano, na kutunga sheria ya kusimamia utekelezaji wa mpango huo;



©2025 Government of Tanzania. All rights reserved. No part of this book may be reproduced or distributed without permission of OAG.

(d) kutunga sheria pale ambapo utekelezaji unahitaji kuwapo sheria; na

(e) kujadili na kuridhia mikataba yote inayohusu Jamhuri ya Muungano na ambayo kwa masharti yake inahitaji kuridhiwa.

Madaraka ya kutunga Sheria. Sheria Na. 12 ya 1984 ib. 12

**64.**–(1) Mamlaka yote ya kutunga sheria juu ya mambo mengine yote yahusuyo Tanzania Bara, yatakuwa mikononi mwa Bunge.

(2) Mamlaka yoyote ya kutunga sheria katika Tanzania Zanzibar juu ya mambo yote yasiyo mambo ya Muungano yatakuwa mikononi mwa Baraza la Wawakilishi.

(3) Endapo sheria yoyote iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi inahusu jambo lolote katika Tanzania Zanzibar ambalo liko chini ya mamlaka ya Bunge, sheria hiyo itakuwa batili na itatanguka na pia endapo sheria yoyote iliyotungwa na Bunge inahusu jambo lolote ambalo liko chini ya mamlaka ya Baraza la Wawakilishi, sheria hiyo itakuwa batili na itatanguka.

(4) Sheria yoyote iliyotungwa na Bunge kuhusu jambo lolote haitatumika Tanzania Zanzibar ila kwa mujibu wa masharti yafuatayo-

(a) sheria hiyo iwe imetamka wazi kwamba itatumika Tanzania Bara na vilevile Tanzania Zanzibar au iwe inabadilisha, kurekebisha au kufuta Sheria inayotumika Tanzania Zanzibar;

(b) sheria hiyo iwe inabadilisha au kurekebisha au kufuta sheria iliyokuwa inatumika tangu zamani Tanzania Bara ambayo ilikuwa inatumika pia Tanzania Zanzibar kwa mujibu wa Mapatano ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, ya mwaka 1964, au kwa mujibu wa Sheria yoyote ambayo ilitamka wazi kwamba itatumika Tanzania Bara na vilevile Tanzania Zanzibar; au

(c) sheria hiyo iwe inahusu Mambo ya Muungano, na kila inapotajwa Tanzania katika Sheria yoyote ifahamike kuwa Sheria hiyo itatumika katika Jamhuri ya Muungano kwa mujibu wa ufafanuzi uliotolewa na masharti ya ibara hii.

©2025 Government of Tanzania. All rights reserved. No part of this book may be reproduced or distributed without permission of OAG.

(5) Bila ya kuathiri kutumika kwa Katiba ya Zanzibar kwa mujibu wa Katiba hii kuhusu mambo yote ya Tanzania Zanzibar yasiyo Mambo ya Muungano, Katiba hii itakuwa na nguvu ya sheria katika Jamhuri nzima ya Muungano na endapo sheria nyingine yoyote itakiuka masharti yaliyomo katika Katiba hii, Katiba ndiyo itakuwa na nguvu, na sheria hiyo nyingine, kwa kiasi inachokiuka Katiba, itakuwa batili.

Muda wa Bunge
Sheria Na. 15 ya 1984 ib. 12

**65.**–(1) Bila ya kuathiri masharti mengineyo ya Katiba hii, maisha ya kila Bunge yatakuwa ni muda wa miaka mitano.

(2) Kwa madhumuni ya Katiba hii maneno "maisha ya Bunge" maana yake ni ule muda wote unaoanzia tarehe ambapo Bunge jipya limeitishwa kukutana kwa mara ya kwanza baada ya Uchaguzi Mkuu na kuishia tarehe ya kuvunjwa kwa Bunge kwa ajili ya kuwezesha Uchaguzi Mkuu mwingine wa kawaida kufanyika.

## SEHEMU YA PILI
## WABUNGE, WILAYA ZA UCHAGUZI NA UCHAGUZI WA WABUNGE

*Wajumbe wa Bunge*

Wabunge
Sheria Na. 15 ya 1984 ib. 13; 4 ya 1992 ib. 18; 12 ya 1995 ib. 9; 3 ya 2000 ib. 11; 1 ya 2005 ib. 13; TS. Na. 150 la 2005

**66.**–(1) Bila ya kuathiri masharti mengineyo ya ibara hii, kutakuwa na aina zifuatazo za Wabunge, yaani-

(a) Wabunge waliochaguliwa kuwakilisha majimbo ya uchaguzi;

(b) Wabunge wanawake wa idadi isiyopungua asilimia thelathini ya wabunge wote waliotajwa katika aya za (a), (c), (d), (e) na (f) wenye sifa zilizotajwa katika ibara ya 67 watakaochaguliwa na vyama vya siasa kwa mujibu wa ibara ya 78, na kwa kuzingatia masharti ya uwiano wa kura.

(c) Wabunge watano waliochaguliwa na Baraza la Wawakilishi kutoka miongoni mwa wajumbe wake na angalau Wabunge wawili kati yao wakiwa wanawake;

(d) Mwanasheria Mkuu;

©2025 Government of Tanzania. All rights reserved. No part of this book may be reproduced or distributed without permission of OAG.

(e) Wabunge wasiozidi kumi walioteuliwa na Rais kutoka miongoni mwa watu wenye sifa zilizotajwa katika aya za (a) na (c) za ibara ya 67 na angalau Wabunge watano kati yao wakiwa wanawake; na

(f) Spika, iwapo hatakuwa amechaguliwa kutoka miongoni mwa Wabunge.

(2) Rais na Makamu wa Rais kila mmojawao hatakuwa Mbunge.

(3) Endapo Mkuu wa Mkoa atachaguliwa kuwa Mbunge anayewakilisha wilaya ya uchaguzi au endapo Mbunge anayewakilisha wilaya ya uchaguzi atateuliwa kuwa Mkuu wa Mkoa, Bunge litahesabiwa kuwa lina idadi ya Wabunge inayohitajika na shughuli zake zitakuwa halali ingawaje idadi ya jumla ya kawaida ya Wabunge kwa mujibu wa masharti ya ibara hii, itakuwa imepungua kutokana na uchaguzi huo wa Mkuu wa Mkoa au uteuzi huo wa Mbunge anayewakilisha wilaya ya uchaguzi.

Sifa za mtu kuwa Mbunge
Sheria Na. 15 ya 1984 ib. 13; 4 ya 1992 ib. 19; 34 ya 1994 ib. 13; 12 ya 1995 ib. 10; 3 ya 2000 ib. 10

**67.**–(1) Bila ya kuathiri masharti yaliyomo katika ibara hii, mtu yeyote atakuwa na sifa za kustahili kuchaguliwa au kuteuliwa kuwa Mbunge endapo-

(a) ni raia wa Jamhuri ya Muungano aliyetimiza umri wa miaka ishirini na moja, na ambaye anajua kusoma na kuandika katika Kiswahili au Kiingereza;

(b) ni mwanachama na ni mgombea aliyependekezwa na chama cha siasa; na

(c) katika kipindi cha miaka mitano kabla ya tarehe ya Uchaguzi hakuwahi kutiwa hatiani katika mahakama yoyote kwa kosa lolote la kukwepa kulipa kodi yoyote ya Serikali.

(2) Mtu hatakuwa na sifa za kustahili kuchaguliwa au kuteuliwa kuwa Mbunge-

(a) ikiwa mtu huyo anao au kwa hiari yake amejipatia uraia wa nchi nyingine yoyote;

(b) ikiwa kwa mujibu wa Sheria inayotumika katika Jamhuri ya Muungano imethibitishwa rasmi kwamba mtu huyo ana ugonjwa wa akili;

©2025 Government of Tanzania. All rights reserved. No part of this book may be reproduced or distributed without permission of OAG.

(c) ikiwa mtu huyo amehukumiwa na Mahakama yoyote katika Jamhuri ya Muungano na kupewa adhabu ya kifo au ya kufungwa gerezani kwa muda unaozidi miezi sita kwa kukutwa na hatia ya kosa lolote, vyovyote linavyoitwa, linaloambatana na utovu wa uaminifu;

(d) ikiwa katika kipindi cha miaka mitano kabla ya tarehe ya Uchaguzi Mkuu amepata kuhukumiwa na kupewa adhabu ya kifungo kwa kosa linalo ambatana na utovu wa uaminifu au kwa kuvunja Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma;

(e) bila ya kuingilia haki na uhuru wa mtu kuwa na maoni yake, kuamini dini atakayo, kushirikiana na wengine na kushiriki shughuli za umma kwa mujibu wa sheria za nchi, ikiwa mtu huyo si mwanachama na mgombea aliyependekezwa na chama cha siasa;

(f) ikiwa mtu huyo ana masilahi yoyote katika mkataba wa Serikali wa aina yoyote aliyowekewa miiko maalum kwa mujibu wa sheria iliyotungwa na Bunge, na iwapo amekiuka miiko hiyo;

(g) ikiwa mtu huyo ameshika madaraka ya afisa mwandamizi katika utumishi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano isipokuwa madaraka ambayo Rais aweza au anatakiwa kukabidhi kwa Mbunge kwa mujibu wa Katiba hii au sheria iliyotungwa na Bunge; au

(h) ikiwa kwa mujibu wa Sheria iliyotungwa na Bunge inayoshughulikia makosa yanayohusika na uchaguzi wa aina yoyote mtu huyo amezuiliwa kujiandikisha kama mpiga kura au kupiga kura katika uchaguzi wa Wabunge.

(3) Mtu hataweza kugombea uchaguzi kuwa Mbunge wa kuwakilisha jimbo la uchaguzi katika Uchaguzi Mkuu wowote ikiwa wakati huo yeye amesimama katika uchaguzi kugombea kiti cha Rais, wala hataweza kugombea uchaguzi kuwa Mbunge katika uchaguzi mdogo wowote ikiwa yeye ni Rais.

(4) Bunge laweza kutunga Sheria kwa ajili ya kuweka masharti yatakayomzuia mtu asichaguliwe kuwa Mbunge wa kuwakilisha jimbo la uchaguzi ikiwa mtu huyo ni mwenye

©2025 Government of Tanzania. All rights reserved. No part of this book may be reproduced or distributed without permission of OAG.

madaraka yanayohusika na shughuli za kuongoza au kusimamia uchaguzi wa Wabunge au shughuli za uandikishaji wa wapiga kura kwa ajili ya uchaguzi wa Wabunge; isipokuwa kwamba Sheria kama hiyo haiwezi kuweka masharti yatakayomzuia Spika wa Bunge asichaguliwe kuwa Mbunge wa kuwakilisha jimbo la uchaguzi, wala masharti yatakayosababisha mtu aliyechaguliwa kuwa Spika kupoteza kiti cha Spika au kiti chake cha kawaida katika Bunge.

(5) Bunge laweza kutunga sheria kwa ajili ya kuweka masharti yatakayomzuia mtu asichaguliwe kuwa Mbunge wa kuwakilisha jimbo la uchaguzi kwa muda wowote utakaotajwa na Bunge (ilimradi muda huo usizidi miaka mitano) ikiwa mtu huyo atapatikana na hatia mbele ya mahakama kwa ajili ya aina yoyote ya makosa yatakayotajwa katika sheria hiyo yanayohusika na uchaguzi wa Wabunge.

(6) Kwa madhumuni ya kutoa fursa ya kukata rufaa kwa mujibu wa Sheria kwa mtu yeyote aliyethibitishwa rasmi kisheria kuwa ana ugonjwa wa akili au aliyehukumiwa na kupewa adhabu ya kifo au ya kufungwa gerezani au aliyepatikana na hatia ya kosa lolote lililotajwa katika sheria kwa mujibu wa ibara ndogo ya (5) ya ibara hii, Bunge laweza kutunga sheria kwa ajili ya kuweka masharti yatakayoeleza kwamba hiyo hukumu inayopingwa na mtu huyo haitakuwa na nguvu kwa ajili ya utekelezaji wa masharti ya ibara ndogo ya (2) au ya (5) ya ibara hii mpaka upite kwanza muda utakaotajwa katika sheria hiyo.

(7) Kanuni zifuatazo zitatumika kwa ajili ya ufafanuzi wa aya ya (c), ya (d) na ya (e) za ibara ndogo ya (2) ya ibara hii, yaani-

(a) ikiwa mtu amepewa adhabu mbili au zaidi za kufungwa gerezani na ameamriwa afungwe kwa muda wa mfululizo, basi adhabu hizo zitahesabiwa kama ni adhabu mbali mbali iwapo muda uliotajwa katika kila moja ya adhabu hizo hauzidi miezi sita; lakini iwapo muda uliotajwa katika adhabu yoyote kati ya adhabu hizo unazidi miezi sita basi adhabu hizo zote zitahesabiwa kama ni adhabu moja; na

©2025 Government of Tanzania. All rights reserved. No part of this book may be reproduced or distributed without permission of OAG.

(b) ikiwa mtu atapewa adhabu ya kufungwa gerezani ikifahamika kuwa adhabu hiyo ya kifungo imetolewa badala ya adhabu ya kutozwa faini au imetolewa kwa sababu mtu huyo ameshindwa kulipa faini aliyoamriwa kulipa, basi muda wa kifungo cha namna hiyo hautahesabiwa.

(8) Katika aya ya (f) ya ibara ndogo ya (2) ya ibara hii *"mkataba wa Serikali"* maana yake ni mapatano yoyote ya mkataba ambayo mmojawapo wa walioshiriki ni Serikali ya Jamhuri ya Muungano au Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar au Idara yoyote ya Serikali hiyo au mtumishi yeyote wa Serikali aliyeshiriki kwa niaba ya Serikali.

*[Ibara ndogo ya (9), (10), (11) na ya (12) zimefutwa na Sheria Na.4 ya 1992 ib.19(d)].*

Sheria Na. 7 ya 1994 Fungu la 8(1)(k)

**(13)** Kwa ajili ya ufafanuzi wa maelezo kuhusu sifa za uchaguzi yaliyomo katika ibara zifuatazo, kila itakapotajwa katika Katiba hii kwamba utekelezaji wa jambo lolote wahitaji mtu mwenye sifa za uchaguzi au mtu ambaye hakupoteza sifa za uchaguzi, basi, isipokuwa kama maelezo yanahitaji vinginevyo, ifahamike kuwa sifa zinazohusika ni zile zinazomwezesha mtu kuchaguliwa kuwa Mbunge wa kuwakilisha jimbo la uchaguzi kama ilivyoelezwa katika ibara ndogo ya (1) ya ibara hii.

Kiapo cha Wabunge Sheria Na. 15 ya 1984 ib. 13

**68.** Kila Mbunge atatakiwa kuapishwa katika Bunge kiapo cha uaminifu kabla hajaanza kushiriki katika shughuli za Bunge; lakini Mbunge aweza kushiriki katika uchaguzi wa Spika hata kabla hajaapishwa.

Tamko rasmi la Wabunge kuhusu maadili ya viongozi Sheria Na. 12 ya 1995 ib. 11

**69.**–(1) Kila Mbunge atatakiwa, kabla ya kumalizika siku thelathini tangu aapishwe kushika madaraka yake kama Mbunge kuwasilisha kwa Spika nakala mbili za tamko rasmi kwamba hajapoteza sifa za uchaguzi kwa mujibu wa masharti ya aya ya (d) ya ibara ndogo ya (2) ya ibara ya 67.

(2) Tamko rasmi linalotakiwa kuwasilishwa kwa Spika kwa mujibu wa masharti ya ibara hii litatolewa kwa kutumia fomu maalum itakayowekwa kwa mujibu wa Sheria iliyotungwa na Bunge.



©2025 Government of Tanzania. All rights reserved. No part of this book may be reproduced or distributed without permission of OAG.

(3) Spika atawasilisha kwa Kamishna wa Maadili nakala moja ya kila tamko rasmi lililowasilishwa kwake kwa mujibu wa masharti ya ibara hii.

(4) Katika ibara hii na katika ibara ya 70 na ya 84 "Kamishna wa Maadili" maana yake ni Kamishna aliyeteuliwa kuwa kiongozi wa Sekretarieti ya Maadili iliyotajwa katika ibara ya 132 ya Katiba hii.

Wabunge kutoa taarifa ya mali
Sheria Na. 12 ya 1995 ib. 12

**70.**–(1) Kila mbunge atatakiwa kuwasilisha kwa Spika nakala mbili za taarifa rasmi ya maelezo ya mali yake na kadri itakavyokuwa, mali ya mke au mume wake. Taarifa itatolewa kwa kutumia fomu maalum itakayowekwa kwa mujibu wa sheria iliyotungwa na Bunge na itatolewa mara kwa mara kama itakavyoagizwa na Sheria hiyo.

(2) Spika atawasilisha kwa Kamishna wa Maadili nakala moja ya kila taarifa rasmi iliyowasilishwa kwake kwa mujibu wa masharti ya ibara hii.

(3) Bunge laweza kutunga sheria kwa ajili ya kuweka masharti kwa makusudi ya kusimamia hifadhi ya taarifa ya mali iliyowasilishwa na mbunge kwa mujibu wa masharti ya ibara hii, na kuhakikisha kwamba watu wasioruhusiwa au wasiohusika hawapati nafasi ya kuona taarifa ya mali wala kujua yaliyomo katika taarifa ya mali.

Muda wa Wabunge kushika madaraka
Sheria Na. 15 ya 1984 ib. 13; 4 ya 1992 ib. 22; 34 ya 1994 ib. 14

**71.**–(1) Mbunge atakoma kuwa Mbunge na ataacha kiti chake katika Bunge litokeapo lolote kati ya mambo yafuatayo:

(a) ikiwa litatokea jambo lolote ambalo, kama asingekuwa Mbunge lingemfanya asiwe na sifa za uchaguzi au apoteze sifa za uchaguzi au asiweze kuchaguliwa au kuteuliwa kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii;

(b) ikiwa Mbunge huyo atachaguliwa kuwa Rais;

(c) ikiwa Mbunge atakosa kuhudhuria vikao vya Mikutano ya Bunge mitatu mfululizo bila ya ruhusa ya Spika;

(d) ikiwa itathibitishwa kwamba amevunja masharti ya Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma;

(e) iwapo Mbunge anachaguliwa au anateuliwa kuwa Makamu wa Rais;

©2025 Government of Tanzania. All rights reserved. No part of this book may be reproduced or distributed without permission of OAG.

(f) iwapo Mbunge ataacha kuwa mwanachama wa chama alichokuwamo wakati alipochaguliwa au alipoteuliwa kuwa Mbunge;

(g) kwa Mbunge ambaye anatakiwa kutoa taarifa rasmi ya mali kwa mujibu wa masharti ya ibara ya 70, ikiwa atashindwa kutoa hilo tamko rasmi kwa mujibu wa masharti ya hiyo ibara ya 70 katika muda uliowekwa mahususi kwa ajili hiyo kwa mujibu wa Sheria iliyotungwa na Bunge,

lakini iwapo Mbunge hatakoma kuwa Mbunge kwa mujibu wa jambo lolote kati ya mambo hayo yaliyotajwa na kama hatajiuzulu au kufariki mapema zaidi basi Mbunge ataendelea kushika madaraka yake kama Mbunge mpaka wakati Bunge litakapovunjwa kwa mujibu wa ibara ya 90, bila ya kuathiri haki na stahili zinazotokana na ubunge wake.

(2) Bunge laweza kutunga sheria kwa ajili ya kuweka masharti yatakayomwezesha Mbunge kukata rufaa, kwa mujibu wa sheria kupinga hukumu ya kuthibitishwa kwake kuwa ni mtu mwenye ugonjwa wa akili au kupinga adhabu ya kifo au ya kufungwa gerezani, au kupinga kupatikana kwake na hatia kwa kosa la aina iliyotajwa kwa mujibu wa masharti ya ibara ndogo ya (5) ya ibara ya 67 ya Katiba hii; na sheria hiyo yaweza kueleza kwamba hiyo hukumu iliyopingwa na huyo Mbunge haitatiliwa nguvu kisheria mpaka umalizike kwanza muda utakaotajwa katika Sheria hiyo.

Watu wenye madaraka Serikalini kukoma utumishi wanapochaguliwa
Sheria Na. 4 ya 1992 ib. 23; 12 ya 1995 ib. 14

**72.** Iwapo mtu yeyote mwenye madaraka katika utumishi wa Serikali, madaraka ya aina iliyotajwa katika ibara ya 67(2)(g) ataamua-

(a) kuwa mgombea uchaguzi wa Rais au wa nafasi nyingine yoyote chini ya Katiba hii; au

(b) kugombea uongozi wa ngazi yoyote katika chama cha siasa kinyume na masharti ya ajira,

mtu huyo atahesabiwa kuwa utumishi wake umekoma tangu tarehe yake ya kuwa mgombea uchaguzi au ya kugombea uongozi katika chama cha siasa.

©2025 Government of Tanzania. All rights reserved. No part of this book may be reproduced or distributed without permission of OAG.

Masharti ya kazi ya Wabunge
Sheria Na. 15 ya 1984 ib. 13

**73.** Wabunge wote wa aina zote watashika madaraka yao kwa mujibu wa Katiba hii, na watalipwa mshahara, posho na malipo mengine kwa mujibu wa sheria iliyotungwa na Bunge.

*Tume ya Uchaguzi*

Tume ya uchaguzi
Sheria Na. 15 ya 1984 ib. 13; 4 ya 1992 ib. 24 7 ya 1993 ib. 2; 3 ya 2000 ib. 14; 1 ya 2005 ib. 14

**74.**–(1) Kutakuwa na Tume ya Uchaguzi ya Jamhuri ya Muungano ambayo itakuwa na wajumbe wafuatao watakaoteuliwa na Rais:

(a) Mwenyekiti ambaye atakuwa ni Jaji wa Mahakama Kuu au Mahakama ya Rufani au ni mtu mwenye sifa ya kuwa wakili na amekuwa na sifa hizo kwa muda usiopungua miaka kumi na tano;

(b) Makamu wa Mwenyekiti ambaye atakuwa ni Jaji wa Mahakama Kuu au Mahakama ya Rufani au ni mtu mwenye sifa ya kuwa wakili na amekuwa na sifa hizo kwa muda usiopungua miaka kumi na tano; na

(c) Wajumbe wengine watakaotajwa na sheria iliyotungwa na Bunge.

(2) Rais atamteua Makamu wa Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi kwa kufuata kanuni kwamba endapo Mwenyekiti ni mtu anayetoka sehemu moja ya Muungano, Makamu wake atakuwa ni mtu anayetoka sehemu ya pili ya Muungano.

(3) Watu wafuatao hawataweza kuteuliwa kuwa wajumbe wa Tume ya Uchaguzi yaani-

(a) Waziri au Naibu Waziri;

(b) mtu mwenye madaraka ya aina yoyote iliyotajwa mahususi na sheria iliyotungwa na Bunge kwamba ni mwiko kwa mtu mwenye madaraka hayo kuwa mjumbe wa Tume ya Uchaguzi;

(c) Mbunge, Diwani au mtu mwingine mwenye madaraka ya aina yaliyotajwa na sheria iliyotungwa na Bunge kwa mujibu wa masharti ya aya ya (g) ya ibara ndogo ya (2) ya ibara ya 67 ya Katiba hii; au

(d) Kiongozi wa chama chochote cha siasa.

©2025 Government of Tanzania. All rights reserved. No part of this book may be reproduced or distributed without permission of OAG.

(4) Bila ya kuathiri masharti mengineyo ya ibara hii, Mjumbe wa Tume ya Uchaguzi atakoma kuwa Mjumbe litokeapo lolote kati ya mambo yafuatayo-

(a) ukimalizika muda wa miaka mitano tangu alipoteuliwa; au
(b) ikiwa litatokea jambo lolote ambalo, kama asingekuwa Mjumbe wa Tume, lingemfanya asiweze kuteuliwa kuwa Mjumbe wa Tume ya Uchaguzi.

(5) Rais aweza tu kumwondoa katika madaraka Mjumbe wa Tume ya Uchaguzi kwa sababu ya kushindwa kutekeleza kazi zake, ama kutokana na maradhi au sababu nyingine yoyote, au kwa sababu ya tabia mbaya au kupoteza sifa za kuwa mjumbe.

(6) Majukumu ya Tume ya Uchaguzi yatakuwa ni-

(a) kusimamia na kuratibu uandikishaji wa wapiga kura katika uchaguzi wa Rais na Wabunge katika Jamhuri ya Muungano;
(b) kusimamia na kuratibu uendeshaji wa uchaguzi wa Rais na Wabunge;
(c) kuchunguza mipaka na kuigawa Jamhuri ya Muungano katika maeneo mbalimbali kwa ajili ya uchaguzi wa Wabunge;
(d) kusimamia na kuratibu uandikishaji wa wapiga kura na uendeshaji wa uchaguzi wa madiwani; na
(e) kutekeleza majukumu mengine yoyote kwa mujibu wa Sheria iliyotungwa na Bunge.

(7) Kwa madhumuni ya utekelezaji bora wa majukumu yake yaliyoainishwa katika ibara hii, Tume ya Uchaguzi itakuwa ni idara huru inayojitegemea, itafanya maamuzi yake rasmi kuhusu utekelezaji wa majukumu yake kwa vikao, na mtendaji mkuu wake atakuwa ni Mkurugenzi wa Uchaguzi ambaye atateuliwa na kufanya kazi kwa mujibu wa masharti ya Sheria iliyotungwa na Bunge.

(8) Bunge laweza kutunga sheria kwa ajili ya kuweka masharti ya kuweka utaratibu wa kusimamia uchaguzi wa Wabunge wanaowakilisha majimbo ya uchaguzi.

(9) Tume ya Uchaguzi yaweza kutekeleza shughuli zake bila ya kujali kwamba kuna nafasi miongoni mwa viti vya wajumbe

©2025 Government of Tanzania. All rights reserved. No part of this book may be reproduced or distributed without permission of OAG.

au kwamba Mjumbe mmojawapo hayupo, lakini kila uamuzi wa Tume ya Uchaguzi ni lazima uungwe mkono na wajumbe walio wengi kati ya wajumbe wote wa Tume ya Uchaguzi.

(10) Bunge laweza kutunga sheria kwa ajili ya kuweka masharti ya kuweka utaratibu wa kuwateua Wajumbe wa kusimamia uchaguzi wa Wabunge wanaowakilisha majimbo ya uchaguzi na, bila ya kuathiri masharti ya sheria kama hiyo au maagizo ya Tume ya Uchaguzi, madaraka ya Tume ya Uchaguzi ya kusimamia uchaguzi yaweza kutekelezwa na wajumbe hao.

(11) Katika kutekeleza madaraka yake kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii, Tume ya Uchaguzi haitalazimika kufuata amri au maagizo ya mtu yeyote au idara yoyote ya Serikali, au maoni ya chama chochote cha siasa.

(12) Hakuna mahakama yoyote itakayokuwa na mamlaka ya kuchunguza jambo lolote lililotendwa na Tume ya Uchaguzi katika kutekeleza madaraka yake kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii.

(13) Katika utekelezaji wa madaraka yake kwa mujibu wa Katiba hii, Tume ya Uchaguzi ya Jamhuri ya Muungano itashauriana mara kwa mara na Tume ya Uchaguzi ya Tanzania Zanzibar.

(14) Itakuwa ni marufuku kwa watu wanaohusika na uchaguzi kujiunga na chama chochote cha siasa, isipokuwa tu kwamba kila mmoja wao atakuwa na haki ya kupiga kura iliyotajwa katika ibara ya 5 ya Katiba hii.

(15) Kwa madhumuni ya ibara ndogo ya (14) watu wanaohusika na uchaguzi ni-

(a) Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi;
(b) Makamu Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi;
(c) Wajumbe wote wa Tume ya Uchaguzi;
(d) Mkurugenzi wa Uchaguzi pamoja na watumishi wote wa Tume ya Uchaguzi; na
(e) Wasimamizi wote wa Uchaguzi katika miji na wilaya zote.

©2025 Government of Tanzania. All rights reserved. No part of this book may be reproduced or distributed without permission of OAG.

*Majimbo ya Uchaguzi*

Majimbo ya uchaguzi Sheria Na. 4 ya 1992 ib. 24

**75.**–(1) Bila ya kuathiri masharti mengineyo yaliyo katika ibara hii, Jamhuri ya Muungano itagawanywa katika majimbo ya uchaguzi kwa idadi na kwa namna itakavyoamuliwa na Tume ya Uchaguzi baada ya kupata kibali cha Rais.

(2) Bila ya kuathiri sheria yoyote inayotumika kuhusu mambo hayo, Tume ya Uchaguzi, baada ya kupata kibali cha Rais itakuwa na mamlaka ya kuweka mipaka ya majimbo ya uchaguzi.

(3) Katika kuweka mipaka ya majimbo ya uchaguzi, Tume ya Uchaguzi itazingatia ipasavyo upatikanaji wa njia za mawasiliano, na pia hali ya kijiografia ya eneo linalokusudiwa kugawanywa katika majimbo ya uchaguzi.

(4) Bila ya kuathiri masharti ya Katiba hii na ya sheria yoyote inayohusika na mgawanyo wa nchi katika majimbo ya uchaguzi, Tume ya Uchaguzi yaweza mara kwa mara, na angalau kila baada ya miaka kumi, kuchunguza mgawanyo wa Jamhuri ya Muungano katika majimbo ya uchaguzi, na yaweza kubadilisha majimbo ya uchaguzi kama matokeo ya uchunguzi huo au kutokana na matokeo ya hesabu ya watu wote katika Jamhuri ya Muungano.

(5) Endapo baada ya uchunguzi kufanywa kuhusu mgawanyo wa Jamhuri ya Muungano katika majimbo ya uchaguzi kunafanyika mabadiliko katika majimbo ya uchaguzi, au katika idadi ya Wabunge wanaowakilisha majimbo ya uchaguzi au mabadiliko kwa idadi ya majimbo ya uchaguzi au idadi ya Wabunge, basi mabadiliko yatakayotokea katika idadi ya Wabunge wanaowakilisha majimbo ya uchaguzi yataanza kutumika wakati Bunge litakapovunjwa tena baada ya kutokea mabadiliko hayo ya idadi ya majimbo au idadi ya Wabunge katika majimbo ya uchaguzi.

(6) Bila ya kujali masharti mengineyo ya ibara hii, hakuna mahakama yoyote itakayokuwa na mamlaka ya kuchunguza jambo lolote lililotendwa na Tume katika utekelezaji wake wa kugawa Jamhuri ya Muungano katika majimbo ya uchaguzi.

©2025 Government of Tanzania. All rights reserved. No part of this book may be reproduced or distributed without permission of OAG.

### *Uchaguzi na Uteuzi wa Wabunge*

Uchaguzi katika majimbo ya uchaguzi
Sheria Na. 15 ya 1984 ib. 13; 3 ya 2000 ib. 15

**76.**–(1) Kila mara baada ya Bunge kuvunjwa, kutakuwa na uchaguzi wa Wabunge katika majimbo yote ya uchaguzi.

(2) Hali kadhalika, kutakuwa na uchaguzi wa Mbunge katika jimbo la uchaguzi, ikiwa kiti cha Mbunge yeyote aliyechaguliwa kuwakilisha jimbo hilo kitakuwa wazi kwa sababu nyingine yoyote isiyohusika na kuvunjwa kwa Bunge.

(3) Bila ya kujali masharti ya ibara hii yaliyotangulia, ifahamike kwamba ikiwa tarehe ya kuvunjwa Bunge imetangazwa au inafahamika kutokana na matukio yaliyoelezwa katika ibara ndogo ya (3) ya ibara ya 90, basi uchaguzi wa namna hiyo hautafanywa katika kipindi chote cha miezi kumi na miwili ya nyuma ikihesabiwa tangu tarehe hiyo.

Utaratibu wa uchaguzi wa Wabunge wa Majimbo ya uchaguzi
Sheria Na. 4 ya 1992 ib. 25

**77.**–(1) Wabunge wanaowakilisha majimbo ya uchaguzi watachaguliwa na wananchi kwa kufuata masharti ya Katiba hii na vile vile masharti ya sheria iliyotungwa na Bunge kwa mujibu wa Katiba hii inayoweka masharti kuhusu uchaguzi wa Wabunge wanaowakilisha majimbo ya uchaguzi.

(2) Isipokuwa pale ambapo Tume ya Uchaguzi, kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii au sheria iliyotungwa na Bunge kwa ajili hiyo, itaagiza vinginevyo, kutachaguliwa Mbunge mmoja tu katika jimbo la uchaguzi.

(3) Wagombea uchaguzi katika jimbo la uchaguzi watatakiwa watimize masharti yafuatayo-

(a) wawe wamependekezwa mmoja mmoja, na chama cha siasa kinachoshiriki uchaguzi katika jimbo hilo; na

(b) wamewasilisha majina yao kwa Tume ya Uchaguzi kwa mujibu wa utaratibu uliowekwa na sheria iliyotungwa na Bunge au uliofafanuliwa na Tume ya Uchaguzi kwa mujibu wa sheria.

©2025 Government of Tanzania. All rights reserved. No part of this book may be reproduced or distributed without permission of OAG.

Utaratibu wa uchaguzi wa Wabunge wanawake
Sheria Na. 4 ya 1992 ib. 26; 3 ya 2000 ib. 16; 1 ya 2005 ib. 15; TS. Na. 133 la 2001

**78.**–(1) Kwa madhumuni ya uchaguzi wa Wabunge wanawake waliotajwa katika ibara ya 66(1) (b), vyama vya siasa vilivyoshiriki katika Uchaguzi Mkuu kwa kufuata utaratibu uliowekwa, na kupata angalau asilimia tano ya kura zote halali za wabunge, vitapendekeza kwa Tume ya Uchaguzi majina ya wanawake kwa kuzingatia uwiano wa kura ambazo kila chama kimepata katika uchaguzi wa Wabunge.

(2) Bila kujali masharti ya ibara ndogo ya (1), zifuatazo zitahesabiwa kuwa ni kura halali za Mbunge aliyepita bila kupingwa katika jimbo la uchaguzi:

(a) endapo chama kimemsimamisha mgombea Urais, kura zilizopigwa katika jimbo kwa mgombea Urais wa chama cha Mbunge huyo; au

(b) endapo chama hakikumsimamisha mgombea Urais, asilimia hamsini na moja ya kura za watu wote waliojiandikisha kupiga kura katika jimbo hilo.

(3) Majina ya watu waliopendekezwa kwa mujibu wa ibara ndogo ya (1) na Tume ya Uchaguzi yatatangazwa kama matokeo ya uchaguzi baada ya Tume ya Uchaguzi kuridhika kwamba masharti ya Katiba na Sheria yanayohusika yamezingatiwa.

(4) Orodha ya majina ya wagombea wanawake iliyowasilishwa kwa Tume ya Uchaguzi na kila chama kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu ndiyo itakayotumiwa na Tume ya Uchaguzi baada ya kushauriana na chama kinachohusika, kwa madhumuni ya kujaza nafasi yoyote ya Mbunge wa aina hii inapotokea wakati wowote katika maisha ya Bunge.

Utaratibu wa uchaguzi wa Wabunge wa kuchaguliwa na Baraza la Wawakilishi

**79.** Baraza la Wawakilishi litaweka utaratibu litakaoufuata kwa ajili ya kufanya uchaguzi wa Wabunge waliotajwa katika ibara ya 66(1)(c) ya Katiba hii.

©2025 Government of Tanzania. All rights reserved. No part of this book may be reproduced or distributed without permission of OAG.

Utaratibu wa uchaguzi wa Wabunge wa Taifa waliopendekezwa na Jumuiya za Wananchi
Sheria Na. 15 ya 1984 ib. 13

**80.** [Ibara 80 ya Katiba imefutwa na Sheria na.4 ya 1992 Ibara 27].

Utaratibu wa Kupendekeza majina ya wagombea Uchaguzi wa Wabunge wanawake
Sheria Na. 4 ya 1992 ib. 29

**81.** Bila ya kuathiri masharti mengineyo ya Katiba hii, Tume ya Uchaguzi yaweza kuweka masharti yanayofafanua utaratibu utakaotumiwa na vyama vya siasa kwa ajili ya kuchagua na kupendekeza majina ya Wabunge wa aina iliyotajwa katika ibara ya 66 (1) (b).

Wabunge wa kuteuliwa na Rais

**82.** [Ibara ya 82 ya Katiba imefutwa na Sheria Na.4 ya 1992 ibara 29].

Uamuzi wa suala kama mtu ni Mbunge
Sheria Na. 14 ya 1979 ib. 8; 15 ya 1984 ib. 13; 14 ya 1990 ib. 4; 4 ya 1992 ib. 30

**83.**–(1) Kila shauri kwa ajili ya kupata uamuzi juu ya suala-

(a) kama uchaguzi au uteuzi wa mtu yeyote kuwa mbunge ulikuwa halali au sivyo; au

(b) kama Mbunge amekoma kuwa Mbunge na kiti chake katika Bunge ki-wazi au hapana, litafunguliwa na kusikilizwa kwanza katika Mahakama Kuu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania bila ya kuathiri masharti ya ibara ndogo ya (2) ya ibara hii.

(2) Iwapo Tume ya Uchaguzi katika kutekeleza madaraka yake kwa mujibu wa masharti ya ibara ya 41(7) ya Katiba hii imemtangaza Mbunge yeyote kwamba amechaguliwa kuwa Rais basi hakuna mahakama wala chombo chochote kingine kitakachochunguza zaidi suala lolote linalohusu kiti cha Mbunge huyo kuwa wazi.

(3) Bunge laweza kutunga Sheria kwa ajili ya kuweka masharti kuhusu mambo yafuatayo-

(a) watu wanaoweza kufungua shauri katika Mahakama Kuu kwa ajili ya kupata uamuzi juu ya suala lolote kwa mujibu wa masharti ya ibara hii;

©2025 Government of Tanzania. All rights reserved. No part of this book may be reproduced or distributed without permission of OAG.

(b) sababu na nyakati za kufungua shauri la namna hiyo, utaratibu wa kufungua shauri na masharti yanayotakiwa yatimizwe kwa kila shauri kama hilo; na

(c) kutaja mamlaka ya Mahakama Kuu juu ya shauri kama hilo na kueleza utaratibu wa kusikiliza shauri lenyewe.

(4) Kutakuwa na haki ya kukata rufaa mbele ya Mahakama ya Rufani ya Tanzania kupinga uamuzi wa Mahakama Kuu juu ya shauri lolote lililosikilizwa kwa mujibu wa masharti ya ibara hii.

## SEHEMU YA TATU
## UTARATIBU, MADARAKA NA HAKI ZA BUNGE

*Spika na Naibu wa Spika*

Spika na Mamlaka yake Sheria Na. 15 ya 1984 ib. 14; 4 ya 1992 ib. 31; 12 ya 1995 ib. 15

**84.**–(1) Kutakuwa na Spika wa Bunge ambaye atachaguliwa na Wabunge kutoka miongoni mwa watu ambao ni Wabunge au mwenye sifa za kuwa Mbunge; atakuwa ndiye kiongozi wa Bunge na atawakilisha Bunge katika vyombo na vikao vingine vyote nje ya Bunge.

(2) Waziri, Naibu Waziri au mtu mwenye madaraka ya aina nyingine yoyote itakayotajwa na sheria iliyotungwa na Bunge kwa madhumuni ya ibara hii, hataweza kuchaguliwa kuwa Spika.

(3) Mtu yeyote atakayechaguliwa kuwa Spika atatakiwa, kabla ya kumaliza siku kumi na tano tangu kuchaguliwa kwake, kuwasilisha kwa Rais tamko rasmi kwamba hajapoteza sifa za uchaguzi kwa mujibu wa masharti ya aya ya (d) ya ibara ndogo ya (2) ya ibara ya 67. Tamko hilo litatolewa kwa kutumia fomu maalum itakayowekwa kwa mujibu wa sheria iliyotungwa na Bunge.

(4) Rais atawasilisha kwa Kamishna wa Maadili nakala moja ya kila tamko rasmi lililowasilishwa kwake kwa mujibu wa masharti ya ibara ndogo ya (3) ya ibara hii.

©2025 Government of Tanzania. All rights reserved. No part of this book may be reproduced or distributed without permission of OAG.

Sheria Na. 7 ya 1994 Fungu la 8(1)(k)

(5) Spika atatakiwa kuwasilisha kwa Rais nakala mbili za taarifa rasmi ya maelezo ya mali na, kadri itakavyokuwa mali ya mke au mume wake. Spika atatoa taarifa hiyo kwa kutumia fomu maalum iliyowekwa kwa ajili hiyo kwa mujibu wa sheria iliyotungwa na Bunge na atatoa taarifa ya namna hiyo mara kwa mara kadri itakavyoagiza sheria hiyo.

(6) Masharti ya ibara ndogo ya (2) na ya (3) ya ibara ya 70 yatatumika pia, kwa kadri itakavyowezekana, kwa taarifa ya mali yoyote itakayotolewa na Spika, kwa mujibu wa masharti ya ibara hii.

(7) Spika atakoma kuwa Spika na ataacha kiti cha Spika litokeapo lolote kati ya mambo yafuatayo:

(a) iwapo mtu huyo alichaguliwa kutoka miongoni mwa Wabunge, basi ikiwa atakoma kuwa Mbunge kwa sababu yoyote ambayo haihusiki na kuvunjwa Bunge;

(b) ikiwa kutatokea jambo lolote ambalo, kama asingekuwa Spika lingemfanya mtu huyo asiwe na sifa za uchaguzi au apoteze sifa za uchaguzi wa Spika;

(c) Bunge litakapokutana kwa mara ya kwanza baada ya Uchaguzi Mkuu uliofanywa baada ya Bunge kuvunjwa, lakini masharti ya aya hii yatatumika bila ya kuathiri masharti ya ibara ndogo ya (4) ya ibara ya 90 ya Katiba hii;

(d) ikiwa mtu huyo ataondolewa kwenye madaraka ya Spika kwa azimio la Bunge lilioungwa mkono na Wabunge ambao idadi yao haipungui theluthi mbili ya Wabunge wote;

(e) ikiwa mtu huyo atashindwa kuwasilisha kwa Rais tamko rasmi kwa mujibu wa masharti ya ibara ndogo ya (5) ya ibara hii;

(f) ikiwa mtu huyo atapatikana na hatia kwa kosa la kutoa habari za uwongo, kwa kiapo kinyume cha sheria ya Kanuni ya Jinai, kuhusu tamko rasmi lolote lililotolewa kwa mujibu wa masharti ya ibara ndogo ya (3) ya ibara hii;

(g) ikiwa mtu huyo huyo atashindwa kuwasilisha kwa Rais taarifa ya mali kwa mujibu wa masharti ya ibara ndogo ya (5) ya ibara hii kabla ya kumalizika muda uliowekwa

©2025 Government of Tanzania. All rights reserved. No part of this book may be reproduced or distributed without permission of OAG.

kwa ajili hiyo kwa mujibu wa sheria iliyotungwa na Bunge; au

(h) ikiwa itathibitika kuwa mtu amevunja masharti ya Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma.

(8) Hakuna shughuli yoyote itakayotekelezwa katika Bunge (isipokuwa uchaguzi wa Spika) wakati wowote ambao kiti cha Spika kitakuwa ki-wazi.

(9) Mtu yeyote ambaye si Mbunge atakayechaguliwa kuwa Spika, atatakiwa, kabla ya kuanza kutekeleza madaraka yake, kuapishwa katika Bunge kiapo cha uaminifu.

Naibu wa Spika Sheria Na. 15 ya 1984 ib. 14

**85.**–(1) Kutakuwa na Naibu wa Spika wa Bunge ambaye atachaguliwa na wajumbe kutoka miongoni mwa Wabunge.

(2) Waziri, Naibu Waziri au mtu mwenye madaraka ya aina nyingine yoyote itakayotajwa na Sheria iliyotungwa na Bunge kwa madhumuni ya ibara hii, hataweza kuchaguliwa kuwa Naibu wa Spika.

(3) Wabunge watamchagua Naibu Spika, nyakati zifuatazo:

(a) Bunge litakapokutana kwa mara ya kwanza baada ya Uchaguzi Mkuu au mapema iwezekanavyo baada ya wakati huo; na

(b) katika kikao cha kwanza cha Bunge baada ya kiti cha Naibu wa Spika, kuwa wazi kwa sababu yoyote isiyohusika na Bunge kuvunjwa au mapema iwezekanavyo baada ya kikao hicho.

(4) Naibu wa Spika, atakoma kuwa Naibu wa Spika na ataacha kiti cha Naibu wa Spika, litokeapo lolote kati ya mambo yafuatayo:

(a) ikiwa mtu huyo atakoma kuwa Mbunge;

(b) ikiwa kutatokea jambo lolote ambalo kama asingekuwa Naibu wa Spika, lingemfanya mtu huyo asiwe na sifa za uchaguzi au apoteze sifa za uchaguzi wa Naibu Spika; au

(c) ikiwa mtu huyo ataondolewa kwenye madaraka ya Naibu wa Spika kwa azimio la Bunge.

©2025 Government of Tanzania. All rights reserved. No part of this book may be reproduced or distributed without permission of OAG.

Utaratibu wa kumchagua Spika na Naibu Spika
Sheria Na. 13 ya 1984 ib. 14

**86.**–(1) Kutakuwa na uchaguzi wa Spika wakati wowote katika Mkutano wa Kwanza wa Bunge Jipya, na katika kikao cha kwanza chochote mara baada ya kutokea nafasi katika kiti cha Spika.

(2) Kutakuwa na uchaguzi wa Naibu wa Spika wakati wowote katika Mkutano wa Kwanza wa Bunge Jipya utakaoteuliwa na Bunge na vilevile katika kikao cha kwanza cha Bunge mara baada ya kutokea nafasi katika kiti cha Naibu wa Spika.

(3) Uchaguzi wa Spika, na vile vile uchaguzi wa Naibu wa Spika, utafanywa kwa kura ya siri, na utaendeshwa kwa kufuata utaratibu uliowekwa na Kanuni za Bunge.

*Ofisi ya Bunge*

Katibu wa Bunge
Sheria Na. 15 ya 1984 ib. 14

**87.**–(1) Kutakuwa na Katibu wa Bunge ambaye atateuliwa na Rais kutoka miongoni mwa watu wenye madaraka ya juu katika utumishi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano.

(2) Katibu wa Bunge atakuwa ndiye mtendaji mkuu katika Ofisi ya Bunge na atawajibika kwa utendaji bora wa shughuli za Bunge kwa kuzingatia masharti ya Katiba hii na ya sheria inayohusika.

Sekretarieti ya Bunge
Sheria Na. 15 ya 1984 ib. 14

**88.**–(1) Kutakuwa na Sekretarieti ya Bunge itakayokuwa na nafasi za madaraka katika utumishi wa Serikali kwa idadi atakayoagiza Rais.

(2) Sekretarieti ya Bunge itakuwa na watumishi kwa idadi na ngazi za utumishi itakavyoamuliwa mara kwa mara na Tume ya Utumishi inayohusika baada ya kushauriana na Katibu wa Bunge.

(3) Sekretarieti ya Bunge chini ya uongozi wa Katibu wa Bunge itaendeleza kazi na shughuli zote zilizowekwa au zitakazokuwa ni muhimu kwa ajili ya kuhakikisha utekelezaji bora wa Bunge na wa Wabunge wa madaraka ya Bunge chini ya Katiba hii.

©2025 Government of Tanzania. All rights reserved. No part of this book may be reproduced or distributed without permission of OAG.

*Utaratibu wa Shughuli Bungeni*

Kanuni za Kudumu za Bunge
Sheria Na. 15 ya 1984 ib. 14

**89.**–(1) Bila ya kuathiri masharti ya Katiba hii Bunge laweza kutunga Kanuni za Kudumu kwa ajili ya kuweka utaratibu wa kutekeleza shughuli zake.

(2) Kanuni za Kudumu zilizotungwa kwa mujibu wa ibara hii zaweza kuweka utaratibu wa kusimamia utekelezaji wa shughuli za Sekretarieti ya Bunge na pia utekelezaji wa shughuli za Bunge ndani ya Bunge na zile za kamati na kamati ndogo za Bunge.

Kuitishwa kwa mikutano ya Bunge na kuvunjwa kwa Bunge
Sheria Na. 15 ya 1984 ib. 14; 20 ya 1992 ib. 13

**90.**–(1) Baada ya Uchaguzi Mkuu Rais ataitisha Mkutano wa Bunge Jipya ufanyike kabla ya kupita siku saba tangu kutangazwa matokeo ya huo Uchaguzi Mkuu katika majimbo ya uchaguzi yote isipokuwa katika majimbo yale ambako uchaguzi umefutwa na kufanywa upya.

(2) Rais hatakuwa na uwezo wa kulivunja Bunge wakati wowote, isipokuwa tu-

(a) kama Bunge limemaliza muda wa uhai wake kwa mujibu wa ibara ya 65 ya Katiba; au wakati wowote katika miezi kumi na miwili ya mwisho ya uhai wa Bunge, isipokuwa tu kama Spika amepokea taarifa rasmi inayopendekeza kuundwa kwa Kamati Maalumu ya Uchunguzi kwa madhumuni ya kumuondoa Rais madarakani kwa mujibu wa ibara ya 46A ya Katiba hii;

(b) kama Bunge limekataa kupitisha Bajeti iliyopendekezwa na Serikali;

(c) kama Bunge limekataa kupitisha Muswada wa Sheria kwa mujibu wa ibara ya 97(4) ya Katiba;

(d) kama Bunge limekataa kupitisha hoja ambayo ni ya msingi katika sera za Serikali, na Rais anaona kwamba njia ya kuendelea kutoka hapo si kumteua Waziri Mkuu mwingine bali ni kuitisha Uchaguzi Mkuu; au

(e) endapo, kutokana na uwiano wa uwakilishi wa Vyama vya Siasa katika Bunge, Rais anaona kwamba hakuna uhalali kwa Serikali iliyopo kuendelea kuwapo, na wala haiwezekani kuunda Serikali mpya.

©2025 Government of Tanzania. All rights reserved. No part of this book may be reproduced or distributed without permission of OAG.

(3) Muda wa maisha ya Bunge ukimalizika Bunge litahesabiwa kuwa limevunjwa; isipokuwa kwamba muda huo ukiisha wakati wowote ambapo Jamhuri ya Muungnao iko katika vita Bunge laweza mara kwa mara kuongeza muda huo uliotajwa katika ibara ya 65 ya Katiba hii kwa muda usiozidi miezi kumi na miwili mara kwa mara lakini maisha ya Bunge hayawezi kuongezwa kwa mujibu wa masharti ya ibara ndogo hii kwa muda unaozidi miaka mitano.

(4) Kukitokea hali ya hatari au kama kuna hali ya hatari ambayo Rais anaona inasababisha kuitisha Mkutano wa Bunge na iwapo wakati huo Bunge limevunjwa na matokeo ya kura zilizo nyingi za Uchaguzi Mkuu hayajatangazwa basi Rais aweza kutoa Taarifa Maalumu ya kuitisha Mkutano wa Bunge na kuagiza kwamba Spika na watu wote waliokuwa Wabunge mara tu kabla Bunge halijavunjwa wahudhurie Mkutano huo wa Bunge na watu hao pamoja na huyo Spika, watahesabiwa kuwa ndio Wajumbe wa Bunge kwa madhumuni ya Mkutano huo na watahesabiwa hivyo mpaka usiku wa manane wa siku yatakapotangazwa matokeo ya kura zilizo nyingi za Uchaguzi Mkuu.

Rais aweza kulihutubia Bunge
Sheria Na. 15 ya 1984 ib. 14

**91.**–(1) Rais atalihutubia Bunge Jipya katika Mkutano wake wa Kwanza na kulifungua rasmi Bunge hilo.

(2) Bila ya kuathiri masharti ya ibara ndogo ya (1), Rais aweza wakati wowote kulihutubia Bunge au kupeleka kwenye Bunge taarifa ambayo itasomwa na Waziri.

Mikutano ya Bunge
Sheria Na. 15 ya 1984 ib. 14, TS. Na. 133 la 2001

**92.**–(1) Bunge litafanya mikutano yake mahali ambapo ni desturi kufanya Mikutano hiyo au mahali pengine popote katika Jamhuri ya Muungano patakapotajwa na Rais kwa ajili hiyo.

(2) Mkutano wa kwanza wa Bunge katika Maisha ya Bunge utaanza siku ile ambayo Bunge limeitwa kukutana, na kila Mkutano ufuatao utaanza siku yoyote itakayopangwa na Bunge lenyewe au siku yoyote itakayopangwa kwa mujibu wa Kanuni za Bunge.

(3) Rais aweza kuitisha Mkutano wa Bunge wakati wowote.

©2025 Government of Tanzania. All rights reserved. No part of this book may be reproduced or distributed without permission of OAG.

Uongozi wa Vikao vya Bunge Sheria Na. 15 ya 1984 ib. 14

**93.** Kila kikao cha Bunge kitaongozwa na mmoja wapo wa watu wafuatao, yaani-

(a) Spika;

(b) ikiwa Spika hayupo, Naibu wa Spika; au

(c) ikiwa Spika na Naibu wa Spika wote hawapo, Mbunge yeyote aliyechaguliwa na Bunge kwa ajili hiyo, lakini Waziri, au Naibu Waziri au mtu mwenye madaraka ya aina nyingine yoyote yaliyotajwa na sheria iliyotungwa na Bunge kwa madhumuni ya ibara hii hataweza kuchaguliwa kwa mujibu wa masharti ya aya hii.

Akidi ya Vikao vya Bunge Sheria Na. 15 ya 1984 ib. 14; 7 ya 1994 Fungu la 8(1)(k)

**94.**–(1) Akidi kwa kila kikao cha Bunge ni nusu ya Wabunge wote.

(2) Isipokuwa kama imeelezwa vingine katika Katiba hii, kila swali litakalotolewa kwa ajili ya kupata uamuzi wa Bunge litaamuliwa kwa kufuata wingi wa kura za Wabunge waliohudhuria na kupiga kura.

(3) Spika, Naibu wa Spika au mtu mwingine atakayeongoza kikao cha Bunge, hatakuwa na kura ya kawaida bali atakuwa na kura ya uamuzi kukitokea usawa wa kura.

(4) Kanuni za Bunge zaweza kuweka masharti kwamba Mbunge yeyote atakayepiga kura juu ya jambo lolote ambalo yeye binafsi ana masilahi nalo atahesabiwa kuwa hakupiga kura.

Viti vilivyo wazi katika Bunge Sheria Na. 15 ya 1984 ib. 14

**95.** Bunge laweza kutekeleza shughuli wakati wa vikao vyake bila ya kujali kwamba kuna kiti kilicho wazi miongoni mwa viti vya Wabunge (iwe kiti hicho kimekuwa wazi tangu Bunge lilipokutana kwa mara ya kwanza baada ya Uchaguzi Mkuu au kimekuwa wazi baada ya Mkutano huo wa kwanza) na iwapo katika shughuli hizo atashiriki mtu yeyote ambaye hana haki ya kushiriki au kama wakati wa shughuli hizo atakuwapo mtu yeyote ambaye hana haki ya kuwapo, basi kushiriki kwa mtu huyo au kuwapo kwake hakutabatilisha shughuli hizo.

©2025 Government of Tanzania. All rights reserved. No part of this book may be reproduced or distributed without permission of OAG.

Kamati za Bunge
Sheria Na.
15 ya 1984 ib. 14;
12 ya 1995 ib. 16

**96.**–(1) Bunge laweza kuunda Kamati za Bunge za namna mbalimbali kadri litakavyoona inafaa kwa ajili ya utekelezaji bora wa madaraka yake.

(2) Kanuni za Bunge zaweza kufafanua muundo na shughuli za Kamati za Bunge zitakazoundwa kwa mujibu wa masharti ya ibara hii.

*Utaratibu wa Kutunga Sheria*

Namna ya kutumia madaraka ya kutunga Sheria
Sheria Na.
15 ya 1984 ib. 14

**97.**–(1) Bila ya kuathiri masharti mengineyo yaliyomo katika Katiba hii, Bunge litatumia madaraka yake ya kutunga sheria kwa kufuata utaratibu wa kujadili na kupitisha Miswada ya Sheria ambayo hatimaye itabidi ipate kibali cha Rais, na Muswada hautakuwa Sheria mpaka uwe umepitishwa na Bunge na kukubaliwa na Rais kwa mujibu wa masharti ya ibara hii.

(2) Baada ya Muswada kuwasilishwa kwa Rais kwa ajili ya kupata kibali chake, Rais aweza kuukubali au kukataa kuukubali, na iwapo Rais atakataa kuukubali Muswada basi ataurudisha kwa Bunge pamoja na maelezo ya sababu zake za kukataa kuukubali Muswada huo.

(3) Baada ya Muswada kurudishwa kwa Bunge kwa mujibu wa masharti ya ibara hii, hauwezi kupelekwa tena kwa Rais kwa ajili ya kupata kibali chake kabla kumalizika muda wa miezi sita tangu uliporudishwa, isipokuwa kama katika hatua yake ya mwisho kwenye Bunge kabla haujapelekwa tena kwa Rais Muswada huo umeungwa mkono na Wabunge ambao idadi yao haipungui theluthi mbili ya Wabunge wote.

(4) Iwapo Muswada umerudishwa kwa Bunge na Rais, halafu ukaungwa mkono kwenye Bunge na Wabunge ambao idadi yao haipungui theluthi mbili ya Wabunge wote kama ilivyoelezwa katika ibara ndogo ya (3) na kupelekwa kwa Rais kwa ajili ya kupata kibali chake kwa mara ya pili kabla haujamalizika muda wa miezi sita tangu uliporudishwa, basi Rais atatakiwa kuukubali Muswada huo kabla ya kumalizika muda wa siku ishirini na moja tangu Muswada huo ulipowasilishwa kwake la sivyo basi itabidi alivunje Bunge.

©2025 Government of Tanzania. All rights reserved. No part of this document may be reproduced or distributed without permission of OAG.

(5) Masharti yaliyomo katika ibara hii au katika ibara ya 64 ya Katiba hii hayatalizuia Bunge kutunga Sheria na kuweka masharti ambayo yaweza kukabidhi kwa mtu yeyote au kwa idara yoyote ya Serikali madaraka ya kuweka Kanuni zenye nguvu ya kisheria au kuzipa nguvu ya kisheria Kanuni zozote zilizowekwa na mtu yeyote au idara yoyote ya Serikali.

Utaratibu wa kubadilisha Katiba hii na baadhi ya Sheria
Sheria Na. 15 ya 1984 ib. 14

**98.**–(1) Bunge laweza kutunga sheria kwa ajili ya kubadilisha masharti yoyote ya Katiba hii kwa kufuata Kanuni zifuatazo:

(a) Muswada wa Sheria kwa ajili ya kubadilisha masharti yoyote ya Katiba hii (isipokuwa yale yanayohusika na aya ya (b) ya ibara hii ndogo) au masharti yoyote ya sheria yoyote iliyotajwa katika Orodha ya Kwanza kwenye Nyongeza ya Pili utaungwa mkono kwa kura za Wabunge ambao idadi yao haipungui theluthi mbili ya Wabunge wote;

(b) Muswada wa Sheria kwa ajili ya kubadilisha masharti yoyote ya Katiba hii au masharti yoyote ya sheria yoyote yanayohusika na jambo lolote kati ya mambo yaliyotajwa katika Orodha ya Pili kwenye Nyongeza ya Pili iliyoko mwishoni mwa Katiba hii, utapitishwa tu iwapo utaungwa mkono kwa kura za Wabunge ambao idadi yao haipungui theluthi mbili ya Wabunge wote kutoka Tanzania Bara na theluthi mbili ya Wabunge wote kutoka Tanzania Zanzibar.

(2) Kwa madhumuni ya ufafanuzi wa masharti ya ibara ndogo ya (1), kubadilisha masharti ya Katiba hii au masharti ya sheria maana yake ifahamike kuwa ni pamoja na kurekebisha au kusahihisha masharti hayo au kufuta na kuweka masharti mengine badala yake au kusisitiza au kubadilisha matumizi ya masharti hayo.

Utaratibu wa kutunga sheria kuhusu mambo ya fedha
Sheria Na. 15 ya 1984; ib. 14

**99.**–(1) Bunge halitashughulikia jambo lolote kati ya mambo yanayohusika na ibara hii isipokuwa kama Rais amependekeza kwamba jambo hilo lishughulikiwe na Bunge na pendekezo hilo la Rais liwe limewasilishwa kwenye Bunge na Waziri.

(2) Mambo yanayohusika na ibara hii ni haya yafuatayo:

©2025 Government of Tanzania. All rights reserved. No part of this book may be reproduced or distributed without permission of OAG.

(a) Muswada wa Sheria kwa ajili ya lolote kati ya mambo yafuatayo:
   (i) kutoza kodi au kubadilisha kodi kwa namna nyingine yoyote isipokuwa kupunguza;
   (ii) kuagiza kwamba malipo au matumizi ya fedha yafanywe kutokana na Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali au mfuko wa Serikali mwingine wowote au kubadilisha kiwango hicho kwa namna nyingine yoyote isipokuwa kupunguza;
   (iii) kuagiza kwamba malipo au matumizi ya fedha yafanywe kutokana na Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali au mfuko wa Serikali mwingine wowote wakati ikifahamika kwamba fedha iliyomo katika mifuko hiyo haikupangiwa itolewe kwa ajili ya malipo au matumizi hayo, au kuagiza kwamba malipo au matumizi yanayofanywa kutokana na mifuko hiyo yaongezwe; au
   (iv) kufuta au kusamehe deni lolote linalotakiwa lilipwe kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano; na

(b) hoja au mabadiliko yoyote ya hoja kwa ajili ya lolote kati ya mambo yaliyoelezwa katika aya ya (a) ya ibara hii ndogo.

(3) Masharti ya ibara hii hayatatumika kwa Muswada wowote uliowasilishwa kwenye Bunge au Hoja yoyote iliyotolewa katika Bunge na Waziri au Naibu Waziri.

*Madaraka na Haki za Bunge*

Uhuru wa majadiliano na utaratibu wa shughuli
Sheria Na. 15 ya 1984 ib. 14

**100.**–(1) Kutakuwa na uhuru wa mawazo, majadiliano na utaratibu katika Bunge na uhuru huo hautavunjwa wala kuhojiwa na chombo chochote katika Jamhuri ya Muungano, au katika Mahakama au mahali penginepo nje ya Bunge.

(2) Bila ya kuathiri Katiba hii au masharti ya sheria nyingine yoyote inayohusika, Mbunge yeyote hatashtakiwa au kufunguliwa shauri la madai mahakamani kutokana na jambo lolote alilolisema au kulifanya ndani ya Bunge au alilolileta Bungeni kwa njia ya maombi, muswada, hoja au vinginevyo.

©2025 Government of Tanzania. All rights reserved. No part of this book may be reproduced or distributed without permission of OAG.

Kuhifadhi na kutilia nguvu uhuru wa majadiliano na wa shughuli
Sheria Na. 15 ya 1984 ib. 14

**101.** Bunge laweza kutunga sheria kwa ajili ya kuweka masharti ya kuwezesha mahakama na sheria kuhifadhi na kutilia nguvu uhuru wa mawazo, majadiliano na utaratibu wa shughuli katika Bunge ambao kwa mujibu wa ibara ya 100 umedhaminiwa na Katiba hii.

## SURA YA NNE

## SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR, BARAZA LA MAPINDUZI LA ZANZIBAR NA BARAZA LA WAWAKILISHI LA ZANZIBAR

### SEHEMU YA KWANZA

### SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR NA RAIS WA ZANZIBAR

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Mamlaka yake
Sheria Na. 45 ya 1980 ib. 55; 15 ya 1984 ib. 14; 34 ya 1994 ib. 16

**102.**–(1) Kutakuwa na Serikali ya Zanzibar itakayojulikana kama "Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar" ambayo itakuwa na mamlaka katika Zanzibar juu ya mambo yote yasiyo mambo ya Muungano kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii.

(2) Bila ya kuathiri masharti yaliyomo katika ibara hii na katika ibara zifuatazo katika Sura hii ya Katiba hii, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itaundwa na itatekeleza madaraka yake kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii na Katiba ya Zanzibar, 1984.

(3) Pamoja na madaraka yake mengine kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ndiye atakayewateua na kuwakabidhi madaraka Mawaziri na Naibu Mawaziri wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Mamlaka yake
Sheria Na. 15 ya 1980 ib. 14; 34 ya 1994 ib. 17

**103.**–(1) Kutakuwa na Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ambaye ndiye atakuwa Rais wa Zanzibar na Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na vile vile Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi la Zanzibar.

(2) Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kabla ya kushika madaraka yake ataapa mbele ya Jaji Mkuu wa Zanzibar kiapo cha kuilinda na kuitetea Katiba ya Jamhuri ya Muungano, na kiapo kingine chochote kwa mujibu wa

©2025 Government of Tanzania. All rights reserved. No part of this book may be reproduced or distributed without permission of OAG.

Katiba ya Zanzibar kinachohusika na utendaji wa kazi yake, kisha atashika na kutekeleza madaraka hayo kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii na Katiba ya Zanzibar, 1984.

(3) Pamoja na madaraka yake mengine kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ndiye atakayewateua na kuwakabidhi madaraka Mawaziri na Naibu Mawaziri wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Uchaguzi wa Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar
Sheria Na. 1 ya 1980 ib. 11; 15 ya 1984 ib. 14; 16 ya 1990 ib. 2; 20 ya 1992 ib. 14

**104.**–(1) Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar atachaguliwa na wananchi katika Tanzania Zanzibar kwa mujibu wa masharti ya Katiba ya Zanzibar, na kwa kufuata utaratibu uliowekwa kwa mujibu wa Sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar inayohusu uchaguzi kwa ujumla au uchaguzi wa Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

(2) Bila ya kuathiri masharti mengineyo ya Katiba hii, kiti cha Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kitakuwa ki-wazi, na uchaguzi wa Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar utafanyika ili kujaza nafasi hiyo kila mara litokeapo lolote kati ya mambo yafuatayo:

(a) baada ya Baraza la Wawakilishi kuvunjwa;
(b) baada ya Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kujiuzulu bila ya kulivunja Baraza la Wawakilishi kwanza;
(c) baada ya Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupoteza sifa za kushika nafasi ya madaraka ya kuchaguliwa;
(d) baada ya Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kushtakiwa katika Baraza la Wawakilishi kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar 1984 na kuondolewa katika madaraka;
(e) baada ya kuthibitishwa kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar 1984 kwamba Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar hawezi kumudu kazi na shughuli zake; au
(f) baada ya Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kufariki.

©2025 Government of Tanzania. All rights reserved. No part of this book may be reproduced or distributed without permission of OAG.

## SEHEMU YA PILI
## BARAZA LA MAPINDUZI LA ZANZIBAR

Baraza la Mapinduzi la Zanzibar na Kazi zake

**105.**–(1) Kutakuwa na Baraza la Mapinduzi la Zanzibar litakalokuwa na wajumbe wafuatao:

(a) Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi;
(b) Waziri Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar;
(c) Mawaziri wote wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar; na
(d) Wajumbe wengine watakaoteuliwa na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa mujibu wa masharti ya Katiba ya Zanzibar.

(2) Bila ya kuyaingilia madaraka ya Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kama Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Baraza la Mapinduzi litakuwa ndicho chombo kikuu cha kumshauri Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar juu ya mambo yote yanayohusika na utekelezaji wa madaraka yake ya uongozi na usimamizi wa shughuli za Serikali ya Zanzibar na pia utekelezaji wa madaraka yake juu ya shughuli zote za Serikali kuhusu mambo yote yasiyo Mambo ya Muungano, kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii na yale ya Katiba ya Zanzibar.

## SEHEMU YA TATU
## BARAZA LA WAWAKILISHI LA ZANZIBAR

Baraza la Wawakilishi Zanzibar na madaraka ya kutunga sheria za Zanzibar
Sheria Na. 1 ya 1980 ib. 93

**106.**–(1) Kutakuwa na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar. Baraza la Wawakilishi litakuwa na sehemu mbili; sehemu moja itakuwa ni ya wajumbe wa Baraza hilo waliochaguliwa na kuteuliwa kwa namna itakavyoelezwa na masharti ya Katiba ya Zanzibar, ya mwaka 1984, na ambao watajulikana kama wajumbe Wawakilishi, sehemu nyingine ya Baraza la Wawakilishi itakuwa ni Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika utekelezaji wa madaraka yake kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii na masharti ya Katiba ya Zanzibar, ya mwaka 1984.

©2025 Government of Tanzania. All rights reserved. No part of this book may be reproduced or distributed without permission of OAG.

(2) Iwapo kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii, masharti ya Katiba ya Zanzibar, 1984, au masharti ya Sheria yoyote iliyowekwa na inayotumika Zanzibar, jambo lolote lahitaji kuamuliwa au kutekelezwa na sehemu zote mbili za Baraza la Wawakilishi, basi jambo hilo halitahesabiwa kuwa limeamuliwa au limetekelezwa ipasavyo ila mpaka liwe limeamuliwa au limetekelezwa na Wajumbe Wawakilishi na vilevile Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kwa mujibu wa madaraka yao kuhusu jambo hilo.

(3) Madaraka yote ya kutunga Sheria katika Zanzibar juu ya mambo yote yasiyo Mambo ya Muungano yatakuwa mikononi mwa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.

Madaraka ya Baraza la Wawakilishi Sheria Na. 15 ya 1984 ib. 20

**107.**–(1) Rais wa Zanzibar kama sehemu moja ya Baraza la Wawakilishi atatekeleza madaraka yote aliyokabidhiwa na Katiba hii na pia Katiba ya Zanzibar kwa ajili hiyo.

(2) Wajumbe Wawakilishi kama Baraza la Wawakilishi watakuwa ndicho chombo kikuu cha Tanzania Zanzibar ambacho kitakuwa na madaraka kwa niaba ya wananchi wa Tanzania Zanzibar, kuisimamia na kuishauri Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na vyombo vyake vyote katika utekelezaji wa majukumu yake kwa mujibu wa Katiba hii na Katiba ya Zanzibar.

(3) Kwa madhumuni ya utekelezaji wa madaraka yake, Baraza la Wawakilishi laweza-

(a) kumuuliza Waziri yeyote wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar swali lolote kuhusu mambo ya umma katika Tanzania Zanzibar yaliyomo katika wajibu wake;

(b) kujadili utekelezaji wa kila Wizara ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar wakati wa Mkutano wa Baraza la Wawakilishi wa kila mwaka wa bajeti;

(c) kujadili na kuidhinisha mpango wowote wa muda mrefu au wa muda mfupi unaokusudiwa kutekelezwa Tanzania Zanzibar, na kutunga sheria ya kusimamia utekelezaji wa mpango huo;

©2025 Government of Tanzania. All rights reserved. No part of this book may be reproduced or distributed without permission of OAG.

(d) kutunga sheria pale ambapo utekelezaji unahitaji kuwapo sheria; na

(e) kutayarisha au kuagiza itayarishwe na kuwasilisha kwenye Chama chochote cha siasa taarifa kuhusu jambo lolote ambalo liko chini ya mamlaka ya Bunge.

## SURA YA TANO

## UTOAJI HAKI KATIKA JAMHURI YA MUUNGANO, MAHAKAMA KUU YA JAMHURI YA MUUNGANO, TUME YA KUAJIRI YA MAHAKAMA YA TANZANIA BARA, MAHAKAMA KUU YA ZANZIBAR, MAHAKAMA YA RUFANI YA JAMHURI YA MUUNGANO NA MAHAKAMA MAALUM YA KATIBA YA JAMHURI YA MUUNGANO

### SEHEMU YA KWANZA

### UTOAJI HAKI KATIKA JAMHURI YA MUUNGANO

Mamlaka ya utoaji haki Sheria Na. 2 ya 2000 ib. 17; 1 ya 2005 ib. 16; TS. Na. 150 la 2005

**107A.**–(1) Mamlaka yenye kauli ya mwisho ya utoaji haki katika Jamhuri ya Muungano itakuwa ni Mahakama.

(2) Katika kutoa uamuzi wa mashauri ya madai na jinai kwa kuzingatia sheria, Mahakama zitafuata kanuni zifuatazo, yaani-

(a) kutenda haki kwa wote bila ya kujali hali ya mtu kijamii au kiuchumi;

(b) kutochelewesha haki bila sababu ya kimsingi;

(c) kutoa fidia ipasayo kwa watu wanaoathirika kutokana na makosa ya watu wengine, na kwa mujibu wa sheria mahususi iliyotungwa na Bunge;

(d) kukuza na kuendeleza usuluhishi baina ya wanaohusika katika migogoro; na

(e) kutenda haki bila kufungwa kupita kiasi na masharti ya kiufundi yanayoweza kukwamisha haki kutendeka.

©2025 Government of Tanzania. All rights reserved. No part of this book may be reproduced or distributed without permission of OAG.

Uhuru wa Mahakama
Sheria Na. 3 ya 2000 ib. 17

**107B**. Katika kutekeleza mamlaka ya utoaji haki, mahakama zote zitakuwa huru na zitalazimika kuzingatia tu masharti ya Katiba na yale ya sheria za nchi.

## SEHEMU YA PILI
## MAHAKAMA KUU YA JAMHURI YA MUUNGANO

Mahakama Kuu ya Jamhuri ya Muungano na Mamlaka yake
Sheria Na. 14 ya 1979 ib. 6

**108.**–(1) Kutakuwa na Mahakama Kuu ya Jamhuri ya Muungano (itakayojulikana kwa kifupi kama "Mahakama Kuu") ambayo mamlaka yake yatakuwa kama ilivyoelezwa katika Katiba hii au katika sheria nyingine yoyote.

(2) Iwapo Katiba hii au sheria nyingine yoyote haikutamka wazi kwamba shauri la aina iliyotajwa mahsusi litasikilizwa kwanza katika Mahakama ya ngazi iliyotajwa mahsusi kwa ajili hiyo, basi Mahakama Kuu itakuwa na mamlaka ya kusikiliza kila shauri la aina hiyo, hali kadhalika, Mahakama Kuu itakuwa na uwezo wa kutekeleza shughuli yoyote ambayo kwa mujibu wa mila za kisheria zinazotumika Tanzania shughuli ya aina hiyo kwa kawaida hutekelezwa na Mahakama Kuu:

Isipokuwa kwamba masharti ya ibara hii ndogo yatatumika bila ya kuathiri mamlaka ya Mahakama ya Rufani ya Tanzania kama ilivyoelezwa katika Katiba hii au katika sheria nyingine yoyote.

Majaji wa Mahakama Kuu na uteuzi wao
Sheria Na. 14 ya 1979 ib. 6; 15 ya 1984 ib. 22; 14 ya 1990 ib. 5

**109.**–(1) Kutakuwa na Jaji Kiongozi wa Mahakama Kuu (ambaye katika ibara zifuatazo kwenye Katiba hii atatajwa tu kwa kifupi kama "Jaji Kiongozi") na Majaji wengine wa Mahakama Kuu wasiopungua thelathini watakaoteuliwa na Rais baada ya kushauriana na Tume ya Utumishi wa Mahakama.

(2) Bila ya kuathiri masharti ya Katiba hii au sheria nyingine yoyote kuhusu madaraka ya Jaji Mkuu aliyetajwa katika ibara ya 118, Jaji Kiongozi atakuwa ndiye msaidizi maalum wa Jaji Mkuu katika utendaji wa kazi katika Mahakama Kuu na mahakama nyinginezo zote za ngazi ya chini yake, na katika madaraka hayo Jaji Kiongozi atatekeleza kazi na shughuli atakazoagizwa au kuelekezwa mara kwa mara na Jaji Mkuu,

©2025 Government of Tanzania. All rights reserved. No part of this book may be reproduced or distributed without permission of OAG.

na kwa madhumuni ya ibara hii, Jaji Kiongozi atajulikana pia kama Mkuu wa Mahakama Kuu.

(3) Mbali ya madaraka yake ya kawaida ya Jaji wa Mahakama Kuu kama Majaji wengine wote wa Mahakama Kuu, Jaji Kiongozi atakuwa pia na mamlaka ya kutekeleza kazi na shughuli zote zinazoambatana na mamlaka ya Mahakama Kuu ambazo kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii au ya sheria nyingine yoyote au kufuatana na mila za kisheria zinazotumika Tanzania hutakiwa zitekelezwe na Mkuu wa Mahakama Kuu:

Isipokuwa kwamba masharti ya ibara hii ndogo hayatatumika kwa ajili ya utekelezaji wa kazi au shughuli ambazo kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii au ya Sheria nyingine yoyote au kufuatana na mila za kisheria zinazotumika Tanzania zimetajwa mahsusi au zinafahamika kuwa ni kazi au shughuli zinazotakiwa kutekelezwa tu na Jaji Mkuu.

(4) Kwa madhumuni ya kuondoa mashaka juu ya ufafanuzi au utekelezaji wa masharti ya ibara ndogo ya (2) na ya (3) ya ibara hii, inatamkwa rasmi hapa kwamba isipokuwa kama masharti ya Katiba hii au ya sheria nyingine yoyote yameagiza vinginevyo, Jaji Mkuu atakuwa na uwezo wa kutoa kwa Jaji Kiongozi mara kwa mara maagizo au maelekezo kuhusu utendaji wa kazi na shughuli zake kama Mkuu wa Mahakama Kuu; vilevile, Jaji Mkuu atakuwa na uwezo wa kukasimu kwa Jaji Kiongozi baadhi ya madaraka yake ya uongozi na usimamizi juu ya utekelezaji wa kazi katika Mahakama Kuu na mahakama nyinginezo zote za ngazi ya chini yake, na kila inapohitajika, Jaji Mkuu anaweza kutekeleza yeye mwenyewe moja kwa moja madaraka yake yoyote aliyoyakasimu kwa Jaji Kiongozi.

(5) Kazi ya Jaji wa Mahakama Kuu haitafutwa wakati yupo mtu aliyeshika madaraka ya kiti cha Jaji.

(6) Bila ya kuathiri masharti ya ibara ndogo ya (8) ya Ibara hii, mtu aweza tu kuteuliwa kuwa Jaji wa Mahakama Kuu ikiwa ana sifa maalum, kama ilivyofafanuliwa katika ibara ndogo ya (7) ya ibara hii, na awe mtu ambaye amekuwa na mojawapo ya sifa maalum kwa muda usiopungua miaka kumi.

©2025 Government of Tanzania. All rights reserved. No part of this book may be reproduced or distributed without permission of OAG.

(7) Kwa madhumuni ya ufafanuzi wa Ibara ndogo za (6), (8) na (10) ya ibara hii, "sifa maalumu" maana yake ni mtu aliye na shahada ya sheria kutoka chuo kikuu kinachotambuliwa na mamlaka ya ithibati Tanzania na-

(a) amekuwa hakimu;

(b) amefanya kazi katika utumishi wa umma akiwa na sifa za kufanya kazi ya uwakili au ni wakili wa kujitegemea; au

(c) ana sifa ya kusajiliwa kuwa wakili,

na amekuwa na sifa hizo mfululizo kwa muda usiopungua miaka kumi.

(8) Iwapo Rais atatosheka kwamba ijapokuwa mtu mwenye sifa mojawapo ya hizo sifa maalum hakuwa nayo sifa hiyo kwa muda usiopungua miaka kumi, lakini mtu huyo ana uwezo, ujuzi na kwa kila hali anafaa kukabidhiwa madaraka ya Jaji wa Mahakama Kuu na kuna sababu za kumfanya mtu huyo astahili kukabidhiwa madaraka hayo, basi Rais aweza kutengua lile sharti la kuwa na sifa maalum kwa muda usiopungua miaka kumi na baada ya kushauriana na Tume ya Utumishi wa Mahakama, Rais aweza kumteua mtu huyo kuwa Jaji wa Mahakama Kuu.

(9) Ikitokea kwamba kiti cha Jaji Kiongozi kitakuwa wazi au kwamba Jaji Kiongozi atashindwa kutekeleza kazi zake kwa sababu yoyote, basi kazi hizo zitatekelezwa na Jaji mmojawapo atakayeteuliwa na Rais kwa ajili hiyo, na Jaji huyo atatekeleza kazi hizo mpaka atakapoteuliwa Jaji Kiongozi mwingine na kushika madaraka ya kiti cha Jaji Kiongozi au mpaka Jaji Kiongozi mwenyewe ambaye alikuwa hamudu kazi zake atakaporejea kazini.

(10) Ikitokea kwamba kiti cha Jaji yeyote kitakuwa wazi au ikiwa Jaji yeyote atateuliwa kuwa Kaimu Jaji Kiongozi au kama atashindwa kutekeleza kazi zake kwa sababu yoyote, au kama Jaji Mkuu atamshauri Rais kuwa kazi za Mahakama Kuu zilivyo wakati huo zahitaji ateuliwe Kaimu Jaji, basi Rais aweza, baada ya kushauriana na Jaji Mkuu kama kawaida, kumteua Kaimu Jaji kutoka miongoni mwa watu wenye sifa maalum:

©2025 Government of Tanzania. All rights reserved. No part of this book may be reproduced or distributed without permission of OAG.

Isipokuwa kwamba-

(a) mtu hatahesabiwa kuwa hastahili kuteuliwa kwa mujibu wa masharti ya ibara hii ndogo kwa sababu tu kwamba ametimiza umri uliotajwa katika ibara ndogo ya (1) ya ibara ya 110 ya Katiba hii;

(b) kwa madhumuni ya kumteua Kaimu Jaji kwa mujibu wa masharti ya ibara hii ndogo, Rais aweza kutengua lile sharti la kuwa na sifa maalum kwa muda usiopungua miaka kumi kwa sababu kama zile zilizotajwa katika ibara ndogo ya (8) ya ibara hii.

(11) Mtu yeyote atakayeteuliwa kuwa Kaimu Jaji kwa mujibu wa masharti ya ibara ndogo ya (10) ya ibara hii, ataendelea kufanya kazi kama Kaimu Jaji kwa muda wowote utakaotajwa wakati wa kuteuliwa kwake au, kama muda haukutajwa, mpaka uteuzi wake utakapofutwa na Rais, lakini bila ya kujali kwamba muda wake wa kazi umemalizika au kwamba uteuzi wake umefutwa, mtu huyo aweza kuendelea kufanyakazi kama Kaimu Jaji mpaka amalize kutayarisha na kutoa hukumu au mpaka akamilishe shughuli nyingine yoyote inayohusika na mashauri ambayo alikwisha anza kuyasikiliza kabla muda wake wa kazi haujamalizika au kabla ya uteuzi wake haujafutwa.

Muda wa Majaji wa Mahakama Kuu kushika madaraka
Sheria Na. 14 ya 1979 ib. 6; 15 ya 1984 ib. 22 na 23; 12 ya 1995 ib.17; 1 ya 2005 ib. 18

**110.**–(1) Kila Jaji wa Mahakama Kuu atalazimika kuacha kazi yake atakapotimiza umri wa miaka sitini lakini masharti ya ibara hii ndogo yatatumika bila ya kuathiri masharti yafuatayo katika ibara hii.

(2) Jaji yeyote wa Mahakama Kuu anaweza kustaafu kazi katika utumishi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wakati wowote baada ya kutimiza umri wa miaka hamsini na tano, isipokuwa kama Rais ataagiza kwamba asistaafu, na iwapo Rais ataagiza hivyo, basi huyo Jaji atakayehusika na maagizo hayo ya Rais hatakuwa na haki ya kustaafu mpaka upite kwanza muda wowote utakaotajwa na Rais kwa ajili hiyo.

(3) Iwapo Rais ataona kuwa kwa ajili ya manufaa ya Umma inafaa Jaji aliyetimiza umri wa miaka sitini aendelee kufanya kazi, na huyo Jaji mwenyewe anakubali kwa maandishi

©2025 Government of Tanzania. All rights reserved. No part of this book may be reproduced or distributed without permission of OAG.

kuendelea kufanya kazi, basi Rais aweza kuagiza kuwa Jaji huyo aendelee kufanya kazi kwa muda wowote utakaotajwa na Rais.

(4) Bila ya kujali kwamba Jaji ametimiza umri ambao analazimika kuacha kazi kwa mujibu wa masharti ya ibara hii, mtu anayefanya kazi ya Jaji wa Mahakama Kuu aweza kuendelea kufanya kazi baada ya kutimiza umri huo mpaka amalize kutayarisha na kutoa hukumu au mpaka akamilishe shughuli nyingine yoyote inayohusika na mashauri ambayo alikwisha anza kuyasikiliza kabla hajatimiza umri huo wa kuacha kazi.

Utaratibu wa kushughulikia nidhamu ya Majaji wa Mahakama Kuu
Sheria Na. 1 ya 2005 ib. 19

**110A**–(1) Utaratibu wa kushughulikia nidhamu ya Majaji, kwa sababu mbali na zile zilizoainishwa katika ibara ndogo ya (2), utakuwa kama utakavyoelekezwa na Sheria itakayotungwa na Bunge.

(2) Jaji wa Mahakama Kuu aweza tu kuondolewa katika madaraka ya kazi kwa sababu ya kushindwa kutekeleza kazi yake (ama kutokana na maradhi au sababu nyingine yoyote) au kwa sababu ya tabia mbaya inayoathiri maadili ya kazi ya Jaji au sheria ya maadili ya viongozi wa umma; na hataweza kuondolewa kazini ila kwa mujibu wa masharti ya ibara ndogo ya (4) ya ibara hii.

(3) Iwapo Rais anaona kuwa suala la kumwondoa Jaji kazini lahitaji kuchunguzwa, basi katika hali hiyo utaratibu utakuwa kama ifuatavyo:

(a) Rais anaweza baada ya kushauriana na Jaji Mkuu, kumsimamisha kazi Jaji huyo;

(b) Rais atateua Tume ambayo itakuwa na Mwenyekiti na Wajumbe wengine wasiopungua wawili. Na huyo Mwenyekiti na angalau nusu ya Wajumbe wengine wa Tume hiyo itabidi wawe watu ambao ni Majaji wa Mahakama Kuu au Mahakama ya Rufani katika nchi yoyote iliyomo kwenye Jumuiya ya Madola;

(c) Tume hiyo itachunguza shauri lote halafu itatoa taarifa kwa Rais kuhusu maelezo ya shauri lolote na itamshauri Rais kama huyo Jaji anayehusika aondolewe kazini kwa mujibu wa masharti ya ibara hii kwa sababu

©2025 Government of Tanzania. All rights reserved. No part of this book may be reproduced or distributed without permission of OAG.

ya kushindwa kufanya kazi kutokana na maradhi au sababu nyingine yoyote au kwa sababu ya tabia mbaya.

(4) Ikiwa Tume iliyoteuliwa kwa mujibu wa masharti ya ibara ndogo ya (3) itamshauri Rais kwamba Jaji ambaye habari zake zimechunguzwa na hiyo Tume aondolewe kazini kwa sababu ya kushindwa kufanya kazi kutokana na maradhi au sababu nyingine yoyote au kwa sababu ya tabia mbaya, basi Rais atamwondoa kazini Jaji huyo anayehusika na utumishi wa Jaji huyo utakuwa umekoma.

(5) Ikiwa suala la kumwondoa Jaji kazini limepelekwa kwenye Tume kwa ajili ya uchunguzi kwa mujibu wa masharti ya ibara ndogo ya (3) ya ibara hii, Rais aweza kumsimamisha kazi Jaji huyo anayehusika, na Rais aweza wakati wowote kufuta uamuzi huo wa kumsimamisha kazi Jaji huyo, na kwa hali yoyote uamuzi huo utabatilika ikiwa Tume itamshauri Rais kwamba Jaji huyo asiondolewe kazini.

(6) Masharti ya ibara hii yatatumika bila ya kuathiri masharti ya ibara ndogo ya (11) ya ibara ya 109 ya Katiba hii.

Kiapo cha Majaji
Sheria Na.
14 ya 1979 ib. 6;
15 ya 1984 ib. 22

**111.** Jaji wa Mahakama Kuu hatashika madaraka yake ila mpaka awe ameapishwa kwanza kiapo cha uamunifu na pia kiapo kingine chochote kinachohusika na utendaji wa kazi kitakachowekwa kwa mujibu wa sheria iliyotungwa na Bunge.

## SEHEMU YA TATU
## TUME YA UTUMISHI WA MAHAKAMA

Tume ya Utumishi wa Mahakama
Sheria Na.
14 ya 1979 ib. 7;
15 ya 1984 ib. 22;
14 ya 1990 ib. 6;
3 ya 2000 ib. 17;
1 ya 2005; ib. 20

**112.**–(1) Kutakuwa na Tume ya Ushauri wa Uteuzi wa Majaji na Ajira ya Mahakimu wa Mahakama za Tanzania Bara ambayo katika Katiba hii itaitwa "Tume ya Utumishi wa Mahakama".

(2) Wajumbe wa Tume hiyo watakuwa:

(a) Jaji Mkuu ambaye atakuwa Mwenyekiti;

(b) Mwanasheria Mkuu wa Serikali;

(c) Jaji mmoja wa Mahakama ya Rufaa atakayeteuliwa kwa ajili hiyo na Rais baada ya kushauriana na Jaji Mkuu;

(d) Jaji Kiongozi; na



©2025 Government of Tanzania. All rights reserved. No part of this book may be reproduced or distributed without permission of OAG.

(e) Wajumbe wawili watakaoteuliwa na Rais.

(3) Mtu hataweza kuteuliwa kuwa mjumbe wa Tume kwa mujibu wa masharti ya aya ya (e) ya ibara ndogo ya (2) ya ibara hii ikiwa mtu huyo ni Mbunge au ni mtu mwenye madaraka ya aina nyingine yoyote iliyotajwa kwa ajili hiyo na sheria iliyotungwa na Bunge.

(4) Katika kutekeleza majukumu yake, Tume yaweza kukasimu kazi zake kwa Kamati mbalimbali zitakazoundwa kwa mujibu wa sheria itakayotungwa na Bunge.

Majukumu na Madaraka ya Tume
Sheria Na. 14 ya 1979 ib. 7; 15 ya 1984 ib. 22 na 24; 1 ya 2005 ib. 20

**113.**–(1) Majukumu ya Tume yatakuwa ni-

(a) kumshauri Rais kuhusu uteuzi wa Majaji wa Mahakama Kuu;

(b) kumshauri Rais kuhusu masuala ya nidhamu ya Majaji;

(c) kumshauri Rais kuhusu mishahara na maslahi ya Majaji;

(d) kumshauri Rais kuhusu uteuzi na nidhamu kwa ajili ya Msajili wa Mahakama ya Rufani na Msajili wa Mahakama Kuu;

(e) kuajiri mahakimu na kusimamia nidhamu yao; na

(f) kuunda kamati mbalimbali kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu yake.

(2) Madaraka ya uteuzi, kudhibiti nidhamu na ya kuwaondoa kazini Majaji yatakuwa mikononi mwa Rais kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii.

(3) Madaraka ya uteuzi, kuwathibitisha kazini, kudhibiti nidhamu na ya kuwaondoa kazini wasajili wa Mahakama ya Rufani na Mahakama Kuu yatakuwa mikononi mwa Rais.

(4) Madaraka ya kuajiri, kuwathibitisha kazini, kudhibiti nidhamu na kuwaondoa kazini mahakimu wa Mahakama za Tanzania Bara yatakuwa mikononi mwa Tume iliyotajwa katika ibara ya 112.

(5) Bunge linaweza kutunga sheria itakayoweka masharti ya utekelezaji wa majukumu ya Tume.

©2025 Government of Tanzania. All rights reserved. No part of this book may be reproduced or distributed without permission of OAG.

Uanachama katika Vyama vya Siasa
Sheria Na. 34 ya 1994 ib. 18; 1 ya 2005 ib. 20

**113A**. Itakuwa ni marufuku kwa Jaji wa Mahakama ya Rufani, Jaji wa Mahakama Kuu, Msajili wa Mahakama ya ngazi yoyote, Hakimu wa ngazi yoyote kujiunga na chama chochote cha siasa, isipokuwa tu kwamba atakuwa na haki ya kupiga kura iliyotajwa katika ibara ya 5 ya Katiba hii.

## SEHEMU YA NNE
## MAHAKAMA KUU YA ZANZIBAR

Mahakama Kuu ya Zanzibar
Sheria Na. 15 ya 1984 ib. 22

**114.** Kwa madhumuni ya ufafanuzi wa Sura hii ya Katiba hii, ifahamike kwamba masharti yaliyomo katika Sura hii hayazuii kuendelea kuwapo au kuanzishwa, kwa mujibu wa sheria zinazotumika Zanzibar kwa Mahakama Kuu ya Zanzibar au Mahakama zilizo chini ya Mahakama Kuu ya Zanzibar.

Mamlaka ya Mahakama Kuu ya Zanzibar
Sheria Na. 15 ya 1984 ib. 22

**115.**–(1) Bila ya kuathiri masharti ya ibara ya 83 na 116 ya Katiba hii, mamlaka ya Mahakama Kuu ya Zanzibar yatakuwa kama itakavyoelezwa katika sheria zinazotumika Zanzibar.

(2) Bila ya kuathiri masharti ya Katiba hii au sheria nyingine yoyote iliyotungwa na Bunge, iwapo sheria yoyote iliotungwa na Bunge inayotumika Tanzania Bara na vilevile Tanzania Visiwani imekabidhi madaraka yoyote kwa Mahakama Kuu, basi Mahakama Kuu ya Zanzibar yaweza kutekeleza madaraka hayo kwa kiasi kile kile inavyoweza kutekeleza Mahakama Kuu ya Jamhuri ya Muungano.

## SEHEMU YA TANO
## MAHAKAMA YA RUFANI YA JAMHURI YA MUUNGANO

Tafsiri
Sheria Na. 15 ya 1984 ib. 25 na 26; 1 ya 2005 ib. 21

**116.**–(1) Bila ya kuathiri masharti ya ibara ndogo ya (2), Jaji Mkuu hatakuwa na madaraka juu ya jambo lolote linalohusu muundo na uendeshaji wa shughuli za siku hadi siku za Mahakama zilizoundwa kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar au sheria yoyote ya Tanzania Zanzibar.

©2025 Government of Tanzania. All rights reserved. No part of this book may be reproduced or distributed without permission of OAG.

(2) Jaji Mkuu atashauriana mara kwa mara na Jaji Mkuu wa Zanzibar kuhusu uendeshaji wa shughuli za Mahakama ya Rufani kwa jumla, na pia kuhusu uteuzi wa Majaji wa Rufani.

Mahakama ya Rufani ya Jamhuri ya Muungano na Mamlaka yake
Sheria Na. 14 ya 1979 ib. 8; 15 ya 1984 ib. 27

**117.**–(1) Kutakuwa na Mahakama ya Rufani ya Jamhuri ya Muungano (itakayojulikana kwa kifupi kama "Mahakama ya Rufani") ambayo mamlaka yake yatakuwa kama ilivyoelezwa katika Katiba hii au katika Sheria nyingine yoyote.

(2) Mahakama ya Rufani haitakuwa na mamlaka yoyote kuhusu usuluhishi wa suala lolote litakaloshughulikiwa kwa mujibu wa masharti ya ibara ya 126 ya Katiba hii ambayo inahusu ubishi kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

(3) Kazi ya Mahakama ya Rufani itakuwa ni kusikiliza na kutoa uamuzi juu ya kila rufaa inayoletwa mbele ya Mahakama ya Rufani kutokana na hukumu au uamuzi wa namna nyingine yoyote wa Mahakama Kuu au Mahakama yoyote ya chini iliyopewa mamlaka maalum ya Mahakama Kuu.

(4) Sheria iliyotungwa kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii na Bunge au na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar yaweza kuweka masharti yatakayoeleza utaratibu wa kupeleka rufaa mbele ya Mahakama ya Rufani, nyakati na sababu za kukata rufaa na namna ya kushughulikia rufaa hizo.

Jaji Mkuu na Majaji wa Mahakama ya Rufani na uteuzi wao
Sheria Na. 14 ya 1979 ib. 8; 15 ya 1984 ib. 28; 7 ya 1994 Fungu la 8(1)(k) 1 ya 2005 ib. 22

**118.**–(1) Kutakuwa na Jaji Mkuu wa Mahakama ya Tanzania (ambaye katika Ibara zifuatazo kwenye Katiba atatajwa tu kwa kifupi kama "Jaji Mkuu") na Majaji wengine wa Rufani wasiopungua wanne, isipokuwa kwamba kikao maalum cha Mahakama nzima kitakamilika kama kitakuwa na Majaji wa Rufani wasiopungua watano.

(2) Jaji Mkuu atateuliwa na Rais kutoka miongoni mwa watu wenye sifa za kuwa Jaji wa Rufani na atakuwa ndiye Kiongozi wa Mahakama ya Rufani na pia Mkuu wa Mahakama ya Tanzania kama ilivyofafanuliwa katika ibara ya 116 ya Katiba na atashika madaraka ya Jaji Mkuu mpaka atakapotimiza umri wa kustaafu kama Jaji wa Rufani, isipokuwa kama:

(a) atajiuzulu;

©2025 Government of Tanzania. All rights reserved. No part of this book may be reproduced or distributed without permission of OAG.

(b) kiti chake kitakuwa wazi kutokana na maradhi au kifo;
(c) atavuliwa wadhifa wa Jaji Mkuu na Rais.

(3) Majaji wengine wa Rufani watateuliwa na Rais, baada ya kushauriana na Jaji Mkuu, kutoka miongoni mwa watu wenye sifa za kuteuliwa kuwa Majaji wa Mahakama Kuu ya Jamhuri ya Muungano zilivyoainishwa katika ibara ya 109 ya Katiba au kutoka miongoni mwa watu wanaoweza kuteuliwa kuwa Majaji wa Mahakama Kuu ya Zanzibar kwa mujibu wa sheria zinazotumika Zanzibar na wamekuwa na sifa hizo kwa muda usiopungua miaka kumi na tano.

(4) Iwapo itatokea kwamba:
(a) Kiti cha Jaji Mkuu kitakuwa wazi;
(b) Jaji Mkuu hayupo Tanzania; au
(c) Jaji Mkuu atashindwa kutekeleza kazi yake kwa sababu yoyote, na, Rais ataona kuwa kwa muda wa tukio lolote kati ya hayo matatu inafaa kumteua Kaimu Jaji Mkuu, basi Rais anaweza kumteua Kaimu Jaji Mkuu kutoka miongoni mwa Majaji wa Rufani.

(5) Kaimu Jaji Mkuu atatekeleza kazi za Jaji Mkuu mpaka atakapoteuliwa Jaji Mkuu mwingine au mpaka Jaji Mkuu ambaye alikuwa hayupo Tanzania au alikuwa hamudu kazi zake atakaporejea kazini.

(6) Ikitokea kwamba kiti cha Jaji wa Rufani kitakuwa wazi au endapo Jaji wa Rufani yeyote atateuliwa kuwa Kaimu Jaji Mkuu au kama Jaji wa Rufani atashindwa kutekeleza kazi zake kwa sababu yoyote, au Jaji Mkuu atamshauri Rais kuwa kazi za Mahakama ya Rufani ilivyo wakati huo zahitaji ateuliwe Kaimu Jaji wa Rufani, basi Rais aweza, baada ya kushauriana na Jaji Mkuu, kumteua Kaimu Jaji wa Rufani kutoka miongoni mwa watu ambao wanaweza kuteuliwa kuwa Majaji wa Rufani kwa mujibu wa masharti ya ibara ndogo ya (4) ya ibara hii.

(7) Mtu yeyote atakayeteuliwa kuwa Kaimu Jaji wa Rufani ataendelea kufanya kazi kama Kaimu Jaji wa Rufani kwa muda wowote utakaotajwa wakati wa kuteuliwa kwake, au, endapo muda haukutajwa, mpaka uteuzi wake utakapofutwa na Rais, lakini bila ya kujali kwamba muda wake wa kazi umemalizika

©2025 Government of Tanzania. All rights reserved. No part of this book may be reproduced or distributed without permission of OAG.

au kwamba uteuzi wake umefutwa, mtu huyo anaweza kuendelea kufanya kazi kama Kaimu Jaji wa Rufani mpaka amalize kutayarisha na kutoa hukumu au mpaka akamilishe shughuli nyingine yoyote inayohusika na rufaa au mashauri mengine yoyote ambayo alikwishaanza kuyasikiliza kabla ya muda wake wa kazi haujamalizika au uteuzi wake haujafutwa.

(8) Kwa madhumuni ya kuondoa mashaka juu ya ufafanuzi wa masharti ya ibara ndogo ya (1) ya ibara hii na ibara ya 119 ya Katiba hii, inatamkwa rasmi hapa kwamba mtu aliyeteuliwa kuwa Kaimu Jaji wa Rufani atakuwa na mamlaka kamili ya Jaji wa Rufani na atatekeleza kazi zote za Jaji wa Rufani na kwamba idadi ya Majaji iliyotajwa katika ibara ya 122 ya Katiba hii, haitaathirika kwa sababu tu mmoja au zaidi ya Majaji wa Rufani katika kikao chochote ni Kaimu Jaji wa Rufani.

(9) Ofisi ya Jaji wa Rufani haitafutwa wakati yupo mtu aliyeshika madaraka ya kiti cha Jaji wa Rufani.

Mamlaka ya Majaji wa Mahakama ya Rufani
Sheria Na. 14 ya 1979 ib. 8; 15 ya 1984 ib. 29

**119.** Jaji yeyote wa Mahakama ya Rufani hatakuwa na mamlaka ya kusikiliza shauri lolote katika Mahakama Kuu au katika Mahakama ya Hakimu ya ngazi yoyote:

Isipokuwa kwamba iwapo Jaji yeyote wa Mahakama Kuu atateuliwa kuwa Jaji wa Mahakama ya Rufani, basi hata baada ya kuteuliwa kwake kuwa Jaji wa Mahakama ya Rufani, Jaji huyo aweza kuendelea kufanya kazi zake katika Mahakama Kuu mpaka amalize kutayarisha na kutoa hukumu au mpaka akamilishe shughuli nyingine yoyote inayohusika na mashauri ambayo alikwisha anza kuyasikiliza kabla hajateuliwa kuwa Jaji wa Mahakama ya Rufani na kwa ajili hiyo itakuwa halali kwake kutoa hukumu au uamuzi mwingine wowote unaohusika kwa kutumia na kutaja madaraka aliyoshika kabla ya kuteuliwa kuwa Jaji wa Mahakama ya Rufani, lakini endapo hatimaye hukumu hiyo au uamuzi huo mwingine utapingwa kwa njia ya rufaa itakayofikishwa mbele ya Mahakama ya Rufani, basi katika hali hiyo Jaji huyo wa Mahakama ya Rufani, hatakuwa na mamlaka ya kusikiliza rufaa hiyo.

©2025 Government of Tanzania. All rights reserved. No part of this book may be reproduced or distributed without permission of OAG.

Muda wa utumishi wa Majaji wa Rufani Sheria Na. 14 ya 1979 ib. 8; 15 ya 1984 ib. 30; 1 ya 2005 ib. 23

**120.**–(1) Kila Jaji wa Rufani atalazimika kuacha kazi yake atakapotimiza umri wa miaka sitini na tano, lakini masharti ya ibara hii ndogo yatatumika bila kuathiri masharti yafuatayo katika ibara hii.

(2) Jaji yeyote wa Rufani aweza kustaafu kazi ya Ujaji wa Rufani wakati wowote baada ya kutimiza umri wa miaka sitini, isipokuwa kama Rais ataagiza kwamba asistaafu, na iwapo Rais ataagiza hivyo, basi huyo Jaji wa Rufani atakayehusika na maagizo hayo ya Rais hatakuwa na haki ya kustaafu mpaka upite kwanza muda wowote utakaotajwa na Rais kwa ajili hiyo.

(3) Iwapo Rais ataona kuwa kwa ajili ya manufaa ya umma inafaa Jaji wa Rufani aliyetimiza umri wa miaka sitini na tano aendelee kufanya kazi, na Jaji huyo wa Rufani anakubali kwa maandishi kuendelea kufanya kazi, basi Rais aweza kuagiza kuwa Jaji huyo wa Rufani aendelee kufanya kazi kwa muda wowote utakaotajwa na Rais.

(4) Bila ya kujali kwamba Jaji wa Rufani ametimiza umri ambao analazimika kuacha kazi kwa mujibu wa masharti ya ibara hii, mtu anayefanya kazi ya Jaji wa Rufani aweza kuendelea kufanya kazi baada ya kutimiza umri huo mpaka amalize kutayarisha na kutoa hukumu au mpaka akamilishe shughuli nyingine yoyote inayohusika na mashauri ambayo alikwisha anza kuyasikiliza kabla hajatimiza umri huo wa kuacha kazi.

Utaratibu wa kushughulikia nidhamu ya Majaji wa Rufani Sheria Na. 1 ya 2005 ib. 24

**120A**–(1) Utaratibu wa kushughulikia nidhamu ya Majaji wa Rufani kwa makosa mbali na yale yaliyoainishwa katika ibara ndogo ya (2) utakuwa kama utakavyoelekezwa na Sheria itakayotungwa na Bunge.

(2) Jaji wa Rufani aweza kuondolewa katika madaraka ya kazi ya Jaji wa Rufani kwa sababu ya kushindwa kutekeleza kazi zake (ama kutokana na maradhi au sababu nyingine yoyote) au kwa sababu ya tabia mbaya, na hataweza kuondolewa kazini ila kwa mujibu wa masharti ya utaratibu unaofanana na ule

©2025 Government of Tanzania. All rights reserved. No part of this book may be reproduced or distributed without permission of OAG.

uliowekwa kwa ajili ya kumwondoa kazini Jaji wa Mahakama Kuu kama ilivyoelezwa katika ibara ndogo ya (2) na ya (3) ya ibara ya 110A ya Katiba hii, na kwa ajili hiyo masharti ya ibara ndogo ya (4) ya ibara hiyo ya 110A yatatumika kwa Jaji wa Rufani kwa namna ile ile yanavyotumika kwa Jaji wa Mahakama Kuu.

(3) Masharti ya ibara hii yatatumika bila ya kuathiri masharti ya ibara ndogo ya (5) ya ibara ya 118 ya Katiba hii.

Kiapo cha Majaji wa Mahakama ya Rufani
Sheria Na. 14 ya 1979 ib. 8; 15 ya 1984 ib. 31

**121.** Jaji wa Mahakama ya Rufani hatashika madaraka yake ila mpaka awe ameapishwa kiapo cha uaminifu na kiapo kingine chochote kinachohusika na utendaji wa kazi kitakachowekwa kwa mujibu wa sheria iliyotungwa na Bunge.

Akidi ya vikao vya Mahakama ya Rufani
Sheria Na. 14 ya 1979 ib. 8; 15 ya 1984 ib. 32; 7 ya 1994 Fungu la 8(1)(k)

**122.**–(1) Akidi ya kila kikao cha Mahakama ya Rufani ni Majaji wa Mahakama ya Rufani wasiopungua watatu.

(2) Katika kila rufaa suala linalohitaji uamuzi wa Mahakama ya Rufani itaamuliwa kwa kufuata kauli ya walio wengi kati ya Majaji wa Mahakama ya Rufani waliosikiliza rufaa.

Mashauri yanayoweza kuamuliwa na Jaji mmoja wa Mahakama ya Rufani
Sheria Na. 14 ya 1979 ib. 8; 15 ya 1984 ib. 33

**123.** Jaji mmoja wa Mahakama ya Rufani aweza kutekeleza madaraka yoyote ya Mahakama ya Rufani ambayo hayahusiki na kutoa uamuzi juu ya Rufaa-

Isipokuwa kwamba:

(a) katika mashauri ya jinai, iwapo Jaji wa Mahakama ya Rufani aliyeombwa kutekeleza madaraka hayo atatoa uamuzi ambao mwombaji haridhiki nao, basi mwombaji atakuwa na haki kutaka maombi yake yaamuliwe na Mahakama ya Rufani;

(b) katika mashauri ya madai, Mahakama ya rufani yaweza kubatilisha au kubadilisha amri, agizo au uamuzi wa namna nyingine wowote uliotolewa na Jaji mmoja wa Mahakama ya Rufani kwa mujibu wa masharti ya ibara hii.

©2025 Government of Tanzania. All rights reserved. No part of this book may be reproduced or distributed without permission of OAG.

## SEHEMU YA SITA

## UTARATIBU WA KUPELEKA HATI NA KUTEKELEZA MAAGIZO YALIYOMO KATIKA HATI ZILIZOTOLEWA NA MAHAKAMA

Utekelezaji wa maagizo ya Mahakama utafanywa nchini Tanzania kote
Sheria Na. 15 ya 1984 ib. 34; 3 ya 2000 ib. 17

**124.**–(1) Hati zenye maagizo yaliyotolewa na Mahakama za Tanzania Bara na Mahakama za Tanzania Zanzibar katika mashauri ya madai ya aina zote na mashauri ya jinai ya aina zote (pamoja na hati za kuamuru kukamata watu) zaweza kupelekwa mahali popote nchini Tanzania na maagizo hayo yaweza kutekelezwa mahali popote nchini Tanzania kwa kufuata masharti yafuatayo:

(a) iwapo Mahakama imetoa hati zenye maagizo yatakayotekelezwa mahali ambako mahakama hiyo haina mamlaka, basi hati hiyo itapelekwa huko na maagizo yaliyomo katika hati hiyo yatatekelezwa kwa mujibu wa utaratibu unaotumika huko kwa ajili ya kupeleka hati au kutekeleza maagizo yaliyomo katika hati iliyotolewa na Mahakama yenye mamlaka huko ilikopelekwa hati; na

(b) iwapo sheria inayotumika huko ilikopelekwa hati imeweka masharti kwamba hati zilizotolewa na Mahakama ya mahali pengine ni lazima ithibitishwe kwanza na Mahakama yenye mamlaka mahali hapo inapotumika sheria hiyo, basi kila hati iliyotolewa na Mahakama ya mahali pengine itabidi ithibitishwe kwanza kwa mujibu wa sheria hiyo kabla maagizo yaliyomo katika hati hiyo hayajatekelezwa.

(2) Iwapo mtu amekamatwa mahali popote nchini Tanzania kwa mujibu wa hati ya kuamuru kukamatwa kwake iliyotolewa na Mahakama ambayo haina mamlaka mahali hapo alipokamatwa mtu huyo, basi mtu huyo atahesabiwa kuwa yuko chini ya ulinzi halali na aweza kufikishwa mbele ya

©2025 Government of Tanzania. All rights reserved. No part of this book may be reproduced or distributed without permission of OAG.

Mahakama iliyotoa hati hiyo, lakini masharti haya yaliyomo katika ibara hii ndogo itabidi yatumiwe bila kuathiri masharti ya sheria inayotumika hapo mahali alipokamatwa mtu huyo.

(3) Masharti yaliyomo katika ibara hii hayatazuia sheria kuweka utaratibu kwa ajili ya kupeleka nje ya Tanzania hati zilizotolewa na Mahakama za Tanzania Bara au Mahakama za Tanzania Zanzibar.

## SEHEMU YA SABA

## MAHAKAMA MAALUM YA KATIBA YA JAMHURI YA MUUNGANO

Mahakama Maalum ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano
Sheria Na. 15 ya 1984 ib. 35; 3 ya 2000 ib. 17

**125.** Kutakuwa na Mahakama Maalum ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano ambayo Mamlaka yake, muundo wake na utaratibu wa shughuli zake ni kama ilivyoelezwa katika ibara ya 126, 127 na 128 ya Katiba hii.

Mamlaka ya Mahakama Maalum ya Katiba
Sheria Na. 14 ya 1979 ib. 9; 15 ya 1984 ib. 36

**126.**–(1) Kazi pekee ya Mahakama Maalum ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano ni kusikiliza shauri lililotolewa mbele yake, kutoa uamuzi wa usuluhishi, juu ya suala lolote linalohusika na tafsiri ya Katiba hii iwapo tafsiri hiyo au utekelezaji wake unabishaniwa kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

(2) Katika kutekeleza kazi yake kwa mujibu wa masharti ya ibara hii, Mahakama Maalum ya Katiba haitakuwa na mamlaka ya kuchunguza au kubadilisha uamuzi wa Mahakama Kuu au uamuzi wa Mahakama ya Rufani uliotolewa kwa mujibu wa masharti ya ibara ya 83 ya Katiba hii au uamuzi wa Mahakama ya Rufani uliotolewa kwa mujibu wa ibara ya 117 ya Katiba hii.

(3) Kila uamuzi wa usuluhishi utakaotolewa na Mahakama Maalum ya Katiba kwa mujibu wa ibara hii utakuwa ndio wa mwisho; hakutakuwa na haki ya kukata rufaa popote.

©2025 Government of Tanzania. All rights reserved. No part of this book may be reproduced or distributed without permission of OAG.

Muundo wa Mahakama Maalum ya Katiba
Sheria Na. 14 ya 1979 ib. 10; 15 ya 1984 ib. 37

**127.**–(1) Mahakama Maalum ya Katiba itakuwa na wajumbe ambao nusu ya jumla ya wajumbe wote watateuliwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano na nusu nyingine ya jumla hiyo watateuliwa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

(2) Mtu anayeweza kuteuliwa kuwa Mjumbe wa Mahakama Maalum ya Katiba ni yule tu ambaye ni Jaji au aliyepata kuwa Jaji wa Mahakama ya Rufani, Jaji wa Mahakama Kuu ya Jamhuri ya Muungano au wa Mahakama Kuu ya Zanzibar, au mtu mwenye uwezo na ujuzi wa kazi ya Jaji na anayestahili kuteuliwa kuwa Jaji au Kaimu Jaji kwa mujibu wa sheria inayotumika Tanzania Bara na sheria inayotumika Tanzania Zanzibar, kadri hali itakavyokuwa.

(3) Mtu aweza kuteuliwa kuwa mjumbe wa Mahakama Maalum ya Katiba ama kwa ajili ya kusikiliza shauri moja tu au mashauri mawili au zaidi kama yatatokea. Mjumbe ataendelea kutekeleza madaraka ya kazi yake kama Mjumbe wa Mahakama Maalum ya Katiba mpaka shauri analohusika nalo litakapokwisha au mpaka uteuzi wake utakapofutwa au mpaka atakaposhindwa kutekeleza kazi yake kama Mjumbe kwa sababu ya maradhi au sababu nyingine yoyote.

Utaratibu katika vikao vya Mahakama Maalum ya Katiba
Sheria Na. 15 ya 1984 ib. 37; 7 ya 1994 Fungu la 8(1)(k)

**128.**–(1) Mahakama Maalum ya Katiba itafanya vikao vyake wakati ule tu kunapokuwa na shauri la kusikiliza, na itafanya vikao vyake mahali popote patakapoamuliwa kwa utaratibu utakaotumika kwa ajili ya mashauri yatakayosikilizwa na Mahakama Maalum ya Katiba.

(2) Akidi ya kila kikao cha Mahakama Maalum ya Katiba ni wajumbe wote, na iwapo mjumbe yeyote atakuwa hayupo au ikiwa kiti cha mjumbe yeyote kitakuwa wazi basi Serikali iliyomteua mjumbe huyo ambaye hayupo au ambaye kiti chake ki-wazi itamteua mjumbe mwingine wa kushika mahali pake. Mjumbe wa muda aliyeteuliwa kwa mujibu wa ibara hii ndogo ataendelea kutekeleza kazi katika Mahakama Maalum ya Katiba mpaka mjumbe wa kawaida atakaporejea kazini au mpaka mtu atakapoteuliwa kujaza nafasi iliyo wazi au mpaka shauri litakapokwisha, kutegemea ni lipi kati ya mambo hayo litakalotokea mapema zaidi.

©2025 Government of Tanzania. All rights reserved. No part of this book may be reproduced or distributed without permission of OAG.

(3) Kila suala linalohitaji uamuzi wa Mahakama Maalum ya Katiba litaamuliwa kwa kufuata kauli ya theluthi mbili ya wajumbe kutoka Tanzania Bara na theluthi mbili ya wajumbe kutoka Tanzania Zanzibar.

(4) Bunge laweza kutunga sheria kwa ajili ya kuweka masharti kuhusu utaratibu wa uchaguzi wa Mwenyekiti wa Mahakama Maalum ya Katiba, utaratibu wa kupeleka shauri mbele ya Mahakama hiyo, utaratibu wa kuendesha shauri katika Mahakama na utaratibu wa kuwasilisha Serikalini uamuzi wa Mahakama Maalum ya Katiba:

Isipokuwa kwamba iwapo shauri lolote litafikishwa mbele ya Mahakama Maalum ya Katiba wakati hakuna sheria yoyote ya aina iliyoelezwa katika ibara hii ndogo, basi shauri litasikilizwa na kuamuliwa kwa kufuata utaratibu utakaowekwa na Mahakama yenyewe kabla ya kuanza kusikiliza shauri, au iwapo Wajumbe wa Mahakama watashindwa kukubaliana juu ya utaratibu huo, basi shauri litasikilizwa na kuamuliwa kwa kufuata utaratibu utakaoamuliwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano kwa kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

## SURA YA SITA
## TUME YA HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA BORA NA SEKRETARIETI YAVIONGOZI WA UMMA

### SEHEMU YA KWANZA
### TUME YA HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA BORA

Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora Sheria Na. 3 ya 2000 ib. 18

**129.**–(1) Kutakuwa na Tume itakayoitwa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, ambayo majukumu yake yatakuwa kama ilivyoelezwa katika ibara ya 130 ya Katiba hii.

(2) Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora itakuwa na Makamishna wafuatao:

(a) Mwenyekiti, ambaye atakuwa ni mtu mwenye sifa ya kuweza kuteuliwa kuwa Jaji;



©2025 Government of Tanzania. All rights reserved. No part of this book may be reproduced or distributed without permission of OAG.

(b) Makamu Mwenyekiti, ambaye atateuliwa kwa kuzingatia kanuni kwamba endapo Mwenyekiti ni mtu anayetoka upande mmoja wa Jamhuri ya Muungano, yeye atakuwa ni mtu wa kutoka upande mwingine wa Jamhuri ya Muungano;

(c) Makamishna wengine wasiozidi watano watakaoteuliwa kutoka miongoni mwa watu wenye ujuzi, uzoefu na upeo mkubwa katika mambo ya haki za binadamu, sheria, utawala, siasa au mambo ya jamii; na

(d) Makamishna Wasaidizi.

(3) Makamishna na Makamishna Wasaidizi wote watateuliwa na Rais baada ya kushauriana na Kamati ya Uteuzi.

(4) Kutakuwa na Kamati ya Uteuzi kwa madhumuni ya ibara hii ambayo itakuwa na wajumbe wafuatao:

(a) Jaji Mkuu wa Mahakama ya Rufani;

(b) Spika wa Bunge;

(c) Jaji Mkuu wa Zanzibar;

(d) Spika wa Baraza la Wawakilishi; na

(e) Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, ambaye atakuwa ndiye Katibu wa Kamati hii.

(5) Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Makamishna wengine wote kila mmoja atashika madaraka yake kwa kipindi cha miaka mitatu na anaweza kuteuliwa tena kwa kipindi kingine kimoja tu cha miaka mitatu.

(6) Kwa madhumuni ya kuwakinga Makamishna kutokana na migongano ya kimasilahi, mtu yeyote akiteuliwa kuwa Kamishna wa Tume atalazimika kuacha mara moja madaraka yoyote katika chama chochote cha siasa au madaraka ya aina nyingine yoyote yatakayotajwa kwa ajili hiyo na sheria iliyotungwa na Bunge.

(7) Kamishna au Kamishna Msaidizi wa Tume aweza tu kuondolewa katika madaraka ya kazi yake katika Tume kwa sababu ya kushindwa kutekeleza kazi yake, ama kutokana na maradhi au sababu nyingine yoyote, au kwa sababu ya tabia mbaya inayoathiri maadili ya kazi ya Kamishna.

©2025 Government of Tanzania. All rights reserved. No part of this book may be reproduced or distributed without permission of OAG.

(8) Tume yaweza kutekeleza shughuli zake bila ya kujali kwamba kuna nafasi iliyo wazi miongoni mwa viti vya wajumbe au kwamba mjumbe mmojawapo hayupo.

Majukumu ya Tume na taratibu za utekelezaji
Sheria Na. 3 ya 2000 ib. 17
TS. Na. 133 la 2001

**130.**–(1) Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora itatekeleza majukumu yafuatayo:

(a) kuhamasisha nchini hifadhi ya haki za binadamu na wajibu kwa jamii kwa mujibu wa Katiba na Sheria za nchi;

(b) kufanya shughuli za kupokea malalamiko ya uvunjaji wa haki za binadamu kwa ujumla;

(c) kufanya uchunguzi juu ya mambo yanayohusu uvunjaji wa haki za binadamu na ukiukwaji wa misingi ya utawala bora;

(d) kufanya utafiti, kutoa na kueneza nchini elimu kwa umma kuhusu haki za binadamu na utawala bora;

(e) kama ikibidi, kufungua mashauri mahakamani ili kuzuia vitendo vya uvunjaji wa haki za binadamu au kurekebisha haki inayotokana na uvunjwaji huo wa haki za binadamu, au ukiukwaji wa misingi ya utawala bora;

(f) kuchunguza mwenendo wa mtu yeyote anayehusika au taasisi yoyote inayohusika na masharti ya ibara hii katika utekelezaji wa kawaida wa madaraka ya kazi au majukumu yake au utekelezaji unaokiuka madaraka hayo;

(g) kutoa ushauri kwa Serikali na vyombo vingine vya umma na vya sekta ya binafsi kuhusu haki za binadamu na utawala bora; na

(h) kuchukua hatua zipasazo kwa ajili ya kukuza na kuendeleza usuluhishi na suluhu miongoni mwa watu na taasisi mbalimbali wanaofika au kufikishwa mbele ya Tume.

(2) Tume itakuwa ni idara inayojitegemea, na bila ya kuathiri masharti mengineyo ya ibara hii, katika kutekeleza madaraka yake kwa mujibu wa Katiba hii, Tume haitalazimika kufuata maagizo au amri ya mtu yeyote au idara yoyote ya Serikali au maoni ya chama chochote cha siasa au ya taasisi nyingine yoyote ya umma au ya sekta ya binafsi.

©2025 Government of Tanzania. All rights reserved. No part of this book may be reproduced or distributed without permission of OAG.

(3) Masharti ya ibara ndogo ya (2) yasihesabiwe kuwa yanamzuia Rais kutoa maagizo au amri kwa Tume, wala hayatoi haki kwa Tume kutofuata maagizo au amri, endapo Rais ataona kuwa, kuhusiana na jambo lolote au hali yoyote, masilahi ya taifa yahitaji hivyo.

(4) Tume itafanya uchunguzi kwa kufuata masharti ya ibara hii na masharti ya sheria iliyotungwa na Bunge kwa ajili hiyo, na itafanya uchunguzi juu ya mtu yeyote anayehusika au taasisi yoyote inayohusika kila itakapoagizwa na Rais kufanya uchunguzi, vilevile, isipokuwa kama Rais ameagiza Tume isifanye uchunguzi, Tume yaweza kufanya uchunguzi wakati wowote inapoona inafaa kuchunguza mwenendo wa mtu yeyote anayehusika, au taasisi yoyote inayohusika, na masharti ya ibara hii anayetuhumiwa au inayotuhumiwa kwa kukiuka madaraka ya kazi yake, kutumia vibaya madaraka ya kazi yake au majukumu ya taasisi hiyo au kwa uvunjaji wa haki za binadamu au misingi ya utawala bora.

(5) Tume haitakuwa na mamlaka yoyote, ama kwa mujibu wa masharti ya ibara hii au masharti ya sheria yoyote iliyotungwa na Bunge kwa madhumuni ya Sura hii ya Katiba hii ya kuchunguza uamuzi wa Jaji yeyote, Hakimu yeyote au wa Mahakama iwapo uamuzi huo ameutoa katika kutekeleza madaraka ya kazi yake; vilevile Tume haitakuwa na mamlaka ya kuchunguza uamuzi wowote uliotolewa na chombo chochote chenye asili ya Mahakama kilichoanzishwa kwa mujibu wa sheria iwapo uamuzi huo umetolewa katika kutekeleza mamlaka yake.

(6) Masharti ya ibara hii yatatumika kwa watumishi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano na wale wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, watumishi na viongozi wa vyama vya siasa wanaoshughulikia mambo ya umma, wajumbe na watumishi wa Tume zote za Serikali ya Jamhuri ya Muungano na za Serikali hizo, mashirika ya umma na vyombo vingine vya binafsi, kama ni kampuni, jumuiya, ushirika, wadhamini au

©2025 Government of Tanzania. All rights reserved. No part of this book may be reproduced or distributed without permission of OAG.

muundo mwingine wowote, kadri itakavyoelezwa katika sheria iliyotungwa na Bunge; lakini masharti haya hayatatumika kwa Rais wala kwa Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar isipokuwa tu kwa kuzingatia masharti ya ibara ya 46 ya Katiba hii au ibara ya 36 ya Katiba ya Zanzibar ya 1984.

Mamlaka ya Tume na Utaratibu wa shughuli zake
Sheria Na. 3 ya 2000 ib. 18

**131.**–(1) Bila ya kuathiri masharti mengineyo ya ibara hii, Bunge laweza kutunga sheria kwa mujibu wa masharti ya Sura hii ya Katiba hii kwa ajili ya kuweka masharti kuhusu mamlaka ya Tume, utaratibu wa kuendesha shughuli zake na kuhusu kinga za kisheria watakazokuwa nazo Makamishna na watumishi wa Tume kwa makusudi ya kuwawezesha kutekeleza kazi zao bila ya matatizo ya kisheria.

(2) Tume haitachunguza mambo yafuatayo, kwa madhumuni ya kutekeleza majukumu yake, yaani-

(a) jambo lolote ambalo liko mbele ya Mahakama au chombo kinginecho cha kimahakama;
(b) jambo lolote linalohusu uhusiano au mashirikiano kati ya Serikali na Serikali ya nchi yoyote ya nje au shirika la kimataifa;
(c) jambo linalohusu madaraka ya Rais kutoa msamaha; au
(d) jambo jingine lolote lililotajwa na sheria yoyote.

(3) Kila mwaka wa fedha Tume itatayarisha na kuwasilisha kwa Waziri anayesimamia haki za binadamu taarifa kuhusu-

(a) shughuli za Tume katika mwaka uliotangulia;
(b) hali ya utekelezaji wa hifadhi ya haki za binadamu katika Jamhuri ya Muungano, na Waziri atawasilisha mbele ya Bunge kila taarifa iliyowasilishwa kwake na Tume mapema iwezekanavyo baada ya kuipokea.

(4) Masharti ya ibara ndogo ya (3) hayatahesabiwa kuwa yanaizuia Tume kuwasilisha taarifa nyingine yoyote kwa mtu mwingine au mamlaka nyingine yoyote.

©2025 Government of Tanzania. All rights reserved. No part of this book may be reproduced or distributed without permission of OAG.

## SEHEMU YA PILI
## SEKRETARIETI YA MAADILI YA VIONGOZI WA UMMA

Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma
Sheria Na. 3 ya 2000 ib. 18; 15 ya 1984 ib. 39; 4 ya 1992 ib. 35; 12 ya 1995 ib. 18

**132.**–(1) Kutakuwa na Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma ambayo itakuwa na mamlaka ya kuchunguza tabia na mwenendo wa kiongozi wa umma yeyote kwa madhumuni ya kuhakikisha kwamba masharti ya sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma yanazingatiwa ipasavyo.

(2) Kwa madhumuni ya ibara hii, maana ya kiongozi wa umma na masharti ya maadili ya viongozi wa umma itabidi ifahamike kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma au masharti ya sheria nyingine yoyote iliyotungwa na Bunge kwa kadri masharti hayo yanavyohusika na suala la uongozi na ufafanuzi wake.

(3) Sekretarieti ya Maadili itakuwa na Kamishna wa Maadili na wafanyakazi wengine ambao idadi yao itatajwa na sheria iliyotungwa na Bunge.

(4) Bunge litatunga Sheria itakayoainisha misingi ya Maadili ya Viongozi wa Umma itakayozingatiwa na watu wote wanaoshika nafasi za madaraka zitakazotajwa na sheria iliyotungwa na Bunge.

(5) Misingi ya Maadili ya Viongozi wa Umma-

(a) itafafanua nafasi za madaraka ambazo watu wenye kushika nafasi hizo watahusika nayo;

(b) itawataka watu wanaoshika nafasi fulani za madaraka kutoa mara kwa mara maelezo rasmi kuhusu mapato, rasilimali na madeni yao;

(c) itapiga marufuku mienendo na tabia inayopelekea kiongozi kuonekana hana uaminifu, anapendelea au si muadilifu au inaelekea kukuza au kuchochea rushwa katika shughuli za umma au inahatarisha maslahi au ustawi wa jamii;

(d) itafafanua adhabu zinazoweza kutolewa kwa kuvunja misingi ya maadili;

(e) itaelekeza taratibu, madaraka na desturi zitakazofuatwa ili kuhakikisha utekelezaji wa maadili;

©2025 Government of Tanzania. All rights reserved. No part of this book may be reproduced or distributed without permission of OAG.

(f) itaweka masharti mengine yoyote yanayofaa na ambayo ni muhimu kwa madhumuni ya kukuza na kudumisha uaminifu, uwazi, kutopendelea na uadilifu katika shughuli za umma na kwa ajili ya kulinda fedha na mali nyinginezo za umma.

(6) Bunge laweza kwa sheria kuweka masharti ya mtu kufukuzwa au kuondolewa kazini kutokana na kuvunja maadili ya viongozi, bila ya kujali kama kazi hiyo ni ya kuchaguliwa au kuteuliwa.

## SURA YA SABA
## MASHARTI KUHUSU FEDHA ZA JAMHURI YA MUUNGANO

### SEHEMU YA KWANZA
### MCHANGO NA MGAWANYO WA MAPATO YA JAMHURI YA MUUNGANO

Akaunti ya Fedha ya pamoja Sheria Na. 15 ya 1984 ib. 42 TS. Na. 133 la 2001

**133.** Serikali ya Jamhuri ya Muungano itatunza akaunti maalum itakayoitwa "Akaunti ya Fedha ya Pamoja" na ambayo itakuwa ni sehemu ya Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano, ambamo kutawekwa fedha yote itakayochangwa na Serikali mbili kwa kiasi kitakachoamuliwa na Tume ya pamoja ya Fedha kwa mujibu wa sheria iliyotungwa na Bunge, kwa madhumuni ya shughuli za Jamhuri ya Muungano kwa Mambo ya Muungano.

Tume ya Pamoja ya Fedha Sheria Na. 15 ya 1984 ib. 42

**134.**–(1) Kutakuwa na Tume ya Pamoja ya Fedha yenye wajumbe wasiozidi saba ambao watateuliwa na Rais kwa mujibu wa ibara hii na masharti ya sheria iliyotungwa na Bunge.

(2) Majukumu ya Tume yatakuwa ni-

(a) kuchambua mapato na matumizi yanayotokana na, au yanayohusu utekelezaji wa Mambo ya Muungano na kutoa mapendekezo kwa Serikali mbili kuhusu mchango na mgawo wa kila mojawapo ya Serikali hizo;

©2025 Government of Tanzania. All rights reserved. No part of this book may be reproduced or distributed without permission of OAG.

(b) kuchunguza kwa wakati wote mfumo wa shughuli za fedha wa Jamhuri ya Muungano na pia uhusiano katika mambo ya kifedha kati ya Serikali mbili; na

(c) kutekeleza majukumu mengine ambayo Rais ataipatia Tume au kama Rais atakavyoagiza, na kwa mujibu wa sheria iliyotungwa na Bunge.

## SEHEMU YA PILI

## MFUKO MKUU WA HAZINA NA FEDHA ZA JAMHURI YA MUUNGANO

Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano Sheria Na. 15 ya 1984 ib. 43

**135.**–(1) Fedha zote zitakazopatikana kwa njia mbalimbali kwa ajili ya matumizi ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano, isipokuwa fedha za aina iliyotajwa katika ibara ndogo ya (2) ya ibara hii, zitawekwa katika mfuko mmoja maalum ambao utaitwa Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali.

(2) Fedha ambazo hazitawekwa kwenye Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ni zile zote ambazo zimetajwa na sheria kwamba zitumike kwa shughuli maalum au ziwekwe katika mfuko mwingine kwa ajili ya matumizi maalum.

Masharti ya kutoa fedha za matumizi kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali Sheria Na. 15 ya 1984 ib. 43

**136.**–(1) Fedha hazitatolewa kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali kwa ajili ya matumizi ila kwa mujibu wa masharti yafuatayo:

(a) fedha hizo ziwe kwa ajili ya matumizi ambayo yameidhinishwa yatokane na fedha zilizomo katika Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali na idhini hiyo iwe imetolewa na Katiba hii au sheria nyingine yoyote;

(b) fedha hizo ziwe kwa ajili ya matumizi ambayo yameidhinishwa ama na Sheria ya Matumizi ya Serikali iliyotungwa mahususi na Bunge au sheria iliyotungwa kwa mujibu wa masharti ya ibara ya 140 ya Katiba hii.

(2) Fedha zilizomo katika mfuko maalum wowote wa Serikali, ukiachilia mbali Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali, hazitatolewa kutoka mfuko huo kwa ajili ya matumizi ila mpaka matumizi hayo yawe yameidhinishwa na sheria.

©2025 Government of Tanzania. All rights reserved. No part of this book may be reproduced or distributed without permission of OAG.

(3) Fedha zilizomo katika Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali hazitatolewa kutoka Mfuko huo kwa ajili ya matumizi ila mpaka matumizi hayo yawe yameidhinishwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na pia kwa sharti kwamba fedha hizo ziwe zimetolewa kwa kufuata utaratibu uliowekwa kwa ajili hiyo kwa mujibu wa sheria iliyotungwa na Bunge.

Utaratibu wa kuidhinisha matumizi ya fedha zilizomo katika Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali
Sheria Na. 15 ya 1984 ib. 43

**137.**–(1) Rais atatoa maagizo kwa watu wanaohusika kwamba watengeneze na kuwasilisha kwenye Bunge katika kila mwaka wa fedha wa Serikali, makadirio ya mapato na matumizi ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano kwa ajili ya kipindi cha mwaka wa fedha unaofuata.

(2) Baada ya Bunge kuyakubali makadirio ya matumizi (mbali na matumizi ambayo yameidhinishwa ama na Katiba hii au sheria nyingine yoyote kuwa yatokane na fedha zilizomo katika Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali) kutawasilishwa kwenye Bunge Muswada ambao utaitwa Muswada wa Sheria ya Matumizi ya Fedha za Serikali, kwa ajili ya kuidhinisha matumizi ya fedha kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali, na fedha hizo zitakazotolewa kulipa gharama za shughuli mbalimbali za Serikali zinazohusika na makadirio hayo.

(3) Ikiwa katika mwaka wa fedha wowote inaonekana kwamba-

(a) fedha za matumizi zilizoidhinishwa na Sheria ya Matumizi ya Fedha za Serikali kwa ajili ya shughuli fulani hazitoshi au kwamba imekuwa lazima kulipa gharama za shughuli ambayo haikupangiwa fedha za matumizi kwa mujibu wa sheria; au

(b) kuna fedha ambazo zimetumiwa kwa ajili ya shughuli fulani kwa kiasi kinachozidi kiwango cha matumizi yaliyoidhinishwa na Sheria ya Matumizi ya Fedha za Serikali kuhusu shughuli hiyo au kwamba fedha zimetumiwa kulipia gharama za shughuli ambayo haikupangiwa fedha za matumizi kwa mujibu wa sheria, kutawasilishwa kwenye Bunge makadirio ya

©2025 Government of Tanzania. All rights reserved. No part of this book may be reproduced or distributed without permission of OAG.

matumizi ya nyongeza au, kadri itakavyokuwa, maelezo ya matumizi ya ziada, na baada ya Bunge kuyakubali hayo makadirio ya matumizi ya nyongeza au maelezo ya matumizi ya ziada, kutawasilishwa kwenye Bunge Muswada wa Sheria ya Matumizi ya Fedha za Serikali kwa ajili ya kuidhinisha matumizi ya fedha kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali, na fedha hizo zitatumiwa kulipia gharama za shughuli zinazohusika na hayo makadirio au maelezo.

Masharti ya kutoza kodi
Sheria Na. 15 ya 1984 ib. 43

**138.**–(1) Hakuna kodi ya aina yoyote itakayotozwa isipokuwa kwa mujibu wa sheria iliyotungwa na Bunge au kwa mujibu wa utaratibu uliowekwa kisheria na uliotiliwa nguvu kisheria na sheria iliyotungwa na Bunge.

(2) Masharti yaliyomo katika ibara ndogo ya (1) ya ibara hii hayatalizuia Baraza la Mapinduzi la Zanzibar kutumia mamlaka yake ya kutoza kodi ya aina yoyote kwa mujibu wa madaraka ya Baraza hilo.

Utaratibu wa kuidhinisha matumizi ya fedha kabla ya Sheria za Matumizi kuanza kutumika
Sheria Na. 15 ya 1984 ib. 43

**139.**–(1) Bunge laweza kutunga sheria kwa ajili ya kuweka masharti ya kuidhinisha matumizi ya fedha kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali kwa kufuata utaratibu ulioelezwa katika ibara ndogo ya (2) ya ibara hii.

(2) Iwapo mwaka wa fedha wa Serikali umeanza na Sheria ya Matumizi ya Fedha za Serikali inayohusika na mwaka huo haijaanza kutumika basi Rais aweza kuidhinisha fedha itolewe kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali kwa ajili ya kulipia gharama za lazima za shughuli za Serikali, na fedha hizo zitatumiwa mpaka ipite miezi minne tangu mwanzo wa mwaka wa fedha mpaka Sheria ya Matumizi ya Fedha za Serikali itakapoanza kutumika, kutegemea ni lipi kati ya mambo hayo litakalotokea mapema zaidi.

Mfuko wa Matumizi ya Dharura
Sheria Na. 15 ya 1984 ib. 43

**140.**–(1) Bunge laweza kutunga sheria kwa ajili ya kuweka masharti kuhusu mambo yafuatayo:

(a) kuanzisha Mfuko wa Matumizi ya Dharura na kumwezesha Rais au Waziri aliyeteuliwa na Rais kwa

©2025 Government of Tanzania. All rights reserved. No part of this book may be reproduced or distributed without permission of OAG.

ajili hiyo kuazima fedha kutoka mfuko huo kulipia gharama za jambo la haraka na la dharura ambalo halikutazamiwa kutokea na ambalo halikupangiwa fedha zozote za matumizi; na

(b) kumwezesha Rais au Waziri aliyeteuliwa na Rais kwa ajili hiyo kutumia fedha zilizotengwa mahsusi kwa ajili ya shughuli fulani kulipia gharama za jambo la haraka na la dharura kama ilivyoelezwa katika aya ya (a) ya ibara hii ndogo.

(2) Iwapo fedha zimeazimwa kutoka Mfuko wa Matumizi ya Dharura au fedha zilitengwa mahsusi kwa ajili ya shughuli fulani zimetumiwa kulipia gharama za jambo la haraka na la dharura, basi kutawasilishwa kwenye Bunge makadirio ya matumizi ya nyongeza, na baada ya Bunge kuyakubali makadirio hayo Muswada wa Sheria ya Matumizi ya Fedha za Serikali utakaowasilishwa kwenye Bunge kwa ajili ya kuidhinisha matumizi hayo ya nyongeza utahakikisha kwamba fedha zozote zilizoazimwa kutoka Mfuko wa Matumizi ya Dharura zitarudishwa kwenye Mfuko huo kutokana na fedha za matumizi yatakayoidhinishwa na Muswada huo.

Deni la Taifa
Sheria Na.
15 ya 1984 ib. 4

**141.**–(1) Deni la Taifa litadhaminiwa na Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano.

(2) Kwa madhumuni ya ufafanuzi wa ibara hii deni la Taifa maana yake ni deni lenyewe na pia faida inayolipwa juu ya deni hilo, fedha zinazowekwa akiba kwa ajili ya kulipa deni pole pole na gharama zote zinazoambatana na usimamizi wa deni hilo.

Mishahara ya watumishi fulani wa Serikali kudhaminiwa na Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali
Sheria Na.
15 ya 1984 ib. 43

**142.**–(1) Watumishi wa Serikali wanaohusika na masharti ya ibara hii watalipwa mishahara na posho kama itakavyoelezwa na sheria iliyotungwa na Bunge.

(2) Fedha za malipo ya mishahara na posho za watumishi wa Serikali wanaohusika na masharti ya ibara hii pamoja na fedha za malipo ya uzeeni na kiinua mgongo kwa wale wanaostahili malipo hayo miongoni mwa watumishi hao zitatolewa kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali.

©2025 Government of Tanzania. All rights reserved. No part of this book may be reproduced or distributed without permission of OAG.

(3) Mshahara anaolipwa mtumishi wa Serikali anayehusika na masharti ya ibara hii pamoja na masharti yake ya kazi havitabadilishwa, baada ya mtumishi huyo kuteuliwa, kwa jinsi ambayo itapunguza maslahi ya mtumishi huyo, lakini maelezo haya hayahusiki na posho anayolipwa mtumishi huyo.

Sheria Na. 7 ya 1994 Fungu la 8(1)(k) TS. Na. 150 la 2005

(4) Iwapo mtumishi wa Serikali anayehusika na masharti ya ibara hii ana hiari ya kuchagua kima cha mshahara au aina ya masharti ya kazi, basi kwa madhumuni ya ufafanuzi wa masharti ya ibara ndogo ya (3) ya ibara hii, mshahara wa kima hicho atakachochagua na aina hiyo ya masharti ya kazi atakayochagua vitahesabiwa kuwa vina masilahi zaidi kwake kuliko kima cha mshahara kingine chochote ambacho anaweza kuchagua au aina ya masharti ya kazi nyingine yoyote ambayo angeweza kuchagua.

(5) Masharti ya ibara hii yatatumika kwa Jaji wa Mahakama ya Rufani, Jaji wa Mahakama Kuu ya Jamhuri ya Muungano, Mwenyekiti na kila Mjumbe wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya Jamhuri ya Muungano.

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali wa Jamhuri ya Muungano Sheria Na. 14 ya 1979 ib. 11; 15 ya 1984 ib. 43

**143.**–(1) Kutakuwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya Jamhuri ya Muungano.

(2) Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali atakuwa na jukumu juu ya mambo yafuatayo:

(a) kuhakikisha kwamba fedha zozote zinazokusudiwa kutolewa kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali matumizi yake yameidhinishwa na kwamba zitatolewa kwa mujibu wa masharti ya ibara ya 136 ya Katiba hii, na iwapo atatosheka kwamba masharti hayo yatatekelezwa ipasavyo, basi ataidhinisha fedha hizo zitolewe;

(b) kuhakikisha kwamba fedha zote ambazo matumizi yake yameidhinishwa yatokane na fedha zilizomo katika Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali au fedha ambazo matumizi yake yameidhinishwa na sheria iliyotungwa na Bunge, na ambazo zimetumika, zimetumiwa kwa ajili ya shughuli zilizohusika na matumizi ya fedha hizo



©2025 Government of Tanzania. All rights reserved. No part of this book may be reproduced or distributed without permission of OAG.

na kwamba matumizi hayo yamefanywa kwa kufuata idhini iliyotolewa kuhusu matumizi hayo; na

(c) angalau mara moja kila mwaka kufanya ukaguzi na kutoa taarifa juu ya ukaguzi wa hesabu za Serikali ya Jamhuri ya Muungano, hesabu zinazosimamiwa na watumishi wote wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano na hesabu za Mahakama zote za Jamhuri ya Muungano na zinazosimamiwa na Katibu wa Bunge.

(3) Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu na kila mtumishi wa Serikali aliyeruhusiwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu atakuwa na haki ya kuchunguza vitabu, kumbukumbu, hati za maelezo, taarifa na hati nyinginezo zote zinazohusika na hesabu za aina yoyote iliyotajwa katika ibara ndogo ya (2) ya ibara hii.

(4) Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu atawasilisha kwa Rais kila taarifa atakayotoa kwa mujibu wa masharti ya ibara ndogo ya (2) ya ibara hii. Baada ya kupokea taarifa hiyo Rais atawaagiza watu wanaohusika wawasilishe taarifa hiyo kwenye kikao cha kwanza cha Bunge kitakachofanyika baada ya Rais kupokea taarifa hiyo na itabidi iwasilishwe katika kikao hicho kabla ya kupita siku saba tangu siku ile kilipoanza kikao hicho. Iwapo Rais hatachukua hatua za kuwasilisha taarifa hiyo kwenye Bunge, basi Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu atawasilisha taarifa hiyo kwa Spika wa Bunge (au Naibu wa Spika ikiwa kiti cha Spika ki-wazi wakati huo au ikiwa kwa sababu yoyote Spika hawezi kutekeleza shughuli za kazi yake) ambaye atawasilisha taarifa hiyo kwenye Bunge.

(5) Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu atakuwa pia na jukumu la kutekeleza kazi na shughuli nyingine, na atakuwa na madaraka mengine ya namna mbali mbali, kama itakavyoelezwa na sheria, kuhusu hesabu za Serikali ya Jamhuri ya Muungano au hesabu za vyombo vya Umma au hesabu za mashirika.

(6) Katika kutekeleza madaraka yake kwa mujibu wa masharti ya ibara ndogo ya (2), (3) na (4) ya ibara hii, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu hatalazimika kufuata amri au

©2025 Government of Tanzania. All rights reserved. No part of this book may be reproduced or distributed without permission of OAG.

maagizo ya mtu mwingine yeyote au idara yoyote ya Serikali, lakini maelezo hayo ya ibara hii ndogo hayataizuia Mahakama nayo kutumia madaraka yake kwa ajili ya kuchunguza kama Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu ametekeleza madaraka yake kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii au sivyo.

Kumwondoa kazini Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu Sheria Na. 15 ya 1984 ib. 43; 12 ya 1995 ib. 19

**144.**–(1) Bila ya kuathiri masharti mengine yaliyomo katika ibara hii, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali wa Jamhuri ya Muungano atalazimika kuacha kazi yake atakapotimiza umri wa miaka sitini au umri mwingine wowote utakaotajwa na Sheria iliyotungwa na Bunge.

(2) Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali aweza tu kuondolewa katika madaraka ya kazi yake kwa sababu ya kushindwa kutekeleza kazi zake (ama kutokana na maradhi au sababu nyingine yoyote) au kwa sababu ya tabia mbaya, au kwa kuvunja masharti ya Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma, na hataweza kuondolewa kazini ila kwa mujibu wa masharti ya ibara ndogo ya (4) ya ibara hii.

(3) Iwapo Rais anaona kwamba suala la kumwondoa kazini Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mujibu wa masharti ya ibara hii lahitaji kuchunguzwa, basi katika hali hiyo mambo yatakuwa kama ifuatavyo:

(a) Rais atateua Tume Maalum ambayo itakuwa na Mwenyekiti na Wajumbe wengine wasiopungua wawili. Huyo Mwenyekiti na angalau nusu ya wajumbe wengine wa Tume hiyo itabidi wawe watu ambao ni Majaji au watu waliopata kuwa Majaji wa Mahakama Kuu au Mahakama ya Rufani katika nchi yoyote iliyomo kwenye Jumuiya ya Madola; na

(b) Tume hiyo itachunguza shauri lote halafu itatoa taarifa kwa Rais kuhusu maelezo ya shauri lote na itamshauri Rais kama huyo Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali aondolewe kazini kwa mujibu wa masharti ya ibara hii kwa sababu ya kushindwa kufanya kazi kutokana na maradhi au sababu nyingine yoyote au kwa sababu ya tabia mbaya.

©2025 Government of Tanzania. All rights reserved. No part of this book may be reproduced or distributed without permission of OAG.

(4) Ikiwa Tume iliyoteuliwa kwa mujibu wa masharti ya ibara ndogo ya (3) itamshauri Rais kwamba huyo Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali aondolewe kazini kwa sababu ya kushindwa kufanya kazi kutokana na maradhi au sababu nyingine yoyote au kwa sababu ya tabia mbaya, basi Rais atamwondoa kazini.

(5) Ikiwa suala la kumwondoa kazini Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali limepelekwa kwenye Tume kwa ajili ya uchunguzi kwa mujibu wa masharti ya ibara hii, Rais aweza kumsimamisha kazi huyo Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, na Rais aweza wakati wowote kufuta uamuzi huo wa kumsimamisha kazi, na kwa hali yoyote uamuzi huo utabatilika ikiwa Tume itamshauri Rais kwamba huyo Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali asiondolewe kazini.

(6) Mtu ambaye ni Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu au aliyepata kuwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu hawezi kuteuliwa kushika au kushikilia madaraka ya kazi nyingine yoyote katika utumishi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano.

(7) Masharti ya ibara hii hayatatumika kwa mtu yeyote aliyeteuliwa kuwa Kaimu Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

## SURA YA NANE
## MADARAKA YA UMMA

Serikali za Mitaa
Sheria Na. 15 ya 1984 ib. 50

**145.**–(1) Kutakuwa na vyombo vya Serikali za Mitaa katika kila mkoa, wilaya, mji na kijiji, katika Jamhuri ya Muungano, ambavyo vitakuwa vya aina na majina yatakayowekwa na sheria iliyotungwa na Bunge au na Baraza la Wawakilishi.

(2) Bunge au Baraza la Wawakilishi, kadri itakavyokuwa, litatunga sheria itakayofafanua utaratibu wa kuanzisha vyombo vya Serikali za Mitaa, miundo na wajumbe wake, njia za mapato na utaratibu wa utekelezaji wa shughuli za vyombo hivyo.

©2025 Government of Tanzania. All rights reserved. No part of this book may be reproduced or distributed without permission of OAG.

Kazi za Serikali za Mitaa
Sheria Na. 15 ya 1984 ib. 50

**146.**–(1) Madhumuni ya kuwapo Serikali ya Mitaa ni kupeleka madaraka kwa wananchi. Na vyombo vya Serikali za Mitaa vitakuwa na haki na mamlaka ya kushiriki kuwashirikisha wananchi katika mipango na shughuli za utekelezaji wa maendeleo katika sehemu zao na nchini kote kwa jumla.

(2) Bila ya kuathiri maelezo ya jumla yaliyomo katika ibara ndogo ya (1) ya ibara hii, kila chombo cha Serikali za Mitaa, kwa kuzingatia masharti ya sheria iliyokianzisha, kitahusika na shughuli zifuatazo:

(a) kutekeleza kazi za Serikali za Mitaa katika eneo lake;
(b) kuhakikisha utekelezaji wa sheria na ulinzi wa wananchi; na
(c) kuimarisha demokrasia katika eneo lake na kuitumia demokrasia kuharakisha maendeleo ya wananchi.

## SURA YA TISA
## MAJESHI YA ULINZI

Marufuku kuunda majeshi ya ulinzi yasiyo majeshi ya ulinzi ya Umma
Sheria Na. 15 ya 1984 ib. 49; 4 ya 1992 ib. 36; TS. Na. 133 la 2001

**147.**–(1) Ni marufuku kwa mtu yeyote au shirika lolote au kikundi chochote cha watu, isipokuwa Serikali kuunda au kuweka Tanzania jeshi la aina yoyote.

(2) Serikali ya Jamhuri ya Muungano yaweza, kwa mujibu wa sheria, kuunda na kuweka Tanzania majeshi ya aina mbalimbali kwa ajili ya ulinzi na usalama wa nchi na wananchi wa Tanzania.

(3) Itakuwa ni marufuku kwa mwanajeshi yeyote kujiunga na chama chochote cha siasa, isipokuwa tu atakuwa na haki ya kupiga kura iliyotajwa katika ibara ya 5 ya Katiba hii.

(4) Kwa madhumuni ya ibara hii, "mwanajeshi" maana yake ni askari aliyeajiriwa kwa masharti ya muda au ya kudumu katika Jeshi la Ulinzi, Jeshi la Polisi, Jeshi la Magereza au Jeshi la Kujenga Taifa.

©2025 Government of Tanzania. All rights reserved. No part of this book may be reproduced or distributed without permission of OAG.

Madaraka ya Amiri Jeshi Mkuu
Sheria Na. 15 ya 1984 ib. 49

**148.**–(1) Bila ya kuathiri masharti yatakayowekwa na sheria yoyote iliyotungwa na Bunge, miongoni mwa madaraka ya Rais akiwa kama Amiri Jeshi Mkuu ni kuyaamuru majeshi ya nchi yatende mambo yanayohusika na vita vya ulinzi wa Jamhuri ya Muungano, mambo ya kuokoa maisha na mali ya watu katika hali ya hatari na mambo mengineyo ambayo Amiri Jeshi Mkuu ataona yahitajika, na kwa ajili hiyo Amiri Jeshi Mkuu aweza kuyaamuru hayo majeshi yatende mambo hayo ama ndani au nje ya Tanzania.

(2) Bila ya kuathiri masharti yatakayowekwa na sheria iliyotungwa na Bunge, madaraka juu ya mambo yafuatayo yatakuwa mikononi mwa Amiri Jeshi Mkuu, yaani-

(a) madaraka ya kuwateua viongozi katika Majeshi ya Ulinzi ya Jamhuri ya Muungano;

(b) madaraka ya kuwateua watu watakaojiunga na Majeshi ya Ulinzi na madaraka ya kuwaondoa jeshini wanajeshi;

(c) madaraka ya kuwateua wanajeshi watakaoongoza vikosi mbalimbali vya Majeshi ya Ulinzi; na

(d) madaraka ya kumwamuru mwanajeshi yeyote asitumie madaraka yoyote aliyokabidhiwa na ambayo yanaambatana na kuwa kwake mwanajeshi.

(3) Jambo lolote atakalotenda mwanajeshi yeyote kinyume cha amri iliyotolewa na Amiri Jeshi Mkuu kwa mujibu wa masharti ya ibara ndogo ya (1) na (2) ya ibara hii litakuwa batili.

## SURA YA KUMI
## MENGINEYO

Maelezo ya mambo yanayohusika na madaraka ya kazi mbalimbali zilizoanzishwa na Katiba hii
Sheria Na. 1 ya 1980 ib. 16; 15 ya 1984 ib. 52; 4 ya 1992; ib. 37

**149.**–(1) Mtu yeyote mwenye dhamana ya kazi yoyote iliyoanzishwa na Katiba hii (pamoja na kazi ya Waziri, Naibu Waziri au Mbunge, isipokuwa Mbunge ambaye ni Mbunge kwa mujibu wa madaraka ya kazi yake), aweza kujiuzulu kwa kutoa taarifa iliyoandikwa na kutiwa sahihi kwa mkono wake, kwa kufuata masharti yafuatayo:

(a) iwapo mtu huyo aliteuliwa au alichaguliwa na mtu mmoja, basi taarifa hiyo ya kujiuzulu; atawasilisha

©2025 Government of Tanzania. All rights reserved. No part of this book may be reproduced or distributed without permission of OAG.

kwa mtu huyo aliyemteua au kumchagua, au iwapo aliteuliwa au alichaguliwa na kikao cha watu, basi taarifa hiyo ya kujiuzulu ataiwasilisha kwenye kikao hicho;

(b) iwapo mtu huyo ni Rais, basi taarifa hiyo ya kujiuzulu ataiwasilisha kwa Spika;

(c) iwapo mtu huyo ni Spika au Naibu Spika wa Bunge, basi taarifa hiyo ya kujiuzulu ataiwasilisha kwenye Bunge; na

(d) iwapo mtu huyo ni Mbunge, basi taarifa hiyo ya kujiuzulu ataiwasilisha kwa Spika.

(2) Mtu aliyetoa taarifa ya kujiuzulu kwa mujibu wa masharti ya ibara ndogo ya (1) ya ibara hii, atahesabiwa kuwa amejiuzulu tangu siku ile ambayo taarifa yake ya kujiuzulu itakapopokelewa na mtu anayehusika au kikao kinachohusika au itakapopokelewa na mtu yeyote aliyeruhusiwa kuipokea taarifa hiyo na mtu anayehusika au kikao kinachohusika, lakini kama taarifa hiyo ya kujiuzulu imeeleza kwamba mtu huyo atajiuzulu tangu siku nyingine baada ya taarifa hiyo kupokelewa na mtu anayehusika au kikao kinachohusika, basi mtu huyo atahesabiwa kuwa amejiuzulu tangu siku hiyo nyingine ya baadaye.

(3) Iwapo mtu yeyote mwenye dhamana ya kazi yoyote iliyoanzishwa na Katiba hii (pamoja na kazi ya Waziri, Naibu Waziri au Mbunge, isipokuwa Mbunge ambaye ni Mbunge kwa mujibu wa madaraka ya kazi yake) amejiuzulu, basi ikiwa anazo sifa zote zinazohitajika na kwa kila hali anastahili, aweza kuteuliwa au kuchaguliwa tena kushika madaraka ya kazi hiyo kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii.

(4) Masharti yaliyomo katika ibara ndogo ya (3) ya ibara hii hayatamzuia mtu ambaye ni Rais kuchaguliwa tena kuwa Rais wakati bado ameshika madaraka ya kazi ya Rais.

©2025 Government of Tanzania. All rights reserved. No part of this book may be reproduced or distributed without permission of OAG.

Maelezo kuhusu utaratibu wa kukabidhi madaraka ya kazi katika utumishi wa Serikali
Sheria Na. 14 ya 1979 ib. 12; 1 ya 1980 ib. 16; 15 ya 1984 ib. 52

**150.**–(1) Kwa madhumuni ya ufafanuzi wa masharti ya Katiba hii kuhusu utaratibu wa kukabidhi madaraka ya kazi katika utumishi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano, ifahamike kuwa mtu yeyote mwenye mamlaka, kwa mujibu wa Katiba hii, ya kumteua au kumchagua mtu mwingine kushika madaraka ya kazi fulani anao pia uwezo wa kumteua au kumchagua Kaimu au mtu ambaye atashikilia kwa muda na kutekeleza madaraka ya kazi hiyo:

Isipokuwa kwamba maelezo hayo hayatatumika kwa madaraka ya kazi ya Waziri, Naibu Waziri, Jaji wa Mahakama ya Rufani, Jaji wa Mahakama Kuu, Mjumbe wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora au Mjumbe wa Tume ya Uchaguzi.

(2) Kanuni zifuatazo zitatumika pia kwa madhumuni ya ufafanuzi wa masharti ya Katiba hii kuhusu utaratibu wa kukabidhi madaraka ya kazi katika utumishi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano, yaani-

(a) iwapo kuna mtu mwenye madaraka ya kazi fulani aliyokabidhiwa kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii na mtu huyo yupo likizoni na wakati huo huo anangojea kuacha kazi hiyo, basi anaweza kuteuliwa mtu mwingine na kukabidhiwa madaraka ya kazi hiyo, bila ya kujali kuwapo kwa yule mtu anayengojea kuacha kazi hiyo;

(b) iwapo kuna watu wawili au zaidi ambao kwa wakati mmoja wote wanashika madaraka ya kazi fulani kutokana na uteuzi wao uliofanywa kwa mujibu wa Kanuni iliyoelezwa katika aya ya (a) ya ibara hii ndogo, basi katika hali hiyo kukitokea haja ya kutekeleza shughuli yoyote inayohusika na madaraka ya kazi hiyo yule mtu wa mwisho kuteuliwa ndiye atakayehesabiwa kuwa mtu pekee mwenye dhamana ya kazi hiyo.

©2025 Government of Tanzania. All rights reserved. No part of this book may be reproduced or distributed without permission of OAG.

Ufafanuzi
Sheria Na. 15 ya 1984 ib. 52 na ib 53; 4 ya 1992 ib. 38; 3 ya 2000 ib. 19; 1 ya 2005 ib. 25; TS. Na. 133 la 2001

**151.**–(1) Katika Katiba hii, ila iwapo maelezo yahitaji vinginevyo-

"amri ya jeshi" maana yake ni sheria au amri iliyotolewa kwa mujibu wa sheria, ya kusimamia nidhamu katika jeshi;

"askari" likitumika kuhusiana na jeshi lolote, maana yake ni pamoja na askari yeyote ambaye kwa mujibu wa amri ya jeshi hilo ni mtu anayewajibika kinidhamu;

"Baraza la Wawakilishi" maana yake ni Baraza la Wawakilishi la Zanzibar lililotajwa katika ibara ya 106 ya Katiba hii na linalotekeleza madaraka yake kwa mujibu wa Katiba hii na Katiba ya Zanzibar ya 1984;

"Bunge" maana yake ni Bunge la Jamhuri ya Muungano lililotajwa katika ibara ya 62 ya Katiba hii;

"Chama cha Siasa" maana yake ni Chama Cha Siasa kilichoandikishwa kikamilifu kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Siasa, ya mwaka 1992;

"Jaji Mkuu" maana yake ni Jaji Mkuu aliyetajwa, kuteuliwa na ambaye majukumu yake yameelekezwa katika Ibara ya 118 ya Katiba:

"Jaji Mkuu wa Zanzibar" maana yake ni Jaji Mkuu wa Mahakama Kuu ya Zanzibar ambaye, kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar ya 1984, ndiye mkuu wa Mahakama ya Zanzibar;

"Jeshi" maana yake ni lolote kati ya majeshi ya ulinzi na ni pamoja na jeshi lolote jingine lililoundwa na Katiba hii au kwa mujibu wa Sheria na linalotawaliwa kwa amri ya jeshi.

Sura ya 258 (Toleo la 2002)

"Jumuiya ya Madola" maana yake ni jumuiya ambayo wanachama wake ni Jamhuri ya Muungano, na kila nchi ambayo inahusika na masharti ya ibara ya 7 ya Sheria ya Uraia, ya Mwaka, 1961;

"kiapo" maana yake itabidi ifahamike kwa maana ya kawaida ya neno hilo na ni pamoja na tamko rasmi la namna yoyote linaloruhusiwa kisheria kutumiwa badala ya kiapo;

"kiapo cha uaminifu" maana yake ni kiapo cha kuwa mwaminifu kwa Nchi na kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano;

©2025 Government of Tanzania. All rights reserved. No part of this book may be reproduced or distributed without permission of OAG.

"Maadili ya Kazi ya Jaji" maana yake ni masharti ya kimaadili yanayoongoza mwenendo wa watu wafanyao kazi ya Jaji au ya Hakimu;

"madaraka ya kazi katika utumishi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano" maana yake itabidi ifahamike kwa mujibu wa maana ya kawaida na maneno hayo na ni pamoja na utumishi katika Majeshi ya Ulinzi ya Jamhuri ya Muungano na katika Jeshi la Polisi au jeshi linginelo lilioundwa kwa mujibu wa Sheria;

"mahakama" maana yake ni mahakama yoyote yenye mamlaka katika Jamhuri ya Muungano isipokuwa mahakama iliyoundwa kwa amri ya jeshi; lakini kwa ajili ya ibara ya 13, ya 14 na ya 15 za Katiba hii, itakuwa ni pamoja na mahakama iliyoundwa kwa amri ya jeshi;

"Mahakama Kuu" maana yake ni Mahakama Kuu ya Jamhuri ya Muungano au Mahakama Kuu ya Zanzibar;

Mambo ya Muungano" maana yake ni mambo yote ya umma ambayo yametajwa na ibara ya 4 ya Katiba hii kuwa ni Mambo ya Muungano;

"Mamlaka ya Nchi" ni pamoja na Serikali na Bunge la Jamhuri ya Muungano, pamoja na Serikali na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar;

"Mwanasheria Mkuu" maana yake ni Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano aliyetajwa katika ibara ya 59;

"Serikali" maana yake ni pamoja na Serikali ya Jamhuri ya Muungano, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar au Halmashauri ya Wilaya au ya Mji, na pia mtu yeyote anayetekeleza madaraka au mamlaka yoyote kwa niaba ya Serikali au Halmashauri;

"Serikali za Mitaa" maana yake ni vyombo vya kiserikali vilivyoundwa kwa mujibu wa ibara ya 145 ya Katiba hii kwa madhumuni ya kutekeleza madaraka ya umma;

"Tanzania Bara" maana yake ni eneo lote la Jamhuri ya Muungano ambalo zamani lilikuwa eneo la Jamhuri ya Tanganyika;

©2025 Government of Tanzania. All rights reserved. No part of this book may be reproduced or distributed without permission of OAG.

"Tanzania Zanzibar" maana yake ni eneo lote la Jamhuri ya Muungano ambalo zamani lilikuwa eneo la Jamhuri ya Watu wa Zanzibar na ambalo kabla ya Sheria hii kutungwa liliitwa Tanzania Visiwani;

"Uchaguzi Mkuu" au "uchaguzi unaofanywa na wananchi" maana yake ni uchaguzi wa Rais na uchaguzi wa Wabunge wanaowakilisha majimbo ya uchaguzi unaofanywa baada ya Bunge kuvunjwa;

"Ujamaa" au "Ujamaa na Kujitegemea" maana yake ni misingi ya maisha ya jamii ya kujenga Taifa linalozingatia demokrasia, kujitegemea, uhuru, haki, usawa, udugu na umoja wa wananchi wa Jamhuri ya Muungano;

"Waziri" maana yake ni Mbunge aliyekabidhiwa madaraka ya kazi ya Waziri, isipokuwa Naibu Waziri, na maana hiyo itatumika pia kwa Makamu wa Rais;

"Zanzibar" maana yake ni sawa na maana ya Tanzania Zanzibar.

(2) Kanuni zifuatazo zitatumika kwa madhumuni ya ufafanuzi wa masharti ya Katiba, yaani-

(a) kila yanapotajwa madaraka ya Rais, ifahamike kuwa madaraka yanayohusika ni pamoja na mamlaka ya kutekeleza shughuli na kazi mbalimbali na vilevile wajibu wa kutekeleza shughuli na kazi mbalimbali kama Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano, na pia mamlaka mengine kama hayo au wajibu mwingine kama huo ikiwa imeelezwa katika Katiba hii au katika Sheria nyingine yoyote kwamba mamlaka hayo mengine ni ya Rais au kwamba wajibu huo mwingine ni wa Rais;

(b) kila yanapotajwa madaraka ya kazi katika utumishi wa Serikali, ifahamike kuwa kazi inayohusika ni kazi katika utumishi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano isipokuwa kama imeelezwa vingine, na kila inapotajwa idara ya Serikali ifahamike kuwa idara inayohusika ni idara ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano, isipokuwa kama imeelezwa vingine;

(c) iwapo kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii kuna jambo lolote linalotakiwa litekelezwe au lishughulikiwe

©2025 Government of Tanzania. All rights reserved. No part of this book may be reproduced or distributed without permission of OAG.

na chama chochote cha siasa basi, jambo hilo litatekelezwa au litashughulikiwa na chama hicho kwa mujibu wa utaratibu uliowekwa na chama hicho kwa ajili hiyo, na pia kwa kuzingatia masharti ya Katiba hii au sheria yoyote iliyotungwa na Bunge kwa ajili hiyo;

(d) kwa madhumuni ya Katiba hii, mtu hatahesabiwa kuwa ana madaraka ya kazi katika utumishi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano kwa sababu tu kwamba anapokea malipo ya uzeeni au malipo mengine ya aina hiyo kwa ajili ya utumishi wake wa zamani katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano au katika Serikali yoyote ya zamani ya Tanzania Bara au katika Jeshi la Ulinzi au la Polisi la Serikali ya Jamhuri ya Muungano au Serikali ya zamani ya Tanzania Bara au ya Tanzania Zanzibar;

(e) katika Katiba hii, ila iwapo maelezo yahitaji vingine, kila anapotajwa mtu mwenye dhamana ya kazi fulani kwa kutaja madaraka ya kazi yake, ifahamike kuwa mtu anayehusika ni pamoja na mtu yeyote ambaye ni Kaimu au aliyeteuliwa kwa njia ya halali kushikilia dhamana ya kazi hiyo;

(f) katika Katiba hii, kila yalipotajwa mamlaka ya kumwondoa mtu katika madaraka ya kazi katika utumishi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano, ifahamike kuwa mamlaka yanayohusika ni pamoja na mamlaka yaliyotolewa kwa mujibu wa masharti ya sheria yoyote yanayomtaka mtu huyo au yanayomruhusu mtu huyo kustaafu:

Isipokuwa kwamba maelezo ya Kanuni hii yasifahamike kuwa yanampa mtu yeyote mamlaka ya kumtaka Jaji wa Rufani, Jaji wa Mahakama Kuu au Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali astaafu;

(g) katika Katiba hii, kila ilipotajwa sheria ambayo inabadilisha au kufuta sheria nyingine, ifahamike kuwa sheria inayohusika ni pamoja na sheria ambayo inarekebisha sheria hiyo nyingine au ambayo inaendeleza kutumika kwa hiyo sheria nyingine, ama bila mabadiliko au baada ya kubadilishwa au

©2025 Government of Tanzania. All rights reserved. No part of this book may be reproduced or distributed without permission of OAG.

kurekebishwa, au sheria ambayo inaweka masharti mapya katika sheria nyingine.

Jina kamili la Katiba, tarehe za kuanza kutumika na matumizi ya Katiba hii
Sheria Na. 15 ya 1984 ib. 52

**152.**–(1) Jina kamili la Katiba hii ni Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ya mwaka 1977.

(2) Katiba hii ilianza kutumika tarehe 26 Aprili, 1977.

(3) Katiba hii itatumika Tanzania Bara na vile vile Tanzania Visiwani.

## NYONGEZA YA KWANZA

*(Imetajwa katika ibara ya 4)*

### MAMBO YA MUUNGANO

1. Katiba ya Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Muungano.
2. Mambo ya Nchi za Nje.
3. Ulinzi na Usalama.
4. Polisi.
5. Mamlaka juu ya mambo yanayohusika na hali ya hatari.
6. Uraia.
7. Uhamiaji.
8. Mikopo na Biashara ya Nchi za Nje.
9. Utumishi katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano.
10. Kodi ya Mapato inayolipwa na watu binafsi na mashirika, ushuru wa forodha na ushuru wa bidhaa zinazotengenezwa nchini Tanzania unaosimamiwa na Idara ya Forodha.
11. Bandari, mambo yanayohusika na usafiri wa anga, posta na simu.
12. Mambo yote yanayohusika na sarafu na fedha kwa ajili ya malipo yoyote halali (pamoja na noti); mabenki (pamoja na mabenki ya kuweka akiba) na shughuli zote za mabenki; fedha za kigeni na usimamizi juu ya mambo yanayohusika na fedha za kigeni.
13. Leseni ya viwanda na takwimu.
14. Elimu ya juu.
15. Maliasili ya mafuta, pamoja na mafuta yasiyochujwa ya motokaa na mafuta ya aina ya petroli na aina nyinginezo za mafuta au bidhaa, na gesi asilia.
16. Baraza la Taifa la Mitihani la Tanzania na mambo yote yanayohusika na kazi za Baraza hilo.
17. Usafiri na usafirishaji wa anga.
18. Utafiti.
19. Utabiri wa Hali ya Hewa.

©2025 Government of Tanzania. All rights reserved. No part of this book may be reproduced or distributed without permission of OAG.

20. Takwimu.
21. Mahakama ya Rufani ya Jamhuri ya Muungano.
22. Uandikishaji wa vyama vya siasa na mambo mengine yanayohusiana navyo.

## NYONGEZA YA PILI

*(Imetajwa katika ibara 98(1)(a))*

### ORODHA YA KWANZA

(Sheria ambazo mabadiliko yake yahitaji kuungwa mkono na theluthi mbili ya Wabunge wote)

Sura ya 500, (Toleo la 1965), Sheria ya kuthibitisha Tanganyika kuwa Jamhuri, ya mwaka 1962 [Ibara ya 3, 27, 18, 23 na 26].
Sura ya 508, Sheria ya Utumishi katika Idara ya Mahakama ya 1962 [Sura hii imefutwa na Sheria Na. 2 ya 2005].
Sheria ya Uhamiaji ya mwaka 1995 [Sheria yote]
Sura ya 509, Sheria ya Utumishi Serikalini ya mwaka 1962 [Sura hii imefutwa na Sheria, Na 8 ya 2002].
Sheria ya Uraia, ya mwaka 1995 [Sheria yote]
Sura ya 557, (Toleo la 1965), Sheria ya Kuthibitisha mapatano ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ya mwaka 1964 [Sheria yote].

### ORODHA YA PILI

*(Imetajwa katika ibara 98(1)(b))*

Mambo ambayo mabadiliko yake yahitaji kuungwa mkono na theluthi mbili ya Wabunge wote kutoka Tanzania Bara na theluthi mbili ya Wabunge wote kutoka Tanzania Zanzibar.

1. Kuwapo kwa Jamhuri ya Muungano.
2. Kuwapo kwa Ofisi ya Rais wa Jamhuri ya Muungano.
3. Madaraka ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano.
4. Kuwapo kwa Bunge la Jamhuri ya Muungano.
5. Madaraka ya Serikali ya Zanzibar.
6. Mahakama Kuu ya Zanzibar.
7. Orodha ya Mambo ya Muungano.
8. Idadi ya Wabunge kutoka Zanzibar.

©2025 Government of Tanzania. All rights reserved. No part of this book may be reproduced or distributed without permission of OAG.

©2025 Government of Tanzania. All rights reserved. No part of this book may be reproduced or distributed without permission of OAG.